

MASWALI NA MAJIBU



Na tuinamishe vichwa vyetu. Bwana Yesu, tuna shukrani Kwako asubuhi hii kwa ajili ya nafasi ya kuja katika Uwepo Wako, na wakati huu wa ushirika, na kuketi hapa katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. Sasa, Bwana, twaomba kuwa Wewe utaendelea kuwa pamoja nasi tunaponena kukuhusu Wewe. Na mioyo yetu ijawe na furaha tunapotazama Neno Lako na ahadi Zako kwetu. Mbariki mchungaji wetu, wasaidizi wetu, ndugu na dada wote wanaokuja hapa kukutanika nasi na kukusanyika hapa katika mahali hapa padogo ambapo tumetenga kuwa mahali pa kukutana Nawe. Nasi twaomba kuwa Wewe utatubariki katika kila kitu tunachofanya siku hii yote. Katika Jina la Yesu twaomba. (Mwaweza kuketi).

[Ndugu Branham anaongea na mtu fulani jukwaani—Mh.]

² Hili ni kama pumziko ndogo kwangu kidogo tu. Nilikuwa na ibada nyuma hapa, mahojiano; nilipaswa tu kuwa na mahojiano au wala—au—au kuchukua na kujibu maswali. Karibu kila kitu kilichoingia asubuhi hii kilikuwa maono, na nilikuwa tu na... Nilimwambia Billy, kama Ndugu Neville hakuwa na kazi nyingi sana, ningeshika hiki kifurushi cha maswali na kukimbia hapa, kutuliza mawazo yangu kidogo. Ni—hunishusha sana, kama... Maono hayo—hayo yana... Lakini watu walisaidiwa; hilo ndilo jambo muhimu. Jambo muhimu, walisaidiwa; hiyo ndiyo sehemu nzuri. Na kwa hivyo, ndipo nitayachukua mapema kidogo jioni hii, ili niweze kuanza jioni hii na mahojiano yangu, yale maalum.

³ Sasa, tuna furaha asubuhi hii kuona marafiki zetu na... Sasa, hili... Msimlaumu Billy kwa hili, kwa hivyo ndipo... Yeye anapaswa kuwajulisha watu kama nitaendelea kujibu maswali haya. Nilidhani lingenipa labda sa—saa au nafasi fulani kujibu maswali. Baadhi ya... Napenda—Sipendi kuacha; napenda kufanya mambo yangu dhahiri. Ona? Ndipo maswali haya na mengineyo, nina—ninataka tu kusema, nina—nina—ninafanya hili. Napata mengi sana katika—kwenye nia yangu; yananipa wasiwasi. Nami sitaki kuwa na wasiwasi kuhusu lo lote; nina—ninaenda nyumbani Utukufuni hivi karibuni.

⁴ Rafiki yangu wa kale aliniambia siku kadha zilizopita, kasema, “Nimechoka sana kuishi katika kasha la mkononi.”

Nilisema, “Ndugu mpendwa, nataka kukuuliza kitu fulani; nami nataka kukwambia kitu fulani. Nina tamaa sana ya kwetu. Nimekuwa na tamaa sana ya kwetu kwa miaka ishirini, na sikuwa na nyumbani pa kuenda.” Ona? Hilo ni kweli. Hilo ni jambo baya sana mno kusema. Ningeleti chini na kulia niende mahali fulani nyumbani. Sina nyumbani pa kuenda. Kila mahali niendako, siwezi kuketi pale siku chache; niko tayari kuenda

mahali pengine. Nadhani nimekuwa hivyo; nili—nilizaliwa hivyo. Mke wangu huniita “Upepo usiotulia.” Nina—niko tu hapa na pale. Na hilo ni jambo gumu mno kuwa nalo, lakini nadhani ilinipasa kuwa hivyo kwa ajili ya huduma yangu. Lakini wengi wenu mnapendelea kile... Vema, tunapenda kutenda cho chote kwa ajili ya Mungu, lakini msithubutu kamwe...

⁵ Sasa, sisi tu kundi la watu wa nyumbani tu asubuhi hii. Ona? Lakini nina—nina tamaa sana ya nyumbani. Nataka kwenda nyumbani, nami sijui niende wapi. Unasema, “Na kwenda Arizona je, jamaa yako iko kule?” Natulia kwa siku mbili au tatu, nami yanipasa kwenda mahali pengine. Naenda pale, na ndipo natulia pale kwa siku mbili au tatu, nami yanipasa kwenda mahali pengine. Kwa hivyo sina nyumbani ya kuenda, nami nina tamaa sana ya nyumbani.

⁶ Vema, kuna nyumbani. Nita—nitaenda huko wakati fulani, lakini yanipasa niwasaidie ninyi kwanza. Ona? Hilo ndilo nililo hapa kwa ajili yalo, ni kuwasaidia ninyi. Na hadi wakati huo uje, ambapo sitawasaidia tena, ndipo nina—ninataka kwenda nyumbani. Ninataka kwenda nyumbani kwenyewe wakati huo. Lakini kuna mahali fulani ambapo nitapapenda mno, sitataka kurudi tena.

⁷ Nitaondoka Jeffersonville, sitakuweko kwa majuma machache; nami nataka kurudi tena. Nikienda Arizona; nadhani hilo ni ajabu; ninataka kurudi tena. Nikienda mahali penginepo; ninataka kurudi tena. Nami naenda hapa, naenda pale, nami—ndipo nadhani nataka kuja hapa. Nafika hapa; niko tu hapa kwa siku chache, nami nawaona ninyi nyote; ninataka kuenda mahali penginepo. Ona, nina watoto wangu wametawanyika ulimwenguni kote, nami—ni—ambao nimemzalia Kristo. Nami... Basi sina makao tena. Nataka kuwakusanya wote pamoja mojawapo wa siku hizi (ona?)—Baba atafanya hivyo, kisha tuta—tutakuwa na makao na hatutazurura tena. Ona? Nachoka kuzurura na bila mahali pa kukaa.

⁸ Nami ningemshauri ye yote, asiwe jiwe lifingirikalo (ona?), ijapokuwa ni aina fulani ya huduma inayokuita hivyo, kwa sababu... Ninge—ningetoa cho chote, asubuhi hii, kama ningekuwa na mahali hapa duniani ambapo ningenda na kusema, “Hapa ni nyumbani!” Ninge—ningetoa... Kama ningekuwa napo, ningetoa dolla milioni. Kama ningelikuwa na mahali ambapo ningesema, “Jamani, napenda hapa sana; sitaki kupaacha tena,” ninge—ningetoa cho chote. Lakini si—siwezi kupapata.

⁹ Mimi ni kama Ibrahimu alivyokuwa; nautafuta Mji huo. Ona? Siwezi kuupata, lakini najua uko. Lakini hakika siwezi kuridhika na mahali po pote duniani humu. Hapaonekani kama... Watu wazuri, mahali pazuri, na unaenda hapa, ni chepechepe sana; unaenda nje pale, ni pakavu sana; ukienda

juu pale, ni baridi mno; ukienda chini pale, ni joto mno. Ona? Nawe... Hakuna mahali, si nyumbani. Sitaki kuchukua wakati wangu kulilia mabegani mwenu, lakini nina...

Vema, tuna shukrani kwa Bwana. Amina! Iweni na shukrani kwa mambo yote. Mimi niko hivyo, kwa sababu niko hivyo. Mungu aliniumba vile nilivyo. Nami siwezi kuwa cho chote ila kile Yeye alichonifanya mimi, huzuni, na mambo kama hayo. Wananiambia yanipasa tu kuwa hivyo ili nipate kuwa msaada ambao Yesu alinituma hapa kuwa. Nami nataka kuwa mtu wa aina hiyo. Kama hivyo ndivyo nipaswavyo kuwa, hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Cho chote Ufalme wa mapenzi ya Mungu utakacho, au mapenzi ya Mungu, hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa.

¹⁰ Sasa, hebu na tuombe tena. Bwana Yesu, maswali haya yamewekwa mbele yetu hapa, Baba. Siwezi kuyajibu, Bwana. Mi—mimi sifai kwa maswali haya, lakini najua kuwa Wewe Unatosha Kabisa, kwa sababu yako kwa mioyo ya watu. Nitumie, Bwana, kutuliza msongo wao, sivyo, Baba? Katika Jina la Yesu Kristo naomba. Amina.

Sasa, tutaanza kwa... Nadhani hawanasi haya, kwa hivyo nina... Ni sawa, nadhani.

¹¹ Sasa, jambo moja ambalo... Sababu ya kuogopa maswali kila mara kuna jambo moja kali—jambo moja baya, samahani, ambalo kila mara hunitatiza: hilo ni kujibu swali kuhusu ndoa na talaka. Jamani, simu, mabarua, na ndugu mmoja alijifunika blanketi na kuketi sebuleni mwangu tangu saa sita hata mapambazuko siku iliyofuata. Wahudumu wakipiga simu toka kila mahali wameoa mara mbili au tatu na kadhalika. Wahudumu... Nataka kuwaulizeni jambo moja. Ninayo baadhi yayo ambayo bado yako humu najua. Sijayasoma yote, lakini kunayo kadha ambayo bado yako humu.

¹² Kumbuka tu hili! Kwenu watu mliooa, na kutaliki, na kuoa tena, niahidini jambo moja. Ona? Mmeweka tumaini lenu kwangu. (Nina—ninadhani haya hayanaswi. Si...) Ninyi—ninyi—ninyi ambao—mnaniamini mimi kuwa nabii wenu aliyetumwa toka kwa Mungu, mtumishi wenu, basi kubalini neno langu kuhusu hili, mtafanya hivyo? Endeleeni kuishi jinsi mlivyo. Msijaribu jambo lingine kama hilo, lakini ishini, endeleeni, ishini kwa furaha. Mna... Mmeokoka. Mukiwa Wakristo, endeleeni kumwishia Kristo; Yeye alikuwa na kusudi la kuwaokoa ninyi.

¹³ Sasa, nitakaporudi, Bwana akipenda, nitawaelezea hilo kutoka katika Biblia. Ona? Na msiudhike. Wanaume wengi waliniambia mimi, wakasema, “Vema, nampenda mke wangu, lakini nina—itanipasa tu kuachana naye; si—sitaki kukosa kunyakuliwa.” Msifanye hilo! Kaeni tu jinsi mlivyo hadi mtakaposikia toka kwangu tena (ona?) kuhusu jambo hili. Ndipo

wakati nita- . . . Siwezi kulieleza katika dakika kumi au kumi na tano; litachukua wakati mwingi kulieleza, kwa sababu lapasa liwe Maandiko. Yapasa liwe BWANA ASEMA HIVI. Kama sivyo, si sahihi.

¹⁴ Najua maswali haya ambayo Yesu alisema hapa, “Mtu akimwacha mkewe na amwoe mwingine isipokuwa kwa habari ya uasherati anazini, mtu akimwoa mwanamke aliyeachwa, yuaishi katika uzinzi.” . . . Mambo haya, Yeye alikuwa na sababu ya kusema hivyo. Yeye alikuwa Mungu; hilo ni Neno Lake.

¹⁵ Sasa, hebu turudi mwanzoni tuone nini maana ya haya yote (ona?), ndipo tulieleze wazi-wazi. Lakini hata tutakapotenda hayo, endeleeni tu kama mlivyo sasa, jinsi mmekuwa mkifanya kila mara, mkiwa Wakristo. Kama ninyi wawili mu Wakristo, na mmeoana, na mna watoto, na mambo kama hayo, vifungo vidogo vinavyowafunganisha, usimtaliki mkeo au mumeo sasa. Usifanye hivyo. Ona? Ngojeni hata mtakaposikia tena juu ya jambo hilo. Je, mtaniahidi hilo? Inueni mikono yenu! Sasa, mna matumaini kwangu kuniamini mimi. Sasa, ninyi—ninyi mmeniamini umbali huu; sasa, niaminini zaidi kidogo kwa jambo hili.

Sasa—sasa, hebu tuone, nina mazuri sana hapa asubuhi hii, mengine . . .

325. Je, wote watakaokuwa katika Bibi-arusi yawapasa waishi umbali usiopungua maili elfu moja na mia tano kutoka kwa yale maskani (naamini nilikuwa na hilo Jumapili iliyopita. Nitayachukua na kuyatumia niwezavyo.)—**maili elfu moja na mia tano kutoka kwa yale maskani, kama inavyoonekana kwenye kanda nambari mbili ya “Makao Yajayo Ya Bibi-arusi?” Mimi kila mara nilidhani Bibi-arusi angetoka kila sehemu ya ulimwengu katika wakati wa kunyakuliwa. Je, nimekosea?**

¹⁶ La, rafiki yangu mpendwa, haujakosea, uko sawa. Sasa, kama nilisema lo lote chini ya kanda hiyo ambalo lingewaongoza kuamini ya kwamba . . .

Sasa, sija- . . . Haya yote ni mageni kwangu sasa, sikuyachunguza ha haya hapa. Mwaona? Haya ni kundi jipya nililopata Jumapili iliyopita, na kuyarudisha tena katika bahasha hii, na kuyaweka tena mle ndani.

¹⁷ Sasa, katika hili . . . La, Bibi-arusi si lazima awe mahali fulani po pote. Wengi wao watakuwa katika mavumbi ya nchi. Watakuwa duniani kote; watakuwa wameganda katika—katika theluji kule Kaskazini, na—na wavumbi ya pori za Tropiki, na—na kote ulimwenguni. Lakini Parapanda ya Bwana itakapolia, waliokufa katika Kristo watafufuliwa, wataamka, na kutoka mavumbini, haidhuru wako wapi. Na sasa, katika hili, ufufuo utakuwa wa ulimwengu wote. Ona? Kila mahali kila kiumbe juu

hii ya duara ya dunia kilicho katika Kristo kitakuja pamoja Naye Yeye ajapo (ona?), haijalishi uko wapi.

¹⁸ Waza tu kuhusu vile viwanja vya tamasha katika siku za mwanzoni za wale wafia imani, kwamba wakati hao Wakristo walipotupwa katika tundu la simba, na hao simba wakawaua Wakristo na kula miili yao. Ona? Hata hivyo walitawanyika, miili yao ilikuwa katika takataka za hao simba kote katika uso wa dunia. Haijalishi ni wapi, huwezi. . . Ona, umeumbwa kwa vitu ambavyo havionekani vikafanywa vionekane, na Mungu ata—atarudisha kitu hicho—atakirudisha tena. Ona?

¹⁹ Sasa, kama ukichukua che—chembechembe hai. Unaivunjavunja toka kwa chembechembe, na inakuwa basi che—chembechembe katika chembechembe, kisha ikawa atomi, na kipande kidogo sana cha kitu, na kuendelea hivyo; na mwishowe kinaishia katika visivyoonekana. Kinatoka kwa kitu fulani cha kawaida unachoweza kukigusa kwa mkono wako, kikawa gezi, toka kwa gezi hata madawa—madawa hadi gezi, na gezi, kurudi nyuma hivyo, hadi mwishowe yote yanaishia kwa kitu kimoja kidogo, na hicho ni roho. Na roho huyu ambaye anakaa katika gezi hizi. . . Huenda isiwe gezi zile zile, lakini umbo lako litakuwa jinsi lilivyo tena. Ona? Roho amesimamia nipo.

²⁰ Na sasa, katika maneno mengine, unapokuwa mvulana au msichana, tuseme, Mungu huchukua picha yako. . . Sasa, haijalishi u mzee vipi na umekunjamana vipi, umeumbuka vipi, hata iwe vipi, hilo litaishia moja kwa moja kwake. Na mwili huo huenda ukaharibiwa, kuumbuka, kutekelezwa, kuliwa na simba, lo lote lile, lakini uliumbwa kwa gezi, vitu kumi na sita vya dunia. Hivyo vilikuwa chokaa, shura, na na petroli, na nuru ya duniani, na kadhalika, vyote pamoja huufanyiza mwili ule. Sasa, haijalishi, hilo ni—dunia nzima imejawa na hivyo.

²¹ Lakini sasa, picha hii ndiyo jambo muhimu. Ndipo katika ule ufufuo, gezi zile, na madawa, na vinginevyo vinarudi tena pale na kuumba picha hii tena. Sasa, picha hii haikuchukuliwa wewe ulipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, au kumi na minane, au umri wa miaka ishirini ulipokuwa mrembo sana. Ilichukuliwa lini? Kabla kuwekwa na misingi ya ulimwengu, iliwekwa katika jalada kuu la Mungu. Ndiposa, jambo tu ililofanya ni kujithibitisha hapa ili ufanye chaguo lako. Ona? Ndipo unakuwa mtumishi wa Mungu. Yeye akilijua tangu awali, inamfanya Yeye Mkombozi, kama vile tumekwisha sikia.

²² Basi picha hiyo hakika ni. . . Hii ni picha ya kufanyizia nyingine. Sehemu ya maisha ya picha ya kufanyizia nyingine ndiyo mnayoishi sasa. Na lo lote, kama kuna picha ya kufanyizia nyingine, yapasa kuwe na picha halisi kusijakuwepo picha ya kufanyizia nyingine. Kwa hivyo, kama hii ni picha ya kufanyizia nyingine, yapasa kuwe na picha halisi mahali fulani. Na hiki si

kitu halisi; hiki ni kivuli cha kile kitu halisi kinachokuja. Sasa mlifahamu?

²³ Kwa hivyo sijali kile wangekufanyia; hawawezi kuharibu sura hiyo, picha hiyo iliyo katika ile nyumba kuu ya sanamu ya Mungu kule juu. Huwezi kuiharibu, iko Mbinguni. Ungeuteketeza, kuulisha simba, kuufanyia lo lote utakalo kufanyia; utafufuka tena kwa hakika tu kama mbili mbili ilivyo nne. Kwa hakika tu kama Mungu alivyosema, utafufuka. Kwa hivyo, haijalishi uko wapi. . .

²⁴ Sasa, nadhani. . . nadhani kama utasikiza kanda. . . (Sijui nani aliliandika; hakuna jina lililoandikwa, ni kipande kidogo tu cha kijikaratasi kilichoandikwa kwa vino wa samawati, kilikwanuliwa toka kwa kijitabu kidogo. Inaonekana kama kwamba kimeraruliwa toka kwa kijitabu ki—kidogo.) Lakini kumbuka, kuhusu hili, katika—katika swali hili sasa, katika kanda, kama mtachunguza, nilisema hili, kitu fulani juu ya hili (huenda isiwe neno kwa neno, ukilinganisha kanda hii na ile nyingine): nilisema, “Kwa mfano, sisi tuko hapa asubuhi hii. Mji huu tunaotarajia kuuona utakuwa maili elfu moja na mia tano mraba.” Nilisema, “Huo ungalianzia Maine hadi Florida, na toka Eastern Seaboard maili mia nane magharibi ya Mto Mississippi, maili elfu moja na mia tano mraba.” Nilisema “Itafakarini, papa hapa asubuhi hii, kuna watu wanaoketi papa hapa ambao—ambao wanatoka umbali kama huo, toka maili elfu moja na mia tano mraba, wanaoketi hapa.” Sasa, sijui ambapo Hekalu lile litawekwa duniani, lakini ninawaza kuwa Hekalu lile litawekwa ambapo Palestina iko sasa. Hiyo itakuwa labda juu ya mlima papo hapo. Litajitokeza. Bila shaka, hakutakuwa na bahari tena wakati huo. Ona, ulimwengu huu ni maili 25,000 mzunguko, bali maili elfu moja na mia tano si kitu kwake. Lakini huu Mji mkubwa utawekwa juu ya huu mlima wa maili elfu moja na mia tano mraba.

²⁵ Sasa, sababu ya kuamini hili ni kwa sababu ya unabii na mengineyo kuhusu ule Mlima Sayuni katika Yerusalemu na miji hiyo. Na hapo ndipo nabii Ibrahimu alipokuwa akiutafuta Mji huo, na ulikuwa ambao Mwenye Kuubuni na Kuunjenga ni Mungu. Yeye aliutafuta Mji huo katika nchi hiyo. Naamini utakuwa ilipo nchi hiyo.

²⁶ Nchi hiyo, ni vigumu kuipata kwenye ramani. Ni nukta ndogo. Na tazama nchi ya Urusi na Marekeni, Amerika Kusini, na mahali pale pote kule. . . Mbona Mungu anapafanyia bidii sana mahali pale (ona?), mahali hapo pamoja? Hilo ndilo swali. Siwezi kulithibitisha, lakini yaonekana hivyo tu kwangu. Lakini hata iwe wapi tunaelekea huko, kwa hivyo Bwana asifiwe kwa hilo.

²⁷ Sasa, kama una wazo kuwa nili—ya kuwa nilisema ingekuwa katika—maili elfu moja na mia tano kuzunguka maskani haya,

hilo lilikuwa wazo baya (Mwaona?), kwa sababu haitakuwa hivyo. Maskani haya yana... Hapa ni mahali padogo tu patakapoangamizwa. Na—na ulimwengu utateketezwa, na haya yote yataangamizwa. Na Indiana hii, na Marekani, na kila kitu kitayeyuka tu kama nta hata kiwe tu mawe ya volkeno. Ona? Dhambi zote, magonjwa yote, viini vyote, kila kitu kitaangamizwa. “Nami nikaona Mbingu Mpya na Nchi, kwa maana ya mbingu ya kwanza...”

²⁸ Waza! Mungu alichukua miaka elfu sita katika akijenga ulimwengu huu, kuuweka pamoja, kuumba. Yeye aliuumbaje? Biblia ilisema, “Yeye aliumba kwa vitu visivyo dhahiri”; hiyo ni kusema, Yeye aliuumba nchi. Sasa tazama; hili ni zuri. Muumba aliyeumba dunia kwa kusudi fulani—Shetani aliichafua—Yeye alikuja kukomboa kile kilichosalia juu hapa. Na Yeye ameenda mahali penginepo na bado angali katika shughuli Zake za uumbaji.

²⁹ Sasa, ilimchukua Yeye miaka elfu sita kuumba nchi, na Yeye atachukua siku mbili kuumba Mji ule ujao duniani. Yeye ana... “Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi: kama sivyo, singaliwaambia. Ninaenda kuwaandalia mahali (kuujenga mji kwa dhahabu inayopenya nuru, barabara za dhahabu).” Ni mahali pazuri jinsi gani.

Yeye angeipata wapi? Je, kuna vitu vya kuujengea katika dunia zingine, au miezi, nyota, na kadhalika? Yeye haimpasi kuwa navyo, Yeye ni Muumba. Yeye ameenda kuujenga Mji huo. Amina! Hilo ni zuri kutosha kwangu, sivyo kwenu? Hilo ni zuri. Kwa maana kama Yeye aliujenga huu, nami naufurahia huu, itakuwaje yeye atakapoujenga huu mpya? Jamani, ni jambo la ajabu vipi. Na kwa hivyo nina furaha kuwa tunaeelekea kwenye Mji huo. Vema.

326. Ndugu Branham, nampenda Bwana, lakini kwa mwaka uliopita nimekuwa—nimekabiliwa na shida. Yaonekana wakati wingine nusuru nirukwe na akili. Ni nini? Tafadhali niombee pamoja na mume wangu.

³⁰ Vema, kama hakuna... Kama mtu huyu alikuwa kwenye mahojiano ya kibinafsi, kama vile ninyi watu mmekuwa mle asubuhi hii, yangevuta hicho kijitokeze. Ona? Bwana angefunua hicho. Lakini sasa, kwa kuwa sijui wewe u nani, na huketi hapa; lilisema tu, Dada katika Kristo...

³¹ Sasa, sasa, kama ni—kama kuna jambo fulani baya ambalo umefanya, ambalo linakusumbua, basi lichunguze kwa Biblia na uone kile kikupasacho kufanya. Lakini kama hujafanya lo lote na hauhukumiwi kwa lo lote, labda ni neva zako. Ona? Yaweza kuwa ni mambo mengi yaliyotendeka: labda shida fulani kule nyuma maishani mwako. Labda ni—mwanamke hapa huenda akawa katika wakati wake wa kuingia ugumba. Hapo ndipo kila kitu humwendea vibaya, na hana kitu, bali kila kitu

kimemwendea mrama. Naye hajifanyi, yeye hakika hujisikia hivyo; ni kweli anasikia. Mtu ye yote aliye na wasiwasi yuko hivyo. Basi msigombane kamwe.

³² Nanyi waume kwa wake zenu, wakiwa katika wakati huo wa maisha, ukiwahi kamwe—kama hajapata kuwa mpenzi wako, umwache yeye awe wakati huo, kwa sababu yeye anakuhitaji. Yeye hakika anahitaji msaada wako; yeye anahitaji mtu wa kumsaidia, na kumwelewa. Kuongea pamoja naye, mchukue mikononi mwako kama—kama—kama kwamba yeye ni mpenzi wako, naye apaswa kuwa. Na—na umwelewe, kwa sababu yeye anapitia katika wakati ambao mwili wake wote unabadilika, na yakupasa uwe mwema kwake wakati huo.

³³ Nadhani hiyo ndiyo sababu Bw. Rockefeller alifanya kosa kubwa sana. Yeye alipendwa na taifa, labda angekuwa rais wetu anayefuata. Lakini mke wake alipoingia katika wakati wa ugumba, na kuingia katika ugumba, yeye alimwacha akamwoa karani wake, mwajua nini kilitendeka? Hilo laonyesha kuna Waamerika wengine ambao bado wana mawazo mazuri.

Sasa, nampenda Bw. Goldwater, au—au Bw. [Ndugu Branham adata vidole vyake—Mh.] Rockefeller. Yeye... nampenda Bw. Goldwater pia; nampenda kila mtu. Lakini si—sikutaka ku... Baadhi yenu—baadhi ya ndugu zangu wa chama cha Republican wakiketi pale wakinisikia nikisema hilo, nina—...

³⁴ Tazama, lakini mimi si mwanasiasa, ni—ninataka kuwa Mkristo. Ona? Na hapa si mahali pa siasa. Ona? Kitu hicho chote kimekwisha haidhuru, hivyo, lakini haya tunayoongea juu yake ni ya Milele. Democrat au Republican... Ee, ni mchafuko mno; haviwezi kamwe kukombolewa. Vimekwisha, kwa hivyo usibishanie hilo. Jambo la kufanya ni kuishia Ufalme huu. “Maana hatuna mji udumuo, bali twautafuta Ule ujao.” Amina! Naam, bwana!

³⁵ Kwa hivyo siasa ni upande mmoja wa ua, nami niko upande mwingine. Nilisema “Nili—nilipiga kura mara moja; hiyo ilikuwa kumpigia Kristo; nina hakika nitashinda.” Naam. Ona? Una kura inayokuja. Ona? Mungu alikupigia wewe kura, na shetani alipiga kura dhidi yako. Sasa, upande unaopigia kura ndio unaotokea.

³⁶ Kwa hivyo—kwa hivyo sasa, naamini mtu huyu ana... Nadhani kuwa huo ni wasiwasi tu. Kama hakuna lo lote linalokuhukumu endelea na kusema tu, “Niondokee, Shetani!” Endelea tu. Jitahidi umwishie Mungu.

327. Je, kuna hali yo yote ambayo inaruhusu kuoa tena baada ya talaka kulingana na (Sasa, nitaona kama hili ni... nafikiri kuna maswali mawili matatu juu ya hili.)—**kulingana na Maandiko? Kama si—kama sidumu katika ndoa katika—toka wakati uliopita, ni—je, kunayo sababu yo yote ya**

kutaliki inayokuruhusu uoe tena? Nita—nita (n—u—nu—)—nitnunua kanda hii (Naam!) kupata jibu hili. Asante sana. Nitaitafuta Jumapili.

³⁷ Vema sasa, nimesema hili, mwaona. Msi—msi...mi—mimi... Hebu niache hilo pekee (mwaona?) hadi tutakapofikia mahali ambapo—sasa ambapo—hili lote litakaponyoshwa. Na sasa, kumbukeni tu, hilo ni Mungu akipenda, mara tu nirudipo tena. Nitakapokuja, Bwana akipenda, nitahubiri juu ya jambo hilo. Ona? Na sasa... Ndiposa, tutainasa haidhuru. Na kama—kama itadhuru, idhuru; kama itaeleza dhahiri, ieleze basi. Lakini uwe na moyo wa ushujaa. Ona?

328. Mpendwa Ndugu Branham, je inawezekana mtu awe na ubatizo wa Roho Mtakatifu na ishara zisifuatane naye, hata-hata kidogo hadi wa—wakati fulani ujao na hali zilizokusudiwa na Roho?

³⁸ Sasa, hilo huenda likaonekana kama swali lililovurugika, lakini hilo ni zuri, zuri sana. Ona? Sasa, hapa lanipa nafasi kidogo, nipate kujua yanayotendeka katika jamaa ya—yangu hapa sasa (ona?), nakusudia ninyi, jamaa yangu, na jamaa kule ulimwenguni ambamo tume—ambapo kanda zetu huenda.

³⁹ Sasa, sehemu kubwa ya waumini wangu ni ya Wapentekoste, na kwa sababu Pentekoste ndio ujumbe wa hivi majuzi sana tulio nao katika mambo ya kidhehebu. Na kwangu mimi, hakika nakubaliana nao kuliko kanisa lo lote la kidhehebu. Naegemea upande wa Wapentekoste, kwa sababu ni—ujumbe wa majuzi. Na waongofu wangu wote ninaowaletea Kristo, ninajaribu kuwaelekeza kwa baadhi ya makanisa ya Kipentekoste. Lakini nimewashutumu kwa kila njia niliyoijsua, kuwa wamekosea katika Maandiko kwa kuunda dhehebu na hawataki kuenenda Nuruni wakati Nuru inapotolewa kwao. Hata hivyo, kama ilinipasa kufanya kuchagua leo kuchukua kanisa lo lote ulimwenguni, ningechukua la Kipentekoste tukinena kuhusu dhehebu. Lakini kuhusu watu binafsi, kama wanaume na wanawake, kuna Wakristo halisi katika madhehebu hayo yote; Methodisti, Batisti, Presbiteria, Walutheri, na kadhalika. Lakini ninaongea kuhusu miongozo watu hawa waliyomo, si mtu binafsi kamwe, lakini miongozo ambamo watu hawa wamenaswa katika madhehebu yao...?... Mnaelewa hilo dhahiri sasa (ona?), kwamba na—nadhani watu... Kama wao ni Wakatoliki wa Kirumi, Mashahidi wa Yehova, wa Dini ya Kiyahudi, hata wawe nini, hilo si hoja kwangu; lakini watu binafsi ndio ambao Kristo aliwafia kuwaokoa.

⁴⁰ Na sasa, nina... Na kukubaliana na mipango yao kuwa ni... naamini kuna Wakristo wengi nje kule katika Batisti, kama walivyo katika Methodisti, au Presbiteria, au lo lote lile. Wao ni Wakristo, waamini halisi. Na kule nje katika kanisa Katoliki la Kirumi kunao watu halisi ndani mle ambao

ni wanaume na wanawake halisi wanaompenda Bwana. Nao hawajiungi na kanisa hilo wakosee, wanajiunga nalo kuwa sahihi. Lakini ni mwongozo ndani mle unaoongoza nia zao kwa njia mbaya. Na kukifikia wakati ambao ningeunda dhehebu, nimewadanganya na kuwaleta katika mwongozo; na iwe mbali nami. Na Mungu anilinde niwe na akili timamu kuwaelekeza ninyi kwa Yesu Kristo, yule Neno. Kaeni na Hilo. Ona?

⁴¹ Lakini sasa, mtu huyu hapa anauliza swali kuhusu uwezekano wa kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu bila ishara kufuatana nao. Sasa, ingekuwa... Kama umezaliwa mara ya pili una—kama umezaliwa kwanza kama mwanadamu na mwanadamu wa kawaida... Sasa, ninajibu hili katika—katika—njia ya kitoto mno ya kulijibu. Lakini kama umezaliwa mwanadamu wa kawaida, bila shaka utafanya mambo ambayo mwanadamu wa kawaida wangepanya. Sivyoy?

⁴² Unapozaliwa kama mwanadamu, tabia za kawaida za mwanadamu zitafuatana nawe. Hutaishi katika mti, na kujaribu kuruka kwa mabawa yako kama ndege, au—au—au kitu kama hicho. Hiyo si—hiyo haingekuwa mwanadamu halisi, matendo ya mwanadamu halisi. Tabia halisi ya mwanadamu halisi ingekuwa kufanya kazi, kuwa... kuo, kuwa na jamaa, na kufanya mambo haya. Huyu ni mwanadamu wa kawaida, wanadamu halisi—halisi, kwa sababu unazaliwa hivyo. Ndipo unapozaliwa Mkristo, unapozaliwa kwa Roho wa Mungu, huna budi kuchukua tabia ya Kristo. Mwaona?

⁴³ Sasa, tukitazama hapa asubuhi hii katika kusanyiko hili ambamo ninyi watu huketi hapa na kusikiza siku baada ya siku na kadhalika, mtatambua kuwa mngekuwa tofauti ninyi kwa ninyi, kwa sababu mko—mko tofauti. Mna—mmeumbwa tofauti; tamaa zenu—zenu ni tofauti; mnakula tofauti; lakini ninyi nyote hula chakula. Lakini sasa, tangu tu... Na mtu binafsi akiwa tu kama mwingine, mnatofautiana. Wakristo hufanya jambo lile lile. Hamwezi kusema, “Sasa wote...” Je, wote hunena kwa lugha, je wote hutabiri, je wote...? Ona?

⁴⁴ Yawapasa mchunguze mambo haya, kwa sababu Mkristo huchukua—huchukua tabia za Mkristo; naye huishi kama Mkristo. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Tazama: “Kwa Jina Langu watatoa pepo; watahika nyoka au... kunywa vitu vya kufisha; nao watanena kwa lugha mpya.” Na—na mambo haya hakika huwafuata Wakristo.

⁴⁵ Sasa, mtu yule ana kitu kizuri mno hapa: “...au tungoje hadi wakati ujao au hali iliyokusudiwa na Roho Mtakatifu?” Napenda hilo. Ona? Sasa mwafahamu wazo lile? Itakapokusudiwa Roho Mtakatifu! Mungu hupanga mambo.

Na pale, nadhani kama Wapentekoste wangeparibu (wanaosikiza kanda hii), mtanifahamu mimi kama mtapata hapa sababu ya mimi kutofautiana nanyi mnaposisitiza wazo

hilo kwamba lazima wote wanene kwa lugha. Si—siwezi kuona hilo sahihi, kwa sababu ingekuwa... Napenda sambusa ya matunda, lakini hakuna haja—nami ni mwanadamu—lakini hakuna haja mimi kujaribu kuwaambieni ninyi, “Msipokula sambusa ya matunda, ninyi si wanadamu.” Ona? Lakini kula sambusa ya matunda ni mojawapo ya tabia za mwanadamu. Ona? Huenda usikubaliane nami juu ya hilo, lakini—lakini ni—ni kweli. Sasa, mmoja atakula hiki, na mwingine atafanya jambo lingine.

⁴⁶ Sasa, Roho Mtakatifu huchagua huduma hizi, lakini unapojaribu kujisukumiza mwenyewe ndani yake... Kama nilisema ilikupasa ule sambusa ya matunda, vipi kama sambusa ya tunda ilikufanya utapike, na... ?... Ona? Una—una—unajidhuru mwenyewe, na hivyo ndivyo unavyojaribu kufanya unapojaribu kujilazimisha kufanya kitu kilicho kinyume cha Roho. Yeye amekusudia maisha yako jambo fulani. Je, Mnafahamu hilo? Ona?

⁴⁷ Nanyi, mnapojazwa na Roho Mtakatifu, hapa kuna mojawapo ya ishara bora nizijuazo: unampendana sana na Kristo na kuamini kila Neno ambalo Yeye asema kuwa ni Kweli. Ona? Hiyo ndiyo ishara kuwa umempokea Roho Mtakatifu. Na maisha yako yamejawa na furaha, na—na lo, kila kitu ni tofauti (ona?) kuliko vile ilivyokuwa. Huyu ni Roho Mtakatifu.

⁴⁸ Sasa, karama hizi ziko katika Roho Mtakatifu. Sasa, kama kusanyiko hili asubuhi hii, hili—ni kanisa nzuri sana lenye raha lililojawa na... (Vyumba vya pembeni, hakika vimejaa.) Lakini katika... Ni... (Hatukutangaza tutajibu maswali haya, lakini watu hawa wameingia tu sasa hivi). Tazama, kama kila mtu ndani humu angekuwa katika upatanifu mkamilifu na Roho Mtakatifu, kila mmoja wenu amejazwa Roho Mtakatifu na yuko katika upatanifu na Roho Mtakatifu, ishara hizi zingekuwa tu zi—zikiongezeka kati yenu wakati wote (ona?); ingekuwa tu kila mara ikiendelea. Lakini wakati kuna farakano, ambapo kuna tofauti, na ambapo tumeketi, Roho Mtakatifu hawezi kutenda kazi. Mwaona? Hawezi kutenda kazi kupitia kwa watu. Ona?

⁴⁹ Na pale, kama nilisema, “Sasa ninyi, kila mmoja wenu, je, mlinena kwa lugha?”

“Naam.”

“Vema, mumepokea.” “Je, mlinena kwa lugha?”

“La.”

⁵⁰ “Haujampokea.” Sasa, najifanya hakimu. Mungu ndiye Hakimu wa mambo haya.

⁵¹ Lakini tazama, Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao.” Ona? Makundi yanayoamini, tabia zote za Roho Mtakatifu zinapitia ndani yao, nao wote wamejawa na upendo, na furaha, na—na kundi kubwa tu la—la—la—la watu waliojawa utauwa.

Ona, huyo ni Roho Mtakatifu. Na ndani—ndani mle, wao hunena kwa lugha katika wakati ambapo lugha hutukia (naam), au unaofaa kwa hayo, wao hunena kwa lugha. Na kama kuna unatolewa, unanenwa. Jamani, hakika ni kamili kila wakati.

⁵² Waulize wale watu kumi na watano au ishirini walioenda ndani mle katika mahojiano asubuhi hii kama kulikuwa na neno moja vyo vyote, lililokosea katika njia yo yote, na ni wageni kabisa. Yale—yale Roho Mtakatifu alichimbua mle ndani kabisa, na kupata mambo hayo, na kuyafichua na kuwaambia hao. Ona, ona? Hakuna kosa ndani yake kawaambia vivyo hivyo jinsi *hili*, na jinsi *hili* lilivyokuwa, na jinsi *hilo* lilivyo, na jinsi *hili* lapaswa kufanywa, mambo kama hayo, na yale wamefanya, na yale yanayowapasa kufanya. Ona? Hilo tu ni. . . Kuliweka moja kwa moja katika taratibu. Sasa, yawapasa kushugulikia hayo.

⁵³ Usiku uliopita nilikuwa ninamzungumzia mtu na mkewe, nami nilikuwa kule nyu—nyumbani ambapo tulikuwa na mkutano, au tu—ilikuwa tu kuketi mezani na kuongea. Na kwa ghafula, Roho Mtakatifu alishuka kati yetu, nami nilimwambia—mtu fulani pale, “Nalimwona mtu *fulani*, nao—yeye alikuwa amevurugika niani mwake kuhusu mambo fulani,” nami nilisema, “kama katika tatanisho katika—katika—katika upambanuzi.” Nilisema, “Sasa iko papa hapa sasa.” Nilisema, “Najua unalowazia.” Nami nilirudi nyuma na kuchukua njia ya kandokando na kujibu kila swali mtu huyo alilokuwa nalo niani mwake juu yake kuwa yeye. . . Hakuna ye yote alijua hata yale niliyokuwa nikinena ila yeye. Ona? Lakini yeye alilipata. Yeye alijua habari zake zote. Mwaona? Na hayo yalikuwa nini kwake? Yakimwonyesha, yakimthibitishia kuwa Roho Mtakatifu alikuwa akinifunulia yale yaliyokuwa kwenye nia yake. Mwaona? Nami haikunipasa kuwaambia yaliyosalia. Mwanamume yule yuko ananisikiza hivi sasa. Naam, hiyo ni kweli. Sasa, mwaona jinsi hilo lilivyo? Hilo ni thibitisho.

⁵⁴ Sasa, kama kanisa lote lingefanya kazi katika upatanifu hivyo, basi kati yetu tungekuwa tukitoa pepo, kushika nyoka, kunywa vitu vya kufisha, na mambo ya kila namna yakiendelea. Lakini unapojaribu kusukumiza hilo watu binafsi, basi unajikuta. . . Huo ni Upentekoste tena. Ndio unapata Babeli, mchafuko. Huwezi kuamua hilo. Ona? Mioyo yenu imejawa furaha na raha, naam, jamani ndege wanaimba, ule. . . Kila kitu ni cha ajabu, lo, umejawa tu na Roho wa Mungu, nasi tuko tunampenda sana Yesu, tunataka kuomba usiku wote.

⁵⁵ Sasa, singehangaisha kundi hili, wala hata nami mwenyewe kwenu. Lakini nashangaa, kama ningeuliza swali hili asubuhi hii ni nani katika kundi hili, au watu hawa aliyekuwa na Roho Mtakatifu, labda asilimia tisini na tano kati yenu mtainua mikono yenu kuwa mlipokea Roho Mtakatifu. Kisha ningegeuka na kuwapa ninyi ushahidi wa Biblia—mmoja tu—ishara ya Biblia; nami nashangaa kama kungekuwa na mkono mmoja au

miwili iliyoinuliwa juu. Ona, ona? Inge—ingewafunga katika mahali fulani, lakini unapofanya hilo (ona?), pia unaumiza kusanyiko lako. Lakini yawapasa uwaondoe katika utoto na kuwapeleka katika uwanaume. Ona?

⁵⁶ Kama mtu fulani alivyoandika swali hivi majuzi, alikuwa juu hapa, kasema kuhusu—kasema jambo fulani juu ya Ndugu junior jackson. Mtu fulani alienda chini kule, nao walisema, “Unaenda chini kule kwa ‘maharagwe mafu,’” au kitu kama hicho. Ndugu Jackson... Kwa sababu kusanyiko la Ndugu Jackson, wanawaacha tu wao wanene kwa lugha kanisani. Po pote wanaposikia Roho na wanataka kunena kwa lugha, wao wanaendelea na kufanya hivyo. Vema, hilo ni kanisa la Ndugu Jackson. Hilo ni sawa kabisa. Sina lo lote dhidi ya hilo, hata kidogo. Junior Jackson ni mmoja wa marafiki zangu wapendwa sana, na mtu mcha Mungu, aliyejazwa Roho wa Mungu, na sisi tu ndugu. Sasa, yeye si lazima ale sambusa yangu ya matunda, naweza... Au hainilazimu mimi kula sambusa yake ya tofaa (ona?), lakini sote wawili tunakula sambusa. Sisi sote tunaamini Ujumbe huu vivyo hivyo. Hiyo ni taratibu ya kanisa. Nilisema, “Nataka kanisa langu kujaribu kukusanyika.” Nilisema... Tunapoanza kunena nje hapa, Roho Mtakatifu akinena kwa lugha na kadhalika, nilisema... Mtu fulani aliniuliza, akasema, “Sasa, Ndugu Branham, je hayo yote ni ya kweli?”

⁵⁷ Nilisema “Mimi si hakimu.” Nilisema, “Hebu niwaambieni, hebu tuilete hadi mahali fulani. Hebu iendeleo kidogo na tuilete hadi wakati Neno litakapotolewa juu yake. Ndipo itazame. Kama ni Roho Mtakatifu, inalingana moja kwa moja na Neno; kama sivyo, haitalingani.” Ona? Hivyo ndivyo tu unavyoweza kuitambua; ndipo ina—inajihukumu yenyewe. Mwaona? Vema, ita—itavurugika kama si Roho Mtakatifu, itapukutika. Bali kama ni Roho Mtakatifu, itaingia moja kwa moja mstarini, kwa sababu hivyo ndivyo ilivyo; ni Roho Mtakatifu akiendelea moja kwa moja kwa taratibu Yake Mwenyewe.

⁵⁸ Sasa, katika kunena huku kwa lugha na kadhalika, laiti kila mmoja angelinena kwa lugha. Hakika. Na mara nyingi, Wakristo wazuri...

⁵⁹ Mwaona, kama nakiwaambia hilo lilikuwa kwenye mpango... Nilipata mtu fulani—si mpango, kuniradhi—kwenye mahojiano asubuhi hii. Mtu fulani (nadhani wao bado wako hapa jengoni humu) ambaye wao... Kuhusu kunena kwa lugha... Mtu yule ni mtu wa kweli, mtu halisi, nao wameishi maisha mema. Nao wamenisikia nikisema ishara ya Roho Mtakatifu haikuwa kunena kwa lugha—na sivyo ilivyo—lakini nilimshauri mtu huyo amsihi Mungu awaruhusu wanene kwa lugha au watoe unabii, kwa sababu ni ile tabia.

⁶⁰ Kwanza, nilimwendea mtu huyo na kupata mahali walipozaliwa, na walizaliwa chini ya ishara gani, nami ningejua

mahali walipozaliwa. Jinsi walivyo katika hali yao ya kawaida inawaelekeza katika hali fulani. Kisha, wanapozaliwa mara ya pili, wako hapa katika tabia nyingine. Na ndipo, unapoichuguza tabia hii, hiyo ni upande wa ndani, dhamiri iliyo ndani, dhamiri ya ndani. . . Dhamiri ya nje inakupeleka katika njia moja; hiyo ni kuzaliwa kwako kwa kawaida. Ndipo watajibunia kitu fulani na inawaweka wapi? Chini ya nne, na kuwaweka katika hali ya kufarakanika. Hawajui la kufanya. Watasema, “Bwana ananitaka mimi nifanye *hili*.”

⁶¹ Upande wa ndani. “Ee, ni—ninajua tu ni—ni—ni—linalingana na Maandiko.” Nao wataanza kulifanya, na muda si muda, Shetani humu nje atawaonyesha kila namna ya makosa ndani yake. Na ndipo wao husema, “Vema, nadhani. . .” Ona, Ona? Wanamsikiza Shetani. Ona? Yakupasa uchukue hicho kitu fulani cha ndani, hicho kilicho ndani yako ndicho kilicho cha Maandiko. Na usimruhusu Shetani asimame mahali po pote. Ni—huo ni wajibu wake kusimama pale na kukutwanga hivyo. Lakini usimsikize.

⁶² Lakini watu wale niliwaambia. Wao walisema, “Vema sasa, laiti ningelikuwa na hakika ya kuwa na Roho Mtakatifu.” Ona? Mtu mzuri, mtu mwaminifu sana mwenye Roho Mtakatifu, lakini ingekuwa vema kwake kusema, “Baba, nipe tu hiki niwe na jambo la kutegemea.”

⁶³ Sasa, kama ningeifundisha hivyo, watu wangechukua hicho bila kuwa na kile mtu huyo alichu nacho? Ona? Roho Mtakatifu hunena kwa lugha, bali yakupasa uwe na Roho Mtakatifu kwanza kabla hujanena kwa lugha. Sasa mnalifahamu? Kwa hivyo ukichukua karama ya kunena kwa lugha pasipo. . .

⁶⁴ Sasa kumbuka, hicho chaweza kuwa kipawa halisi; huyo aweza kuwa Roho Mtakatifu akinena ndani yako kwa lugha zisizojulikana, na ungepotea na uende kuzimuni. Biblia ilisema hivyo. Mnaamini hilo? Je, mnetaka Andiko kwake? Mkitaka Andiko; inueni mikono yenu. “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika (sivyo? Zote mbili zinazoweza kufasiriwa na zile zisizoweza kufasiriwa, lugha halisi za Roho Mtakatifu), mimi si kitu.” Ona, isipokuwa hayo mengine yaambatane nayo. Unaweza kuwa na *hiki* (ona?), kwa hivyo usichukue *hicho* bila *hiki*. Pata *hiki* kwanza, ndipo *hiki* hakika kitakifuata.

⁶⁵ Sasa, mvua hunyea wenye haki na wasio haki. Jua huangazia waovu na wema. Mvua hunyesha kuivisha mimea; huivisha magugu pia; mvua ile ile. Roho Mtakatifu anaweza kuwashukia kundi la watu, na kunena kwa lugha, na kuifanya kweli hasa, ataenea kati ya watu, na kuwafanya watoe unabii, na uwe kweli hasa. Hiyo ni kweli hasa.

⁶⁶ Wakati mwingine unaweza kwenda kwa—kwa mganga na mchawi, nao wanaweza kukwambia kitu fulani kilicho kweli

hasa. Mtazame yule mchawi wa Edori. Sauli . . . Huenda ikawa kweli kabisa; bali hiyo siyo. Wao ni wachawi. Kunena kwa lugha, nimeshaona pepo wakinena kwa lugha, na kuandika kwa lugha isiyojulikana. Hilo halimaanishi lo lote. Lakini jambo halisi ni Neno hilo tena. Rudi kwa Neno hilo!

⁶⁷ Kwa hivyo, unaweza kufanya mambo haya bila Neno. Lakini upatapo Neno, na linafanya hivyo basi litazame likitimia kabisa, jambo sahihi hasa. Ona? Ndipo uko sawa.

⁶⁸ Naam, Roho Mtakatifu huwatumia watu hawa kama ilivyokusudiwa kwa hekima Yake Mwenyewe ya Kiungu. Lakini kwanza . . .

⁶⁹ Sasa nini? Hebu niwape tu kikazio kidogo hapa kwa dakika chache. Ningesema, “Wangapi wana Roho Mtakatifu?” Nyote inueni mikono yenu. Ningesema, “Vema, nitaona kama mnaye.” Biblia ilisema kuwa wale waliompokea Roho Mtakatifu waliugua na kulia mchana na usiku kwa ajili ya machukizo yaliyofanywa mjini. Sasa, mikono mingapi ingenda juu? Wangapi wenu hawawezi kupumzika usiku mzima, wamejawa na furaha, nguvu za Mungu, na wana huzuni mwingi kwa ajili ya watu waliopotea, ambao mchana na usiku huugua na kulia kwa ajili ya machukizo? Hutaweza . . . Ona? Huyo angekuwa nani mjini? Wangapi walioko ambao—kanisani? Hiyo ndiyo Biblia ilisema ni ishara ya Roho Mtakatifu.

⁷⁰ Yeye alimwambia yule Malaika wa kutia mhuri (Ezekieli 9, papa hapa), Yeye alisema, “Chukua . . . Pitia katika mji na ukatie alama juu ya wale wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yanayofanyika katika mji ule. Wengine wote, acha yule Malaika wa kuangamiza awaangamize.” Haidhuru wao walikuwa washiriki jinsi gani na walikuwa wamefanya mambo mangapi, kasema, “Tia . . .” Na mtu aliyekuwa—kidau cha wino cha mwandishi, aliyevalia vazi jeupe (ambalo llinawakiliisha Roho Mtakatifu) akajitokeza na kutia alama juu yao wote waliougua na kulia kwa ajili ya machukizo yaliyofanywa katika mji huo. Sasa, unasema . . . Na tazama kile yeye alisema ndani mle pia. “Waueni kabisa, watoto wachanga, mama wazee, watoto wachanga, waueni wote!” Watoto wachanga? Naam!

⁷¹ Yoshua alipoingia katika nchi ya Kanani, yeye alisema, “Msiache mmoja wao hai. Kama ni kitoto kidogo, Mwameleki mdogo, au Mwamori, kiue! Mkumbuke yeye atakua awe Mwameleki; yeye atachafua kambi.” Na hivyo vitu vidogo virudipo hivyo na kutokubaliana na Neno la Mungu, ondoa kitu hicho. Sijali u wa dhehebu gani.

⁷² Mnasema, “Vema, wao ni wazuri . . .” Sijali watu wale ni wazuri vipi! Kama wanaenda kinyume cha Neno hilo, ondoa kitu kile ndani yako. Ni Mwameleki mdogo anayekua. Laonekana nzuri, laonekana lisilo na hatia; laonekana kama ni kweli, lakini usiwe na uhusiano wo wote nalo. Liondokee.

⁷³ “Vema, Ndugu Branham, ni—ninaenda chini hapa, kwa sababu... Vema, si-...” Kumbuka tu, Mwameleki ye yote, lo lote linalokana Neno, liondokee; usiwe na uhusiano wo wote nalo kabisa! wangapi wanaamini hiyo ni Kweli? Hakika. Ona? Liondokee kabisa.

⁷⁴ Wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanyika mjini... Unaona hilo wapi? Naweza kuwaonyesha makumi elfu wanaonena kwa lugha kwa mmoja aliyelemewa kabisa kwa ajili ya dhambi... ambao hata hawawezi kuomba kwa saa moja. Lakini je, mlijua Biblia ilisema kuwa... watie alama wale pekee wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yaliyo mjini. Wangapi waliwahi kusoma haya? Hakika! Huyu alikuwa ni Roho Mtakatifu aliyejitokeza kutia wale watu alama, naye akamwambia Malaika anayeangamiza, “Nenda ukaangamize kila kitu ambacho hakina alama hiyo juu yao.” Na alama ya Mungu ni Roho Mtakatifu; huo ndio muhuri wa Mungu.

⁷⁵ Sasa, wako wapi watu wenye hamu hivyo? Naweza kuwaonyesha ninyi watu ambao huruka juu na chini na kulia na kulia kanisani; naweza kuwaonyesha ninyi watu ambao hupiga shangwe na kukimbia jengoni mwote; naweza kuwaonyesha ninyi watu ambao hutoa unabii, na unatimia: naweza kuwaonyesha wale wanaonena kwa lugha, na—na kukimbia juu na chini majengoni, na kusema mambo ambayo hakika yanafasiriwa na kutimia; lakini yuko wapi yule anayeugua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini? Yuko wapi mtu iliyolemewa? Mngelirekebisha mienendo. Mwaona ninalomaanisha?

⁷⁶ Sasa, nimejaribu kadiri niwezavyo ku—ku—kuwaarifu ninyi watu na kuwaongoza kama baba angewaongoza watoto wake. Ninyi mu watoto wangu; nimewazaa katika Kristo kwa Injili hii ninayohubiri. Ona? Nami—ni—ni—ninawatakeni mkuze watoto waliokomaa vilivyo, au—au watoto. Nami nataka kuwakabidhini Kristo siku hiyo, kama vile Paulo alivyosema, “Bikira safi.” Hakuna kitu katika Neno ila lile moyo wako utaitikia kwa “amina.”

⁷⁷ Dhambi haina... Bila shaka utafanya makosa, lakini wakati yale mengine, jambo la kwanza litakapokuhukumu, “Baba, nisamehe.”

⁷⁸ Nitasema hili. Nilimtaazama mtu fulani dakika chache zilizopita. Yeye alikuwa akiniuliza kuhusu mvulana mzuri hivi majuzi. Tulikuwa tukiwinda kuchakulo. Asubuhi hiyo nilipata watano; niliacha mmoja wao kwa ajili ya jioni hiyo. Unapata tu sita katika jimbo la Kentucky; hicho ndicho kikomo. Kwa hivyo huyu mtu *fulani* alisema, “Nimepata tisa.” Mvulana Mkristo, mtoto mzuri.

Nilimwambia, “Ulikosea. Ulikosea!”

Yeye alisema, “Vema...”

⁷⁹ Nilisema, “Niliwaua watano asubuhi hiyo, nikaacha moja kwa ajili ya jioni hiyo. Na nilipopata kuchakulo huyo mmoja, nilitazama mtini, na kuhesabu watano au sita wameketi papo hapo ambapo ningewatazama, nikaondoka na kuwaacha.” Nilisema, “Nilipitia hapa si muda mrefu uliopita, na kulikuwa na karibu kumi na watano au ishirini wameketi pale. Nilichukua tu kiasi kinachoruhusiwa, nikaondoka, na kuacha wengine wao pale.” Nilisema, “Nikija katika nchi hii, na kuwahubiria ninyi wavulana nanyi watu hapa ukweli, yanipasa kuishi hivyo kama kielelezo.” Ukristo si yale usemayo, ni yale uishiyo, yale utendayo; ni kielelezo. Ninyi ni chumvi ya ulimwengu. Nilisema, “Naam, sheria inasema . . . Yesu alisema, ‘Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari.’ Unapovunja hiyo sheria ya spidi pale, unafanyaje? Unafanya kosa; unatenda dhambi. Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu.”

⁸⁰ Unasema, “Vema, sheria imekosea.” Sijali ni kosa vipi; ni kosa kuvunja amri ya Yesu. Na usipompa Kaisari yaliyo ya Kaisari, basi umefanya kile Yesu hakukwambia ufanye, na umeasi sheria za dhambi. Sivyo?

⁸¹ Sisi sote tuna hatia; tunalifanya. Lakini unapojiona umekosea, koma! Watu wanakutazama; watu hawataenda kanisani, lakini watakusoma wewe, waone unachofanya.

⁸² Kwa hivyo, weka Kristo moyoni mwako; hilo ni kweli . . . Kristo na Roho Mtakatifu ni kitu kile kile. Roho Mtakatifu, *Kristo* maana yake ni “Aliyetiwa Mafuta.” Na Roho Mtakatifu ndiye huko kutiwa Mafuta, na wewe ndiwe uliyetiwa mafuta. Ona? Na ni Kristo ndani yako anayekutia mafuta. Mwafahamu ninalokusudia?

⁸³ Ndipo una kitu halisi. Ndipo Yeye aweza kukutumia wewe kwa cho chote anachotaka kukutumia, kwa sababu wewe uko katika Mwili ule na una haki ya yote ya karama hizo. Lakini ona, kuwa na mojawapo ya karama hizo nje ya Mwili ule, haifaidi kitu. “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za Malaika, na sina upendo, hainifaidi. Nijapokuwa na imani na naweza kufahamu siri zote za Mungu, hainifaidi. Nijapojitoa mwili wangu uteketezwe kama sadaka, nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, nijapokuwa na imani ya kuhamisha milima, mimi si kitu.” Ona? Usitegemee vitu hivyo. Roho Mtakatifu ni Kiumbe; ni Mungu, na Mungu ndani yako, Nafsi ile, Mungu, ambayo inaangaza utu wako wote. Umegeuzwa; wewe u kiumbe kipya. Jambo lo lote ndogo baya, Yeye atakwambia ni kosa, ndipo liache; usilifanye. “Baba, sikukusudia kufanya hivyo (Ona?). Nisamehe.” Ona? Na huyo ni—huyo ni Roho Mtakatifu.

⁸⁴ Sijali ulinena kwa lugha mara ngapi, ulikimbia mara ngapi, uliruka mara ngapi, ulifanya *hivi* mara ngapi, *vile* au *vinginevyo* (Ona?), cho chote ulichotenda, hakingemaanisha kitu kama Roho

Mtakatifu hakuwa ndani mle kukuhukumu kwa vitu vizuri na vibaya.

⁸⁵ Sasa, hiyo ndiyo sababu mtu huyo hapa yuko sawa. Acha Roho Mtakatifu alifanye. Lakini sasa (mwaona?), sasa, nini kinachosababisha hili... Hebu niseme hili kwa upendo, nikilinyunyizia upendo na—na kutiwa mafuta na Neno. Ona? Kama Roho Mtakatifu halisi alikuwa ndani yako, haungeswali hilo. Wewe mwenyewe unalijua, ni jambo la mtu binafsi kati yako na Mungu. Ona? Unajua kuwa kitu fulani kimetendeka. Unajua kuwa mabadiliko, kama kuna lingine—lingine lo lote, wewe mwenyewe, wewe u badiliko. Ona? Wewe ndiwe umebadilika, ndani yako, na unajua unaye. Au ulinena kwa lugha, au uliruka, ulipiga shangwe, au lo lote lile, unajua kuwa Mungu yuaishi ndani yako, ya kwamba hauenendi kwa nia yako, ni nia ya Kristo inayokuongoza wewe pamoja na Neno, vivyo hivyo tu jinsi aendavyo.

⁸⁶ Sasa! Lakini mimi... Kama watu wakisema, “Vema basi, Ndugu Branham, hauamini yatupasa kunena kwa lugha?” Ona? Basi umepata kinyume cha yale ambayo nimekwisha sema. Hakika, naamini yawapasa mnene kwa lugha. Na baadhi yenu watu... Ona? Lakini unapata haya, nami napata haya, kama nyuma hapa hizi maili elfu moja na mia tano (mwaona?), kuwa hapa maskani. Kama hamyafahamu, basi niulizeni. Ona? Niandikieni kama hamfahamu. Semeni tu yale nisemayo hapa. Ona? Nami... Nanyi... Kama Paulo alivyosema, “Nifuateni mimi kama ninavyomfuata Kristo.” Mwaona? Ndipo mkiona nimekosea, basi msinikaribie (Ona? Hivyo tu), kwa sababu ninge—ningekuwa mtu mbaya. Ona?

329. Tafadhali eleza. Watu wanasema Ndugu Branham ni zaidi ya mwanadamu, yeye aweza kuumba, na Yesu aweza kufanana kabisa na Ndugu Branham.

⁸⁷ Sasa, hebu ni... Mtu huyu alisema hili. Ye yote yule, simjui. Lakini mimi ni ndugu yenu. Ona? Yesu ndiye Mwokozi wenu. Siwezi kuwa Mwokozi wenu, kwa kuwa Yeye amekwisha waokoa ninyi. Sasa, uko karibu sana na Kweli pale, na hata hivyo uko mbali sana na Kweli, mtu aliyemwambia mtu huyu hivi. Sasa, i—inaonekana kwangu kama mwandiko wa mwanamke, mwandiko mzuri mno. Nami ningesema huo ni mwandiko wa mwanamke, sivyo? Ndugu Capps, si ungedhani huo ni mwandiko wa mwanamke? Mwandiko mzuri. Nami sijui ni nani. Ona?

⁸⁸ Basi “Ndugu Branham, je, unafanana na Yesu, ama wewe ni Yesu, au kitu kama hicho?” Kwa upande mmoja, hiyo ni Kweli hasa; kwa upande mwingine huo ni upinga Kristo. Hiyo ndiyo tofauti baina ya kweli na uongo. Kunifanya Utu wa Yesu Kristo ni upinga Kristo (mwaona?), kwa sababu ule Utu wa Bwana Yesu umeketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu, na utarudi tena kwa nguvu nyingi na utukufu. Lakini kuhusu ule Uhai Wake

uliokuwa ndani Yake kuwa juu yangu, na juu yenu mliye Naye, hiyo ni Kweli hasa; nanyi mnakuwa Kristo.

⁸⁹ Mnakumbuka ujumbe wangu kwa Mamasihi? Ona? Ninyi ni... Neno *Masihi* maana yake ni—"mtiwa mafuta." Sasa, uko hivyo, kama una Roho Mtakatifu, unakuwa mtiwa mafuta. Ona? Ndipo kuna kila namna ya watiwa mafuta.

⁹⁰ Sasa tazama, kama ni mtiwa mafuta wa Biblia. Wengi wao wametiwa mafuta... Ona? Jambo lote ni kusanyiko kuu la... kila namna ya mvurugo; na—na ya—Shetani kwa hila zake zote aliingia kuiga hilo kikamilifu kabisa, karibu kabisa. Kuna njia moja pekee unayoweza kuwa na hakika kabisa; chunguza neno kwa neno, neno kwa neno! Hivyo tu ndivyo uwezavyo.

⁹¹ Lakini kwangu kama m—mtu binafsi, William Branham, au—au mwanamume mwingine au mwanamke kuwa Bwana Yesu Kristo, Mwokozi wetu, hilo ni kosa. Lakini kutiwa mafuta na Roho Wake, ambaye huleta Utu Wake binafsi wa Uhai Wake ndani yako...

⁹² Ilionyeshwa katika mfano mzuri mno katika Eliya na. Elisha, aliponyakuliwa, yule Eliya, yule nabii mzee, akienda nyumbani. Naye alikuwa amechoka na kuishiwa nguvu; na kulikuwa na gari lililofungwa ng'ambo ya mto pale, naye—kumpeleka yeye nyumbani kwa farsi wa moto. Na ulitambua wakati huo, Eliya na Elisha walipovuka mto ule (kundi la manabii lilikuwa pale likiwatazama) kisha Eliya akachukua joho lake na au—akapiga mto ule, na alipoupiga, ukagawanyika, naye akavuka. Naye akamwambia yule nabii kijana, "Una—unanifuata kwa sababu gani? Una—una—unataka nini?"

⁹³ Yeye alisema, "Ya kwamba sehemu maradufu ya roho wako injie." Sehemu maradufu ya huyo nabii mkuu injie mimi?

Yeye alisema, "Umeuliza jambo gumu; lakini kama utaniona nikienda, basi itakujia." Kwa hivyo unaweza kuwazia jinsi yeye alivyomkazia macho nabii yule.

⁹⁴ Sasa, katika siku hiyo, nabii yule alikuwa Neno, kwa maana yeye alikuwa dhihirisho la Neno kwa ulimwengu. Ona? Naye alijua hapana budi huduma kuu itakuja, kwa sababu kitu kikuu zaidi kilihitijika. Na Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa yule Eliya. "Kazi nizifanyazo mimi, ninyi nanyi mtazifanya pia; naam, na kubwa kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba." Sasa, mtazifanyaje? Mtazame! Yeye yu Nani? Neno! Ona? Mtazame!

⁹⁵ Sasa, inapofikia kuumba vitu, ni kweli. Yesu hakuwahi kamwe kuumba cho chote moja kwa moja na kukifanya kiwepo. Yeye alichukua kitu kwanza. Yeye alichukua maji, akafanya divai. Yeye alichukua mkate na kuumba mikate mingine. Yeye alichukua samaki na kuumba samaki wengine. Lakini Yeye aliahidi kuwa kazi kubwa kuliko hizi zingefanywa. Ona? Mwaona? Sasa, kwa nini? Ni katika siku mbovu mno kuliko

wakati Yeye alipokuwa hapa. Ona? Ingali ni Yeye, lakini akitumia maskani yako. Ona?

⁹⁶ Na mtu huyu aliye ndani yako, ambaye ni kuzaliwa kwako. . . Wewe u John Doe; ulizaliwa mwezi *fulani*, na ulizaliwa chini ya nyota *fulani*; ulizaliwa chini ya kitu *fulani*, na hilo lina uhusiano *fulani* nawe. Bila shaka!

⁹⁷ Najua nilizoea ku- . . . Baba yangu alizoea kusema, “Siwezi kupanda viazi wakati huu, kwa maana mwezi hauko sahihi. Huwezi kupanda viazi hivyo, Billy.”

⁹⁸ Nami nilisema, “Sivipandi kule mwezini, ninavipanda humu ardhini!”

Kasema, “Vema, kimbelembele, endelea! Utapigwa kichwani mara kadhaa kwa mawe kisha utajifunze jambo *fulani*.” Ikawa hivyo. Ikawa hivyo.

⁹⁹ Nawaambieni: chukua ubao na uweke chini kule nyasi mwezi ukiwa giza na tazama kipi kitendekacho. Nyasi hiyo itakufa wakati uu huu. Iweke kwenye mbalamwezi; unaweza kuuacha ukae pale juma moja; hautadhuru hata kidogo.

¹⁰⁰ Tazama bahari hiyo mwezi huo ugeukapo kule juu. Maji yajaapo na kupwa—mwezi upoteapo, maji kujaa na kupwa huufuata, na uko mamilioni ya maili toka duniani. Isitoshe, nenda chini kule katika jimbo la Kentucky ukasindilie ufito ardhini hadi ufikie maji ya chumvi; na tazama bomba hiyo, iko umbali gani mwezi unapo—wakati wa kupwa na kujaa kwa maji na tazama jinsi unatoka, chini kabisa ya ardhi. Hakika!

¹⁰¹ Panda kitu *fulani* ambacho hutandaa juu ya ardhi. Katika giza la mwezi kinaingia chini moja kwa moja na kufanya kama figili au muhogo ufanyavyo. Kipande vinginevyo na kitazame kikitandaa juu ya nchi. Hakika, kina kazi.

¹⁰² Sababu gani Haruni alikuwa na yale mawe ya kuzaliwa kwa kila mmoja wa hawa wazee katika kile kifuko chake cha kifuni? Tazama wale mama walipotoa yale matamshi. Wakati hao mama na wale wanawake Waebrania katika utungu wa kuzaa walitoa matamshi kwa watoto waliokuwa wakizaliwa, iliweka majina yao mahali panapofaa; ilieleza kuzaliwa kwao; iliwaweka katika nchi ya uenyeji wao; iliwaweka utukufuni.

¹⁰³ Hivi karibuni nitakapoingia na kukaa kwa wakati mdogo, nataka kuchukua somo hili. Hakika! Ndipo mtazame Yakobo, alipokuwa akifa pale, yeye aliweka mikono yake juu ya hao wazee wetu na kuwabariki, yeye angewaambia hasa mahali wangukuwa. Na hiyo inalingana hasa na majina yao, na kulingana kabisa na kuzaliwa kwao. Na bila shaka, lina uhusiano *fulani* nawe.

¹⁰⁴ Sasa, hiyo ndiyo njia ya kuzaliwa kwako; hivyo ndivyo ulivyo, mwanamume wa kawaida au mwanamke wa kawaida. Lakini unapozaliwa mara ya pili, hiyo si dhamiri ya nje. Ya nje

ni kile uonacho, unachoonja, unachogusa, unachosikia, lakini ndani ya hiyo ni jinsi wewe ulivyo hasa. Sasa, hii nje hapa, Shetani hukujaribu na kukugongesha hapa na pale kwa kila njia hapa; lakini chini hapa yeye hawezi kulifanya isipokuwa unamruhusu afanye. Maana ndani humu una imani, na imani haitokani na dhamiri ya nje, hiyo inatoa hoja. Lakini katika imani hakuna kuhoji. Unaipata toka kwa Mungu, na unajua iko humo. Sijali inaonekana kosa vipi, wewe bado unajua ni sahihi; ni BWANA ASEMA HIVI. Ona? Na hakuna lo lote litakalosumbua hiyo. Hakuna lo lote liwezalo kuitatiza; inaendelea moja kwa moja. Ugumu haumaanishi lo lote kwake; inayumbayumba ikaupita, maana ni Neno. Na Neno ni Upanga, na Neno hukata. Upanga hukikatilia mbali na kitu cho chote. Mwaona? Inachukua mkono wa imani kushikilia Neno hilo. Imani hiyo yapaswa . . .

¹⁰⁵ Sasa ona, wakati hiyo dhamiri ya ndani . . . Hapa kuna ya ndani, hapa kuna ya nje. Inafunuliwa ndani humu, ile Kweli; nje hapa, ni hoja. Sasa, si laonekana la busara kama tungalisema tu, “Tuendeni sote tukajiunge na Assemblies?” Sasa, napenda Assemblies of God, napenda Oneness, nayapenda makanisa hayo yote. “Mbona sote tusiende na kujiunga nayo, huenda yakatufaidi.” Hiyo ni hoja, ya nje. Lakini kule chini upande wa ndani, tazama. Ukiangalia nje hapa, hii ita—hii haitakubali, ndipo tazama Assemblies. Mambo mengi wanayofanya ambayo siaamini ni—ni ya Kimaandiko, na naweza kuwathibitishia wao si ya Kimaandiko. Lakini nia nyingi mno zimejazwa mle. Kuna maelfu ya hao ndugu na dada wa Assembly wanaoamini hili, Neno, na hawaamini yale Assemblies inafundisha kuwa sahihi. Lakini wako katika utando ule.

¹⁰⁶ Wabaptisti, Presbiteria, Oneness, na wengine wote, wako ndani ya utando huo pale ambapo kundi la watu hukusanyika pamoja na kuhojiana. Wanadamu wana kiburi sana. Hapa kuna askofu fulani anayeketi hapa, msimamizi mkuu; yeye husema lo lote, maskini yule mtu mdogo atasemaje? Yeye anaogopa kusema lo lote. “Nakubaliana nawe. Naam, ndivyo! Enhee! Naam, Askofu, au—au Mzee wa kanisa, wewe u—ndivyo hasa.” Yeye anakubaliana naye.

¹⁰⁷ Hapa, hebu na tuchukue mlevi nje hapa barabarani, ambaye—raia wa kawaida anapita barabarani na kusema, “Maskini mvivu, yeye si kitu.” Mpeleke chini hapa, mweke kwenye jeshi la polisi, na mvike nishani, na kumpa bunduki. “Habari za asubuhi, Yohana, nafurahi kukuona tena!” Ona? Kuheshimiana.

¹⁰⁸ Yesu alisema, “Unawezaje kuwa na imani unapokuwa na kuheshimiana kwa namna hiyo,” mwajua, tusihi, kuheshimiana (sikumbuki neno linavyosema pale)—lakini unapotamani—kuheshimiana. Ona? Huwezi kufanya hivyo.

109 Basi watu wale wanapokusanyika katika dhehebu, wanaketi chini; na maskini mtu mdogo anaogopa kusema lo lote, kwa sababu askofu alisema hivyo, mzee wa kanisa alisema hivyo. Lakini usimdharau mtu yule, naamini yeye ni mtu mzuri; lakini kila mara kumbuka, Neno la Mungu li sahihi na mengine yanayolipinga ni uongo. “Na Neno Langu liwe kweli, na neno la kila mtu liwe uongo.” Mwaliona? Hilo ndilo tunalotaka kufanya, ni kuamini hilo.

110 Sasa kumbuka, sisi si Neno, lakini sisi tu Neno. Enhee! Sasa mnalifahamu? Yesu hakuwa Mungu, lakini Yeye alikuwa Mungu. Yeye alikuwa mwanadamu, hata hivyo Yeye alikuwa Mungu. Yeye angelia, walakini angefufua wafu. Yeye angemlilia mtu aliyekufa kisha amfufue tena. Yeye alikuwa Yehova-yire, Yehova-rafa, Yehova Manase; Yeye alikuwa Yehova, wote kabisa. Yeye alikuwa Yehova, walakini alikuwa Mwanadamu. Yeye alimiliki nchi, na akaumba nchi, na hakuwa na mahali pa kuweka kichwa Chake. Yeye alisema, “Ndege wa angani wana viota vyao, nami sina mahali pakuweka kichwa Changu. Mbweha, niliowaumba, wana matundu ardhini nami sina mahali hata pamoja, hata pa kuzikiwa.” Hiyo ni kweli. Iлимпasa Yeye kuomba kaburi la mtu fulani azikiwe mle.

111 Yeye aliumba tumbo la uzazi lililokuwa ndani ya mwanamke. Yeye hakuwa na tumbo la uzazi la kuzaliwa, ilimlazimu kuazima tumbo la uzazi. Yeye aliumba dunia na hakuwa na mahali pa kuzikiwa; ilimlazimu kuomba shi—shimo katika ardhi ili azikwe mle, Yusufu wa Arimathea. Ona? Wao walikuwa—iliwalazimu—alilazimika kuomba mahali, hali Yeye alikuwa Mungu, alithibitisha ya kuwa Yeye alikuwa Mungu.

112 Sasa, mwafahamu? Sisi hatu. . . Sisi ni Mamasihi wadogo bali si yule Yesu. Yeye ni Baba yetu; sisi tumetiwa mafuta tu kwa Roho Wake, na hiyo ndiyo sababu Uhai Wake. . . Na hilo huwapata watu. Ona, usipoketi na kuliwazia lote, lafanya watu kuamini, “Vema, mtu huyu ndiye Masihi.” Hakika ndivyo alivyo.

“Huyu hapa angekuwa hivyo.” Wote wawili wako hivyo. Ona? “Vema, waweza je kuwa wawili?” Ona? Kuna maelfu yao. Ona?

113 Lakini mwoana, Uhai Wake uligawanywa katika siku ya Pentekoste. Wakati hiyo Nguzo ya Moto iliposhuka, ilijigawanya kama ndimi na kukaa juu ya kila mmoja wao. Mungu akijigawanya Mwenyewe kati ya watu Wake, kwa sababu Kanisa na Kristo ni Mmoja, kama tu vile mume na mke ni mmoja.

330. Ndugu Branham, ninapaswaje kumwonyesha mke wangu kuwa hakika namjali na hata hivyo nidumishe—kukaa na Neno (Hilo ni)—kukaa—kukaa na Neno, lakini bado ningali na swali kama hili lisemalo: “Mbona hutendi yale unayohubiri au kuamini?”

114 Vema basi, kama mkeo, kama mkeo anakwambia wewe hayo wakati yeye ana—ana haki kuyasema, yakupasa uwe sawa.

Ona, ona? Bali kama yeye, na kama yeye anasema hayo kwa chuki, kumbuka, Biblia ilisema, “Yakufaa ufungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoshwa katika kilindi cha bahari kuliko kumkosesha mmojawapo wa wadogo Wangu hawa.” Sasa, hilo ni swali lako.

¹¹⁵ Na labda mke huyu si mtu wa namna hiyo. Labda yeye yu tofauti—labda yeye ni mtu mzuri. Labda anakujaribu tu kuona utafanyaje.

¹¹⁶ Sasa, endelea kumpenda na acha yeye amwone Yesu ndani yako. Fanya hivyo. Ona? Endelea tu. Wengine... Nilitoa mfano mdogo asubuhi hii kuhusu mtu ambaye... Wakati mmoja maskini mwanamke huyu alikuwa—alikuwa amempokea Roho Mtakatifu. Yeye alikuwa mtu mpendwa sana. Wao... Yeye alisema... Vema, yeye alikuwa na maisha magumu, na mumewe alikuwa mlevi kupindukia. Na kwa hivyo, yeye aliendelea tu; yeye alimvumilia. Mumewe kamwuliza, “Unataka kwenda kanisani, Mpenzi, nenda! Lakini nitaenda tu pale kwenye kilabu cha pombe, chini kule kwa Brown Derby ya kale, chini kule. Enda na—endelea.” Kwa hivyo wao walikaa kule wakati wote, kilikuwa kikiitwa Bonifers. Wengi wenu watu wa kale hapa mwakumbuka wakati Bonifers ilikuwa pale pembeni na... Inaitwa Brown Derby sasa, naamini.

¹¹⁷ Kwa hivyo, akizunguka pale, na muda si muda, usiku mmoja kukazuka swali kuhusu kanisa na kuhusu Wakristo. Mmoja wa walevi wa kale akiketi pale kasema, “Hakuna tena kitu kama Wakristo.” Kasema, “Hakuna kitu kama hicho. Kundi hili lote ni la manafiki,” kasema, “unawaona nje hapa wakivuta sigara, wakinywa pombe, wakitenda mambo yale yale tunayofanya, na,” akasema, “wanajiita Wakristo. Hakuna kitu kama hicho.”

¹¹⁸ Huyu mlevi mmoja akasimama na kusema, “Hebu kidogo! Kuna mmoja ninayemjua.”

Kasema, “Ni nani huyo?”

Kasema, “Ni mke wangu.” Ona? Yeye alikuwa amekolea. Yeye alikuwa akilishika wakati wote.

Yeye kasema, “Nawahakikishia kama yeye akifinywa...”

Yeye alisema, “La, yeye yungali Mkristo; nitawathibitishia.” Kasema, “Nitawaambia tutakachofanya; hebu tuende nyumbani, nami nitawaonyesha kama yeye ni Mkristo au la.” Kasema, “Hebu twende nyumbani, na sasa, hebu tujifanye walevi sana. Tutajifanya kama tulio walevi sana.” Wakabisha mlango, wakaingia wakiweweseka juu ya kila kitu na—na... “Mbona msiketi hivi,” na kila kitu. Na mke yule akampa kila mmoja wao kiti na (wageni wake, mwajua)—na akajaribu kuwakaribisha jinsi alivyoweza. Kasema, “Nataka utupikie chakula cha jioni.” Na kwa hivyo hao—yule mama akaenda akawapikia. Kasema, “Tunataka mvungu wa paja na mayai.” Yeye alijua walikuwa nayo, kwa hivyo ukapikwa mvungu wa

paja na mayai. Alipofika pale kwa mezani, akakitazama hivyo, akachukua sahani yake, na kutupa chakula kile sakafuni, kasema, “Wajua, sipendi mayai yangu yapikwe hivyo. Njoooni vijana tuondoke mahali hapa haidhuru,” hivyo—hivyo.

¹¹⁹ Waliondoka nje na kuketi chini hivyo, mwajua. Naye akaja; akasema, “Mpenzi, nina—ninasikitika sikuyapika vizuri, nitawapikia ninyi mengine.”

¹²⁰ “Ee, upuzi, kwanza ulijua sikuvitaka hivyo,” wakiendelea tu kufanya yasiyofaa hivyo. Wakaondoka nje pale, wakaketi chini, na kutenda kama walevi. Walimsikia ndani mle kama anayejidharau, akiimba kwa sauti ya chini sana:

Je, yambidi Yesu auchukue msalaba pekee

Yake,

Na ulimwengu wote uwe huru?

Kila mtu ana msalaba,

Nami nina msalaba.

Huu msalaba uliotiwa wakfu nitaubeba,

Hadi kifo kitakachoniweka huru.

Mlevi mmoja alimtazama mwingine, kasema, “Yeye ni Mkristo; yeye amelishika.” Na maskini mwanamke huyo alimleta mumewe, pamoja na hao wengine kwa Kristo usiku huo. Ona? Kwa nini? Ona? Kuwa mzuri kabisa. Kumbuka tu, Yeye anajua hayo yote.

¹²¹ Kwa hivyo, Dada, au Ndugu, ye yote yule au Ndugu, iko hapa, kwa sababu yeye aliuliza kuhusu mkewe, basi kolea tu; yeye atashikwa na kiu kama kuna cho chote ndani yake cha kusikilia kiu. Kama hamna, kumbuka, kama ulimpata asiye faa, utapata anayefaa katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Zidi kuendelea tu; mabaya yote yatarekebishwa kule.

331. Ndugu Branham, je unafundisha ya kwamba Bibi-arusi hapaswi kuhudhuria kanisa lo lote isipokuwa wewe uko pale ukihubiri, la sivyo, humu maskanini—kwa maneno mengine, humu maskanini? (lina “la sivyo,” maana yake “kwa maneno mengine”)

332. Pia, unafundisha kuwa hatupaswi kuadhimisha Ju—Jumapili au sikukuu, kama kufanya kazi, kuvua samaki, na kadhalika? Au... (Ningesema hiyo ilikuwa Jumapili. Ilionekana kama Jumapili kwangu, Au pale chini ilionekana kama—au Jumapili, nadhani ndivyo ilivyo, sikukuu au Jumapili. Naam, Jumapili, hivyo ndivyo lilivyo? [Ndugu Branham aongea na mtu fulani—Mh.] Siku takatifu—siku takatifu, Jumapili na siku takatifu.)

¹²² La! Umekosea. Ona? Hebu nilisoma kwa utaratibu na kulijibu nitakapolifikia.

“Je, unafundisha kuwa Bibi-arusi hapaswi kuhudhuria kanisa lingine lo lote isipokuwa wewe unahubiri—unahubiri la

sivyo, ama, maskini haya?” La! Sifundishi hayo. Siamini hivyo; siamini. Tuna wahudumu wanaoketi hapa waliotawanyika kote nchini, nami naamini wao ni sehemu ya yule Bibi-arusi. Naamini kuwa mwanamume au mwanamke aweza kwenda kanisani po pote wanakotaka kwenda ambapo hufundishwa Neno. Nami naamini, kama hawafundishi Neno lote, na huwezi kwenda mahali pengine po pote ambapo wanafundisha Neno lote, nenda ambapo wanafundisha Neno nusu hadi utakapopata ambapo wao wanafundisha Neno lote. Nenda kanisani kwa vyo vyote vile. Fanya hivyo.

123 “Pia unafundisha kuwa yatupasa—yatupasa—kuadhimisha Jumapili, au siku takatifu yo yote, au—au kufanya kazi—au—kama kufanya kazi, au kuvua samaki siku ya Jumapili?”

124 Naamini ni dhambi kuvua samaki, na kuwinda, na kufanya kazi Jumapili wakati unapoweza kwenda kanisani. Sasa, naamini unavunja sheria za Mungu. “Je, kunayo sheria kwa hilo?” Naam, bwana! Sasa, katika Agano la Kale tulikuwa na mfano wa siku ya Sabato. Yote ilikuwa... Na Yesu hakuja kwenu kuadhimisha siku ya Sabato. Ile siku ya kale ya Sabato ilikuwa Jumamosi, ambayo ilikuwa mwisho wa juma. Jumapili ni siku ya nane, au siku ya kwanza ya juma, ambapo Yesu alifufuka,

125 Siamini ni haki ku... Sasa, kama uko mbali sana nyikani mahali fulani, na uko kule nje kwa safari ya kuwinda, hakuna kanisa karibu, kitu kama hicho, hakuna lo lote uwezalo kufanya; na kama ulikuwa ukivua samaki, naamini hilo lingekuwa sawa. Lakini kama uko karibu na mji, au karibu na mahali kanisa linaendelea, yakupasa uhudhurie kanisa kwa vyo vyote vile, mahali fulani.

126 Nami naamini, kwa habari ya kufanya kazi, naamini kama ng’ombe yumo shimoni, au jambo fulani linapaswa kutendwa Jumapili, endelea ukalifanye, kama ni jambo fulani huwezi kujizuia, ilipasa lifanyike hivyo. Lakini kama unalifanya tu, na kungoja hadi Jumapili ifike ndipo ulifanye, au ulifanye tu hivyo, umekosea. Ona? Yatupasa tusifanye hivyo, yatupasa tuheshimu hiyo siku takatifu.

127 Na sasa, kumbuka, enda kanisani mahali fulani, mahali po pote. Kama... Ni—ningetaja kanisa fulani la kidhehebu, lakini singefanya hivyo, kwa sababu kanisa hili, jambo pekee nijualo wanalofundisha ambalo naamini ni, wao husema wanaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Vema, naamini hilo. Mafundisho yao mengine yote ni... Wanaamini... na ondoleo la dhambi ni kwa maji. Sasa, si wa umoja; wao hufanya vivyo hivyo, lakini siongei habari zao. Wanaamini kuwa—kuwa kuzaliwa mara ya pili ni kwa maji, na kadhalika. Nami siamini hilo. Nao, ee, wanaamini kama cho chote kilicho na uponyaji wa Kiungu ni cha ibilisi. Nao wanaamini katika yote... Wao ndio pekee—

ndio kitu pekee kilicho, na kitu pekee kikupasacho kufanya ni kuandika tu jina lako katika kitabu. Na kama halimo humo, umepotea. Sasa, siamini hilo. Lakini kama kulikuwa hakuna kanisa lingine lo lote kuhudhuria (singeenda mle kulaumu), ningeenda mle kwa nia ya kuhudhuria, na kuketi karibu na mtu fulani, kusudi Kristo aliyekuwa moyoni mwangu apate kumshawishi mtu fulani mle. Enda kati yao, lakini usiwe mshiriki wa kutokuamini kwao.

333. Ndugu Branham, nataka kumpokea Roho Mtakatifu. Nataka nijue la kufanya. Ninalemewa kwa ajili ya jamaa yangu ipate kuokoka. Na dada yule aliandika jina lake.

¹²⁸ Kama unataka kumpokea Roho Mtakatifu, hebu nikwambie jambo fulani, Dada yangu mpendwa, kama uko hapa. Na—na—mimi. . . Ndugu Neville, je, huyo ni mshiriki wa kanisa hapa? [Ndugu Branham aongea na Ndugu Neville—Mh.] Nami pia si—siwakumbuki, lakini kama—kama uko hapa, Dada B—o—u—g—h, kama uko hapa, hebu nikwambie, Biblia ilisema, “Heri walio na njaa na kiu ya haki. . .” Umebarikiwa sana kwa kumtaka. Ona? Sasa, kumbuka, si kwamba una—una—umempokea, lakini heri wale walio na njaa na kiu Yake, “kwa maana watashibishwa.” Kaa tu moja kwa moja nacho.

¹²⁹ “Yanipasa nifanyeje kwa ajili ya jamaa yangu?” Tumia imani ile ile unayotumia kwako mwenyewe, kwa ajili ya jamaa yako. Wakabidhi kwa Bwana na uamini kwa moyo wako wote ya kuwa utaokolewa. Hebu. . . Usiache tu lije kwa mawazo yako ya kawaida hapa, acha limiminike mle ndani, hiyo dhamiri ya ndani, ndipo ni wako. Mungu atakupa hayo ukiwa naye mle ndani.

¹³⁰ Lo lote ulilo nalo moyoni mwako humu na unaliombea, unapoomba, amini kuwa unapokea kile unachoomba. Sasa, huwezi kukitilia shaka. Huwezi kuamini na kutilia shaka wakati uo huo. Wangapi wajua hilo? Huwezi kuamini na kutilia shaka wakati uo huo. Sharti uamini ya kwamba unachoomba, unakipokea, ndipo Yeye alisema ungepewa. Kwa hivyo amini tu kwa ajili ya jamaa yako, nao watalipata.

334. Ndugu Branham, vipi kuhusu mtoto wetu wa kiume kwa kuwa—kwa kuwa—hauhubiri zile Parapanda? Unakumbuka ile ahadi uliyonipa kwa simu kumhusu yeye na zile Parapanda Saba?

¹³¹ Siikumbuki. Sikumbuki ilikuwa nini. Lakini hata iwe nini, umjulishe Billy Paul ni nini cho chote nilichoahidi nitatekeleza. Siikumbuki. Mwanjua mimi—wakati napata—labda wakati wa usiku mimi hujibu simu thelathini, arobaini katika wakati mmoja (mwaona?), kwa hivyo sikumbuki usiku baada ya usiku—wakati mwingine ninapokuwa humu—kwa hivyo sielewi ni nini.

Itakuwaje kwa dada na ndugu yangu Mkatoliki? Asante.

¹³² Ee, mtu huyu anatoka mbali sana nje ya mji, kule Texas. Nina... Vema, Dada, kama u—kama unatoka Texas na utapata ukanda huu, au kama kuna ukanda (nadhani hakutakuwa na ukanda wa huu), lakini kama kuna... [Ndugu Branham auliza kuhusu kunasa ibada hii—Mh.] Je, wanafanya kanda? Je, mnainasa? vema, kama wananasa... Kanda ile... Basi hebu niwaambieni. Kama mna... Kwenye kanda hii, unapopata hili, kumbuka, “Itakuwaje kwa mtoto wetu wa kiume wakati—kuhusu zile Baragumu Saba?” Sikumbuki kuhusu hilo, isipokuwa kama niliahidi kumwona yeye wakati zile Parapanda Saba. Kama nilifanya hivyo, nitamwona; kwa sababu sikuhubiri zile Parapanda Saba, nilihubiri ile *Sikukuu ya Parapanda*. Mwafahamu hilo?

¹³³ “Na itakuwaje kwa dada na ndugu yangu Mkatoliki? Asante!” Nakwambia, Bi. C-o-r-n-i-l-s-e-n... Kama mwanamke yule ako hapa, mwone Billy Paul asubuhi hii. Na—na kama sivyo, vema, nita—nita—si—sifahamu hili ni nini (mwaona?); ni swali tu. Si sifahamu (ona?), ni nini, kwa sababu niliahidi kitu fulani kuhusu mfulana wake na zile Parapanda na kuhusu dada fulani Mkatoliki; nami si—sifahamu—haliko mawazoni mwangu kulikumbuka. Mwone tu Billy.

Hili lazima... Hilo ni kuomba maombi. Limeandikwa jina la mtu yule na kusema, “kichwa na homa ya mapindi.” Kwa hivyo ilikuwa tu... kuwaombea tu, nadhani. Vema.

335. Tafadhali fafania ndoa na talaka. (Nimekwisha pata hilo. Haya ni maswali saba—maswali manane kwenye karatasi moja.) **Tafadhali fafania ndoa na talaka.**

Nilifanya hivyo.

336. Musa na—na Eliya wako duniani sasa? Je, Musa na Eliya wako duniani sasa? Je, wako Amerika?

¹³⁴ La! Ona? La, hawako hapa; hawatakuwako hadi Kanisa litakaponyakuliwa, ndipo Musa na Eliya... Wangapi wanaelewa hilo? Vema. Hebu tuone. Hamna jina lo lote lililoandikwa kwa hili, kwa hivyo... Vema. Kama ye yote aliyeuliza maswali haya... naamini ni saba; nimeweka—nimetia alama saba. Vema!

337. Eleza tofauti kati ya lile “Jina la Yesu,” na “Jina Lake Yesu.” (Ngoja kidogo.) **Eleza tofauti kati ya Jina “Yesu” na “Jina Lake Yesu.”**

¹³⁵ Vema, yote yatakuwa sawa yakitumiwa sawa (ona?), yakitumika kwa Mtu yule yule, jina *Yesu*, na *Jina Lake Yesu*. *Jina Lake Yesu*, na *jina—jina Yesu* linaonyesha Yeye ni nani. *Jina Lake Yesu* linanena juu ya Mtu huyo, kwa hivyo ingekuwa ni kama... Nadhani hilo lingekuwa... Je, si hilo laonekana lenye busara? Jina *Yesu* ni Mtu Binafsi, na *Jina la Yesu* ni wewe ukimtaja Mtu huyo. Ona?

¹³⁶ Tuseme, jina langu ni *William*. Huyu ni mimi. Vema. Sasa, tuseme . . . ninanena . . . *Jina lake William*, ndipo unanitaja mimi. Hilo ni jina langu. Ona? Sasa.

338. Je, Jina la Bwana, limebadilika katika nyakati mbalimbali?

¹³⁷ Naam, ndivyo! Wakati mmoja aliitwa—Yeye aliitwa MIMI NIKO. Yeye aliitwa Yehova, na Yeye ameligeuza mara nyingi. Wakati wa mwisho lilipogeuzwa ilikuwa Mungu alipofanyika mwili na kuchukua jina la kibinadamu.

¹³⁸ Yehova, MIMI NIKO, na hayo yote, ni vyeo vya Jina fulani. Ona? Mlibatizwa kwa jina la Yehova, halina budi kuwa lile Jina la Yesu Kristo. Ulibatizwa kwa jina la Yehova-rafa, Yehova Manase, na Yehova Yire, na hayo yote, itapasa kuwa Yesu Kristo. Yule MIMI NIKO ni Yesu Kristo.

¹³⁹ Kumbuka, akisimama pale siku hiyo, Yeye alisema, “Mnasema mlikula mana jangwani . . .”

“Baba zetu walikula mana.”

“Nao wamekufa!” Yeye aliwaambia.

¹⁴⁰ Wao walisema, “Vema, sasa tumeng’amua ya kwamba una wazimu, kwa sababu wewe u mwanadamu tu na hupati miaka hamsini na unasema umemwona Ibrahimu.”

Yeye alisema, “Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Ona? Yeye alikuwa MIMI NIKO. Na vyeo vyote na majina yaliyowahi kuwa ya Mungu yalifanywa jina moja la kibinadamu, Bwana Yesu Kristo. Vema.

339. Sasa, kama wakati unakwisha zile Muhuri zilipofunguliwa, basi—ni . . . Kama wakati ulikwisha (samahani) zile Muhuri zilipofunguliwa, basi ule Utawala wa Miaka Elfu pia una—ndipo ule Utawala wa Miaka Elfu umekwisha, sivyo?

¹⁴¹ La, la! Wakati haukwisha Muhuri ilipofunguliwa. Ulikosa kufahamu. Kile kilichotendeka, siri zile zilifunuliwa, wakati haukwisha. Ona? Tazama tu. Chunguza kwa makini sasa, na uta—cheza kanda yako kama ulisikia hayo kwa ukanda fulani. Ona?

¹⁴² Wakati haukwisha hadi . . . Huyu hapana shaka ni mtu anayeamini ya kwamba ule Utawala wa Miaka Elfu utafuata kule Kunyakuliwa au kitu kama hicho aliyeuliza swali hili. Kwa sababu ona? Tuna miaka elfu baada ya Kanisa kwenda nyumbani na kurudi juu ya nchi. Ndipo wakati utakoma katika Mbingu Mpya na Nchi Mpya.

¹⁴³ Sasa, ule Utawala wa Miaka Elfu si Mbingu Mpya na Nchi Mpya. Bado kutakuwa na dhambi baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Ule Utawala wa Miaka Elfu ni mfano wa Nuhu alipoingia safinani, na kuelea juu, na kuwaleta Hamu

na wengineo upande wa pili. Na dhambi hata zilitoka kwenye safina. Ona?

144 Lakini Henoko, mtu aliyegeuzwa, alikuwa mfano wa Bibi-arusi aliyepaa juu, si yule aliyeelea juu. Kwa hivyo dhambi bado itakuwako ng'ambo ya pili ya ule Utawala wa Miaka Elfu lakini si katika siku za ule Utawala wa Miaka Elfu. Ona? Katika ule Utawala wa Miaka Elfu kuna amani. Ona? Lakini dhambi itahukumwa ng'ambo ya pili ya ule Utawala wa Miaka Elfu, na ndipo wakati utakapotoweka.

145 Na sasa, kule kufunguliwa kwa zile Muhuri Saba zilizotolewa na Roho Mtakatifu, zile Muhuri Saba zilikuwa tu zijulishe yale yaliyokuwa yameachwa katika zile nyakati zilizokuwako nyuma yetu.

146 Sasa, kama mwanatheologia mashuhuri alivyojaribu kuninasia hilo, yeye alisema, "Ndugu Branham, wewe—Mungu siku moja atakupea wewe siri za hizo Muhuri Saba. Hizo Muhuri Saba zitakuwa kitu fulani ambacho hatujawahi kamwe kujua, hizo zitakuwa kitu fulani ambacho hata hakiko katika Biblia." La, la! hazitakuwa hivyo, kwa sababu ukifanya hivyo, hilo lingefanya... Kama ningaliwaambia hayo, ningekuwa nabii wa uongo, kwa sababu (mwaona?) Neno hili... Pale... Kila kitu ambacho—ambacho... Ufunuo wote wa Yesu Kristo wote umekamilishwa katika Neno hili. Ona? Na kama zile Muhuri Saba zinahusu yale makanisa saba, ilipasa iwe imekwisha pita, kwa sababu sisi tuko katika wakati wa kanisa la Laodikia... Na zile Muhuri Saba zilikuwa tu zikifunua yale wao walikuwa wameyaacha nyuma kule, na zilifunua yale wao walikuwa wameyaacha; yale Luther aliacha; yale aliyoacha Wesley; na wale watengenezaji wote, na Wapentekoste, na kuendelea hadi wakati huu.

147 Sasa, kitu kilichobaki ni kule kugeuzwa kwa Kanisa, kule kurudi kwa Musa na Eliya, ule Utawala wa Miaka Elfu juu ya dunia yule Bibi-arusi akiwa pamoja na Bwana—arusi kwa miaka elfu, kisha ile hukumu, halafu kuangamizwa kabisa kwa dhambi. Haitakuwako tena wakati huo.

148 Sasa, si... Koma... zile Muhuri haikumaliza wakati. Wakati au majira yatakuwepo hadi baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu. La! Bado kutakuwa na wakati hadi baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu.

340. Je, ule Utawala wa Miaka Elfu sharti uwe miaka elfu hasa? Ingewezekana kuwa ni kizazi kimoja?

149 La! Kizazi kimoja katika Biblia kimepewa miaka arobaini. Lakini biblia ilisema, "Nao waliishi na kutawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu." Itakuwa miaka elfu juu ya dunia, kwa sababu miaka elfu juu ya dunia ni wakati tu uliohesabiwa, kwa mfano kwa Mungu, kama siku moja. Miaka elfu juu ya dunia

ni siku moja tu kwa Mungu, kama Mungu akihesabu wakati. Wangapi wanafahamu hilo sasa?

¹⁵⁰ Kwa hivyo, ni hiyo siku ya Sabato wakati Kanisa halitasumbuka tena dhidi ya dhambi. Na Shetani atafungwa kwa muda mchache, miaka elfu, kwa sababu raia wake wote wako kuzimuni, na... Kanisa lililo duniani limekombolewa na liko katika uwepo wa Kristo kabisa, kwa hivyo yeye hawezi kufanya lo lote. Kwa hivyo, si nyororo, kama nilivyosema, nyororo ndefu, ni nyororo ya hali ya mambo; hana la kufanya. Yeye ni hoihoi na amekata tamaa anangoja tu kufufuka kwa raia wake; ndipo watabaguliwa kama vile wabaguliwayo kondoo na mbuzi.

341. Je, si yule Malkia wa Sheba alimjia Sulemani kumjaribu—kumjaribu ajionee mwenyewe kama—kama jina la Bwana lilikuwa Sulemani au la? (Siamini napata hilo. Ngoja.) Je, si yule Malkia wa Sheba alimjia Sulemani kumjaribu ajionee mwenyewe kama jina la Bwana hakika lilikuwa Suleimani au la? (Labda si—sielewi hili. Hebu... Kunradhi kwa dakika moja hivi. Hebu nilisome tena). Je, si yule Malkia wa Sheba alimjia Suleimani kumjaribu ajionee mwenyewe kama jina la Bwana hakika lilikuwa Suleimani au la?

¹⁵¹ La! Yeye hakumjaribu kamwe kuona kama—kama jina la Mungu lilikuwa Suleimani. Suleimani alikuwa mfalme. Yeye alikuja, naye kasema, yeye—yeye alisema, “Hakika Mungu yuko pamoja na mfalme Wake na pamoja na watu Wake.” Ona? Yeye alikuja na akajaribiwa—Malkia yule alimjaribu Suleimani kuhusu karama yake, kwa sababu yeye alikuwa na mambo moyoni mwake ambayo Suleimani alimfunulia, ambayo yalionyesha ya kwamba yeye alikuwa mfalme wa Mungu juu ya nchi.

¹⁵² Mwakumbuka chini kule, naamini, chini kule—kule—kule ambako yeye alitoka, chini kule katika ile nchi ya—ya—ya—ya Sheba alikotoka, watu wale wangepitia kule, mwajua, na—na kuna habari za mambo makuu yanayotendeka, ya kwamba walikuwa na Mungu kule chini aliyemtia mfalme wao mafuta, na—jinsi yule mfalme alivyotiwa mafuta na Mungu. Siamini yeye alidhani kuwa jina la Suleimani—au jina la Mungu lilikuwa Sulemani, kwa sababu kama yeye alifanya hivyo, hilo lingemfanya yeye kafiri tena. Ona? Kwa hivyo, yeye—yeye angalifanya hilo. Moyoni yeye angedhani kuwa Mungu alikuwa Suleimani—Suleimani alikuwa Mungu, kwa sababu yeye kwanza alikuwa kafiri. Lakini Suleimani alipomfunulia siri ya moyo kwa ka—karama ya upambanuzi—ambayo iliitwa wakati huo, hekima—yeye alipopambanua hayo, yeye alijua kuwa Mungu alikuwa pamoja na Suleimani, kwa sababu basi... Wao walikuwa... Yeye alitambua... Kama yeye alikuja na hilo niani mwake...

153 Kama yule—kama mtu yule yuko hapa, yule aliyeuliza swali hili, anauliza, “Je, yeye basi alijua ya kwamba kweli Suleimani—jina la Bwana lilikuwa Suleimani kweli?”... Ona? Suleimani hakuwa Bwana; yeye alipata hayo kwa watu, kwa sababu wao walimwabudu Yehova, na kulikuwako lile sanduku kubwa, na lile agano kubwa, lile—lile sanduku mlimokuwemo zile amri za Bwana. Nao walimwambia kuhusu Mlima Sinai na mahali mbalimbali ambapo walikwisha kuwepo. Ndiposa, yeye angeona kuwa Mungu—kuwa Mungu wa agano hilo alikuwa ndani ya mtu huyu, kwa sababu yeye alikuwa na—yeye alikuwa na upambanuzi ambao ulikuwa wa Mungu pekee. Ona? Kwa hivyo yeye alijua kuwa—kuwa Mungu alikuwa katika Suleimani. Lakini sasa, huenda ingesomeka hivyo kama yule aliyeuliza aliuliza hivyo. Lakini, “Je, yeye alijua kuwa jina la Bwana hakika lilikuwa Suleimani?” Labda hao hawakuliandika tu jinsi walivyokuwa wakiwazia. Mwaona? Kwa hivyo nadhani labda wao wangesema—wangesema hivi: “Kuwa Bwana alikuwa katika Suleimani.” Naam, hakika Yeye alikuwa. Kwa sababu kama swali ndilo hilo, hakika! Yeye alimjua Mungu, kwa sababu yeye alitoa matamshi hayo. Naye hangemwabudu Mungu mwingine. Nami naamini yeye—yeye alisema alikuwa kila mara... Yeye aliona sababu... Hakuwa na pumzi iliyobaki ndani yake; hakuwa na swali lilosalia ndani yake. Suleimani alifunua tu jambo lote, naye alijua Mungu alikuwa pamoja naye.

342. Tuli—tuliozwa miaka ishirini na mmoja iliyopita na hakimu. Je, ilikuwa—ilikuwa kosa?

154 Ndiyo, ilikuwa kosa kwenu kufanya hivyo. Ndoa ni ya nyumba ya Mungu. Lakini kwa kuwa mmeoana, hapa ndipo mnapoana hakika: mnaoana mnapowekeana nadhiri ninyi kwa ninyi, mnapoahidiana ninyi kwa ninyi ya kuwa mna—ya kwamba mtaoana. Hakimu anaweza kuwapa ninyi cheti, hayo ni mambo ya kisheria, ya kuishi pamoja kama mume na mke bila kuwa mwanamume wa kimila au mwanamke wa kimila. Lakini unapomwahidi msichana huyu na huyu—unapomwahidi mwanamume huyo kuwa utakuwa mwaminifu kwake, na unamchukua yeye kuwa mumeo, umeolewa basi. Mnakumbuka, nilieleza hayo juma lililopita, naamini ilikuwa wakati huo. Ona? Unapomwahidi msichana yule. Ona?

155 Hata katika ya kale—katika Biblia ya kale, kama mwanamume alikuwa amemposa mwanamwali, na (mwajua sheria kuhusu hilo. Naam, ilikuwa tu sawa na uzinzi. Bila shaka!) yeye alipomwahidi, imekwisha.

156 Swali liliulizwa majuzi, “Je, kutangua ndoa—kutangua ndoa—kutangua ndoa ni sawa na kutaliki?” Ona? Mnaponiuliza maswali hayo, rafiki, hamjui hilo lanifanyaje mimi. Nina marafiki wengi wanaoketi hapa ambao wameoa mara mbili au tatu. Je, mlitambua nanena kuhusu mwanangu binafsi, Billy Paul? Je, ningemwachilia Billy Paul? Hapana kamwe! Billy

Paul alimwoa msichana fulani, kisha akaja, na kusema, “Baba, nataka kuoa.”

¹⁵⁷ Nilikuwa nikisafisha motokaa yangu; nikasema, “Piga pembe ukuta,” nikaendelea tu kusafisha motokaa yangu hivyo.

Yeye alisema, “Nataka kuoa.”

Nilisema, “Jamani, endelea,” niliendelea tu hivyo. Yeye akaenda akamwambia mama yake, na mama yake akamchekelea. Mwajua alifanyaje? Akatoroka na mtoto mdogo ambaye bado alikuwa kwa shule ya msingi wakaoana. Sisi tulitangua arusi ile, mimi na baba wa msichana huyu. Sisi tulitangua arusi ile, lakini yeye aliisha oa haidhuru. Yeye ni mwanangu anayeketi hapa akinisikiza mimi sasa. Naam, hiyo ni kweli hasa.

¹⁵⁸ Yeye alinijia mimi na msichana anayeishi naye sasa, mkwe wangu. Mjukuu wangu mdogo... Yeye alisema, “Utanioza baba?”

¹⁵⁹ Nilisema, “Hapana kwa vyo vyote vile.” Huyu ni mwanangu. Mwadhani hilo halinimumizi hadi ndani kabisa wakati nilipombeba mikononi mwangu na kufanya lo lote nililoweza, na nimekuwa kwake baba na mama? Mwadhani hilo haliniui mimi kusema hivyo? Lakini ni Kweli. Hakika! Mwanangu akiketi hapa akisikiza... Mkwe wangu na mjukuu wangu wanaketi papa hapa sasa... Lakini namwambia yeye ni kosa (ona?), kwa sababu yanipasa kufanya hivyo. Nina wajibu kwa Neno hilo.

¹⁶⁰ Nami nasema, uliozwa na hakimu? Ulipaswa kuozwa na kanisa, na mhudumu. Hilo ndilo jambo la heshima Mkristo analopaswa kufanya. Lakini kwa kuwa wewe umekwisha toa ahadi hiyo, na nadhiri, na ulioa miaka ishirini na moja iliyopita, nadhani ni sawa.

Mnasema, “Vema nina-...”

¹⁶¹ Huenda swali likawa, “Je, yanipasa kuja na kuozwa tena?” Ukipenda. Usiwe na jambo lo lote niani mwako linalotatiza imani yako, kwa sababu kama kuna lo lote mle, huwezi kuendelea zaidi ya papa hapo; utakomea papo hapo. Wakati hiyo alama ya kuuliza ijapo, hapo ndipo utakapokomea, papo hapo. Lakini sasa, kwangu ingekuwa sawa.

¹⁶² Mtu yule aliyenibatiza kwa Jina la bwana Yesu Kristo mwishowe alinifukuza kanisani, kwa sababu singekubaliana naye kuhusu wahubiri wanawake. Vema, hilo halikunifanya nibatizwe tena. Ona? Naam, la. Ona? Hilo ni sawa.

¹⁶³ Lakini kumbuka tu, haya yananichoma moyo. Nina marafiki wapendwa sana wanaoketi hapa, wanaume kwa wanawake ambao—wangechukua—kuwekwa—kung’oa macho yao na kunipea mimi kama ningewaomba (naam, bwana!), nao wameoa mara mbili, wakati mwingine mara tatu, wanaoketi papa hapa sasa. Na mwanangu, mjukuu wangu, mju—na mkwe wangu

ninayempenda... Mtazame Billy, jinsi nilivyomsaidia na jinsi alivyonisaidia, lakini kusema kweli au kweli, ni kweli ya kweli.

164 Nina... ningeenda nje pale leo na kuita baadhi ya hawa Wa-Assemblies of God au baadhi ya watu hawa na kuwaambia, "Nina—nina—nilikosea pote, sitadumu kwa Neno, nitakaa pamoja nanyi." Ngingekuwa labda mtu mashuhuri sana hivi karibuni na karama ya Mungu. Kutupa ushawishi wangu kwa mojawapo ya madhehebu hayo, ngingekuwa labda na jina kubwa kati yao. Sijali kuhusu jina langu kati yao. Nawapenda, hiyo ni kweli. Lakini yanipasa niwe mwaminifu. Ninge—ninge—ningekuwa mnafiki kama ningefanya hivyo.

165 Nami—ningekuwa mnafiki kama ningesimama hapa kwa sababu mwanangu anayeketi hapa aliahidi msichana, nami nilisema... Kama—kama hata hakuwahi kufanyiwa sherehe, haidhuru kama yeye aliishi na mwanamke yule kamwe, au akalala naye, au lo lote lile, yeye aliweka hiyo nadhiri, yeye ameo, Billy Paul au si Billy Paul. Hiyo ni kweli hasa! Yeye alioa wakati alipotoa ahadi hiyo. Kama ni mimi, ni vivyo hivyo.

166 Yatupasa kuwa waaminifu. Kama siwezi kuwa mwaminifu kwa mwanangu, siwezi kuwa mwaminifu kwenu. Kama mimi si mwaminifu kwenu, sitaweza kuwa mwaminifu kwa Mungu. Nami nawatakeni muamini yale ninayowaambia kuwa—ni maoni yangu mwaminifu. Msiwazie mengine juu yake, semeni tu jinsi nisemavyo (ona?), kwa sababu nitawaambia yaliyo Kweli.

167 Sasa, siongei nanyi nyote hivyo mara kwa mara, kwa sababu ninyi mu watoto wangu, nawaita. Nimewazaa ninyi kwa Kristo kupitia kwa Injili. Nasi tukiwa hapa pamoja, kundi letu tu limeketi hapa, ni—ninawanyoa kidogo. Ila nataka kuwaambieni: lakini manapokuja kwangu na kuuliza lo lote, nitawaelezeni kadiri nijuavyo! Kama liko katika Neno, sijali kama linanihukumu mimi, nina mafundo mengi ambayo yapaswa yakatwe na kuondolewa kwangu. Hakika!

168 Lakini mnaponiuliza jambo lo lote, nitawaambieni. Kama nikiwambieni jambo lo lote, nitawaambieni. Kama nikiwambieni jambo lo lote, nitawaambieni yaliyo Kweli. Mimi kila mara nimejaribu kuishi hivyo. Hivyo ndivyo ninavyotaka kuishi na kufa hivyo, nikiwa mwaminifu kwa ye yote.

169 Msichana mdogo alinijia si muda mrefu umepita; mwanamke huyo hayuko hapa sasa. Tom Simpson, wengi wenu mnamjua. Tom ni mtu mzuri; hakuna ye yote wa watu wake aliye hapa. (Nadhani watu wale wote walirudi, isipokuwa Fred awe yuangali hapa. Mimi... Fred Sothmann, sijui kama yeye yuko hapa au la, lakini ni—ninadhani wako). Lakini Tom Simpson, wao—yeye alishuka akaja toka Canada pamoja na—na Fred. Nao... (Mnamjua Ndugu Fred, mdhamini wetu).

170 Na Ndugu Tom, wengi wenu hapa mnamjua. Na Tom ni mtu mzuri; yeye ni mtu mpendwa; vivyo hivyo na Bi. Simpson

pia. Laiti Bi. Simpson angelisikiza yale ninayomwambia yeye pia atatembea tena. Naye anaketi katika gari la kusukumia wagonjwa akiwa kiwete. Yeye atatembea kama atafanya tu yale aliyoambiwa afanye. Nanyi tazameni tu muone kama hilo si kweli. Ona? Sasa. Lakini yeye apaswa afanye yale yeye aliyoambiwa afanye kama yeye anatarajia kufanya hivyo.

¹⁷¹ Na mmojawapo wa wasichana wake wadogo, wasichana wapendwa . . . Mimi . . . Walipokuwa wachanga, ningewashika pajani mwangu na kucheza nao. Wao ni wakubwa sana sasa; karibu wawe wanawake, umri wa miaka kumi, kumi na miwili. Na kwa hivyo, mmoja wao alinjia akasema, “Ndugu Branham, nilikuwa na ndoto.” Naye akanisimulia ndoto ile. Naye akasema, “Nini maana yake?”

Nilimwambia, “Sijui, kipenzi. Nitaomba, na Bwana akinipa, nitakwambia.”

¹⁷² Yeye kasema, “Vema!” Siku chache akarudi akauliza, “Umepata ndoto hiyo?”

Nilisema, “La, kipenzi sijaipata; Yeye hajanifunulia.”

¹⁷³ Yapata juma moja au mawili baadaye yeye akarudi, kasema “Ndugu Branham, na ile ndoto je?”

Nilisema, “Sijui.” Vema, ilionekana kama yeye aliudhika. Mimi . . .

¹⁷⁴ Kumbukeni, mnaponiuliza niwaambie lo lote, nami silipati toka kwa Bwana, mimi pia huudhika. Lakini sitakuwa mnafiki, au mwongo, nitawaambieni yaliyo kweli. Yeye akiniambia, nitakwambieni; Yeye asiponiambia, sitawaambieni. Hilo tu ndilo niwezalo kufanya. Nami nawatakeni mnamini hivyo.

¹⁷⁵ Na sasa, nilidhani nilijua maana ya ndoto hiyo mawazoni mwangu, lakini nilijua. Yanipasa kuona kitu kile tena. Na hakuna hata mmoja wenu awezaye kuelekeza kidole chake wakati wote au mahali po pote, ambapo niliwahi kuwaambia ninyi tafsiri ya ndoto katika Jina la Bwana ila iliyokuwa vivyo hivyo hasa. Naam, bwana! Sijapata kuwaambia lo lote katika Jina la Bwana ila lile lililotimia pia, hivyo tu, kwa sababu nina—ni—ni Yeye. Na ndipo si wajibu wangu wakati huo, ni Yeye; ni wajibu Wake.

¹⁷⁶ Nilisema, “Tazama, Trudy, vipi kama tunaenda Arizona. Na vipi kama—kama nilikwambia wakati huo ya kwamba utakapofika kule, ‘BWANA ASEMA HIVI,’ ndugu yako mdogo anaenda (Yohana mdogo, yule ninayemsumbua kuhusu tumbo lake kuwa wazi wakati wote). . .” Nilisema “Vipi kama akikanyagwa barabarani nami niseme, Wajua nini kitatendeka, yeye atakanyagwa barabarani”; na unanijia na—na unasema, ‘Ndugu Branham . . . Nenda kampelekeni kwa Ndugu Branham,’ ama hivyo. Na ndipo unaenda kunitafuta hapa na pale, na utanikuta mimi nimesimama kwenye vipandio nikiongea na

mtu fulani aliyevalia suti nyeupe. Ndiposa, naenda tu kuweka mikono yangu juu ya mtoto Yohana; naye atafufuka tena na kukimbia.” Sasa, kasema, “Ndipo unaenda Magharibi, na muda si muda, siku moja utasikia mama yako akilia, baba yako akilia, na tazama, na mtoto Yohana amekanyagwa. Ungefanyaje?” Ona? Unaniamini. Ona? Nami nawatakeni muwe na tumaini kwangu. Siendi kuwaambia ninyi lo lote kwa kubahatisha tu; nitawaambieni yaliyo kweli, au nisiwaambieni lo lote. Nami nilisema, Ndipo unanijia na kusema, ‘Ee, maskini Yohana’—au unamwendea mama yako, ‘Ee maskini Yohana amekanyagwa. Yeye amekufa! Yeye amekufa!’

¹⁷⁷ Daktari yule aja, anayafungua macho yake, apima moyo wake, kupumua kwake; “Yeye amekufa; mpelekeni kwenye chumba cha maiti.” Ungefanyaje?

Utamwambia, “Ngoja kidogo! Ngoja kidogo! Nitambeba kwa mikono yangu; hebu tuanze kutembea.” Amina!

“Unaenda wapi, Trudy?”

“Sijui.”

“Una nini?” Umebeba maskini ndugu yako aliyekufa mikononi mwako. Unatembea barabarani. Watu wanasema, “Je, msichana yule amerukwa na akili?” La, bwana! Yeye ana BWANA ASEMA HIVI. Kipi kitatendeka?

¹⁷⁸ Muda si muda unamwambia baba yako na mama, “Ngoja, tutampata Ndugu Branham. Yeye atakuwa amesimama kwenye vipandio akiongea na mtu aliyevalia suti nyeupe. Yuko pale amesimama papo hapo. Tazama nini itatendeka.” Huna tashwishi katika mawazo yako. Unatembea juu pale na kusema, “Ndugu Branham, unakumbuka yale uliyoniambia.”

“Naam, Trudy. Yohana, amka!” Anaruka na kukimbia kule chini barabarani.

¹⁷⁹ Lakini vipi kama nilibahatisha tu kukwambia mambo fulani niliyodhani tu ni sahihi, na kukwambia hivyo, BWANA ASEMA HIVI, na si sahihi, na lisitendeke, halikutimia; ndipo ungeogopa sana kifo cha mvulana yule. Hungejua kama umlete au la.

¹⁸⁰ Mungu alinituma mimi hapa kuwasaidia, nami nataka kuwa msaada kwenu. Na haijalishi hata kama linanichoma, moyo, linaumiza au vyo vyote vile, yanipasa niliseme haidhuru.

¹⁸¹ Lakini sasa kuhusu ndoa na takala, nimewauliza ninyi kama ndugu, tulieni hadi mtakaposikia toka kwangu. Mnasikia? Endeleeni tu kama mlivyokuwa mkiishi. (Nachukua muda mwingi mno pale).

¹⁸² “Tuliozwa miaka ishirini na moja iliyopita (naam)... hakimu.” Dada mpendwa, Ndugu mpendwa, wakati mmoja mwuzaji alikuwa akiniambia yeye aliingia kanisani (yeye alikuwa Mkristo) kule Connecticut au mahali fulani juu pale, kanisa kuu mno, aliingia tu ndani kuomba. Halikuwa—

yeye hakuwa Mpentekoste, lakini yeye aliingia ndani mle kuomba. Naye kasema yeye alipoingia mle na kupiga magoti kanisani kuomba. . . Kasema yeye alikuwa akiendesha motokaa, alikuwa amechoka, na ana tamaa sana ya nyumbani, yeye ni mwuzaji, naye anauza bidhaa, naye kasema—viwandani. Naye aliingia ndani mle ku—kununua bidhaa au kitu cho chote kile, ndiposa yeye akapitia karibu na kanisa, akawazia, “Nitaenda. . . naamini nitaingia nikaombe.” Milango i wazi; kasema, yeye akaingia. Hakumsikia mtu ye yote, kwa hivyo akapiga magoti akaanza kuomba. Baada ya yeye kuomba pale, akakaa karibu saa moja, kasema, moja kwa moja yeye alisikia mlango fulani ukifungwa au cho chote kile; yeye alidhani ni bawabu au mtu fulani kanisani. Kasema, baada ya muda mchache akaona akija—yeye alimsikia mtu fulani akiongea. Akanyemelea juu pale na akatazama, na kutazama hapa na pale kuona kama alikuwa ni bawabu. Ilikuwa ni mwanamume na mwanamke wakisimama mbele ya madhabahu wameshikana mikono, kasema, “Nakuchukua mpenzi kuwa mke wangu halali wa ndoa.” Ona?

Yeye kasema, “Nakuchukua wewe, mpenzi, kuwa mume wangu halali wa ndoa.”

“Mbona,” yeye alisema, “hili ni jambo geni,” kasema, huu Upentekoste, yeye kasema, “mwanamume huyu na mwanamke wanaoana bila mhubiri.” Ona? Na kwa hivyo yeye aliketi tu chini na kungoja; na baada ya wao kuwekeana nadhiri zao kuishi waaminifu wao kwa wao, kifo tu ndicho kingewatenganisha, wakakumbatiana, wakabusiana, wakageuka na kuondoka wakitabasamu. Yeye alisema, “Ngoja kidogo!” Yeye kasema, “Nina hamu sana kujua; mimi ni mgeni.” Kasema, “Ninyi mnafanya arusi?”

Kasema, “Naam!”

“Bila mhubiri?”

Mwanamume yule kasema, “La!” Kasema, “Tumeona miaka arobaini.” Akasema, tulifanya ndoa papa hapa kwenye madhabahu haya miaka arobaini iliyopita, na kila mwaka tunarudi tena kufanya upya nadhiri zetu.” Hilo ni wazo zuri. Ona?

¹⁸³ Lakini kwa habari za ndoa, unapomwahidi mwanamke huyo, yeye anachukua neno lako; wewe unachukua neno lake; na Mungu anachukua maneno yenu nyote mawili. Ona? Kwa hivyo usiahidi isipokuwa. . . [Upande wa kwanza wa kanda waisha—Mh.]

343. Wanapoikata katika. . . Je, ndefu—je, nywele ingali ndefu wanapoikata upande wa mbele? (Sasa, ngoja kidogo, hebu nipate hili hapa). **Je, nywele ingali ni ndefu wana-. . .**

¹⁸⁴ Vema, huenda ni—nime—wanakusudia hili: “Je, nywele ingali ndefu wanapoikata mbele?” Si ndefu tena, wameikata.

Ona? Lakini kama mwanamume aliyekata suruali yake ndefu mara tatu na bado fupi sana. Wasemaje? Wasemaje? [Ndugu Branham aongea na mtu fulani katika kusanyiko—Mh.] Ee, hilo ndilo wanalonena habari zake. Kama ninavyomsumbua-sumbua msichana wangu mdogo, yeye alisema... Ule “mkatoo” nauita, mwajua, chapa, au yo yote ile, mnajua, kupitia upande wa mbele hapa.

¹⁸⁵ Vema, nadhani hao watoto wanaokata nywele zao upande wa mbele... Wewe—labda huenda mama yako angekwambia kuhusu hilo (ona?), kama anakutaka ufanye hivyo. Nafikiri ingeonekana kama—kama maskini huyo mwanamke alikuwa akitazamia kioo cha kutazamia nyuma kama yeye amepita yapata umri wa miaka ishirini na mitano na alitaka kuzikata upande wa mbele hivyo, aonekane kama mtoto. Tazama nje hapa unakoenda, dada, si kule ulikokuwa. Ona?

¹⁸⁶ Na sasa, lakini kukata nywele, ni—ni—ni—ninakwambia hili. Siwezi si—si—sina Andiko lo—lo lote la kusema unaweza kukata kiasi hiki na huwezi kufanya vinginevyo. Si—sina Andiko lo lote kwake, si—singe kwambia hilo, dada, au ndugu, awaye yote.

¹⁸⁷ Nasema jambo moja. Laiti... Sasa, najua watoto wangu wamefanya hivyo pia, Rebeka na Sara, nimeona wakikata nywele zao upande wa mbele hapa, na kuzisuka nyuma kule upande wa nyuma, na kufanya vitu huku mbele, hivi. Si—sipendi, mimi... Sasa, si kuwahukumu. Ona? La, bwana! Kwangu, laiti hawangeingiza makasi kwenye nywele zao kwa vyo vyote vile. Lakini zinapokuwa zote ndefu, zikining'inia chini hivi, na kuzikatakata upande wa mbele kuziondoa machoni mwao, watoto wadogo labda. Si—singejua kama hilo lilikuwa kosa, singedhani hivyo. Ona? Lakini unapopata... Kama unaweza, mimi—kwenu dada, ningeziacha tu jinsi Bwana alivyoziumba. Ona?

¹⁸⁸ Na bila shaka, najua wanawake wanataka kuonekana warembo; hayo ni maumbile, na hivyo—hivyo ndivyo iwapasavyo kuwa. Ona? Yapasa wawe hivyo. Na kwa hivyo, hilo ni zuri, ila tu msi—msiwe, ama tuseme hivi, msionekane kama ulimwengu (ona?); msiige mitingo ya ulimwengu. Mambo mabaya... Unataka zikatwe, hivyo, lakini msikate nywele zenu basi. Kama una msongo unaoning'inia chini, au—au cho chote kile ndani ya nywele zako, ziache ndefu. Msizikate zikaonekana kama ulimwengu. Kama wewe u mmoja wa hao wasichana wadogo.

¹⁸⁹ Mjomba wangu alikuwa na msichana mdogo kule—kule New York. Yeye alikuwa na nywele nzuri sana. Zilikuwa nyekundu nyeusi naye alikuwa akisuka nywele zake... Mama yangu alikuwa aki... Masongo yake ya nywele yaligusa chini hapa nyuma ya magoti yake. Na msichana huyu alikuwa na misuko kama hiyo pia; jina lake lilikuwa Jacqueline. Naye alikuwa amechana sehemu moja chini hivi na kuzikata hivi.

Na sasa, imekuwa karibu miaka kumi na mitano, kumi na minane, ishirini iliyopita. Nami nilikuwa nikishangaa, mbona yeye hakuzichana zote nyuma, ilionekana nzuri zaidi kuliko kuzifanya hivyo, kukata hapa kama hawa Beatles mamboleo walioko siku hizi, mwajua. Na . . . Ee, naam, siamini ningefanya hivyo. Cho chote kionekanacho kama hao Beatles, hicho chaonekana kama kilichotoka ulimwenguni, kwa hivyo hebu—ziache hivyo tu. Naam!

344. Mimi na mume wangu hatukubaliani katika Biblia, zile Kweli—kama Kweli hizi unazohubiri. Yeye hafahamu. Je, yanipasa niende pamoja naye makanisani hali siamini mafundisho yao? Hili linanititiza sana.

¹⁹⁰ Ndiyo! Kama wewe u mke wa mume huyu, naye hakuhukumu, hu—haikupasi umhukumu (ona?), kwa sababu mume hutakaswa na mkewe. Ona? Nami naamini, yeye akienda kwa kanisa fulani la kidhehebu au kitu kama hicho, yeye anataka uende pale naye. . . Waona? Usipoenda. . . Ona, hakuna cho chote huko kinachoweza kukudhuru, kwa sababu hutaenda kusikiza yale wanayosema haidhuru, kwa sababu umekwisha sema hapa huamini mahubiri yao. Ona? Kwa hivyo halitakudhuru, lakini unaonyesha tu heshima kwa mumeo. Unajitolea kwake, na labda katika kufanya hivyo, uta—uta. . . Kama wanafundisha na kufanya mambo chini kule. . . Umefunzwa mambo ya juu sana kuliko hayo; wewe kolea; yeye ataona na amjie Bwana. Naamini ningeendelea. Jamani, tazama hapa ni saa ngapi?

345. Je, Zekaria 4 na Ufunuo 11:3-12, yanena kuhusu mtu yule yule? Soma Zakaria 4:12-14 na Ufunuo 11:4. Waliandika jina lao kwake—Ndugu na Dada wa kanisa hapa.

¹⁹¹ Hebu tuone, Zekaria 4. Enhee, naam, hao ni wale mizeituni miwili. Naam, ile mizeitumi miwili ya Ufunuo 11 ni. . . Ee, naam, ndivyo. Kitu kile kile. Hiyo ni wote wawili. Ha—hao ni—ni Musa na Eliya, ile mizeitumi miwili.

Ombea . . . Hilo ni Ombi la maombi.

Nasikitika, siwezi kusoma hili kabla . . . Linahusu uhusiano wa kijamaa. Naam, weka hilo na hili lingine pale. Siwezi kusoma hilo hadharani. Wako kwa mahojiano ya kibinafsi haidhuru, kwa hivyo—kwa hivyo. . .

346. Ndugu Branham, je ni kosa ku—ku. . . [Ndugu Branham aongea na mtu fulani jukwaani—Mh.] Je, ni kosa kufanya kazi Jumapili?

¹⁹² Nilieleza tu hilo. Kama ng'ombe yuko shimoni, mwondoe, lakini usimsukume shimoni kusudi ukamwondoe Jumapili!

Ndugu Branham, utahubiri hapa Jumapili ijayo?

¹⁹³ Hilo ni swali tu. La, Dada, Ndugu, ye yote yule. Sasa, haya ni mengine yaliyokuwa yamewekwa hapa. Huenda yaliwekwa, au mtu fulani aliyaweka katika bahasha.

Ndugu... hili ni la kwako, Ndugu Capps. “Je, waweza kuimba, *“Hatutazeeka Kamwe?”* Huenda nililiweka ndani... Nimeyachanganyisha mengine yote.

347. Ndugu Branham, mtu fulani anataka kujua sababu gani huja— (ta—a—j—...) hujatajwa katika Biblia. Naamini wewe ni Habakuki 2:1-4. (Fungua hapo, Ndugu Neville, Habakuki 2:1-4) Hebu wasome haya na kuyasoma kirefu, sura ya 3... waza jina na mifano ya sura nne, naamini— naamini ni wewe.

¹⁹⁴ Sasa, anapotafuta hivyo, ni Habakuki 2:1-4. Ndugu au Dada, ye yote yule aliyeuliza swali lile (hamna jina; hilo ni jema), ni—nanapenda ninyi mwulize mambo hayo. Najua yaliyo moyoni mwako (ona?), ndiposa nitakwambia. La. Ona? Si lazima jina lako liwe katika Biblia (waona, ona?) lakini mradi tu uko katika Biblia, uko—mradi tu uko katika Kristo, uko katika Biblia; wewe uko ndani Yake (mwaona?) katika Biblia. Ona? Mradi tu uko katika Kristo, basi uko katika utimilifu wa Biblia. Ona? Uko katika mahali pako halisi unapokuwa katika Kristo. Nyote mwafahamu hilo?

¹⁹⁵ Je, umevipata, Ndugu Neville? Nini? Naam. Habakuki—Habakuki... Sijayasoma. Hili liliwekwa tu ndani humu, nadhani, asubuhi hii. Habakuki 2:1-4. Ndipo hapa. Habakuki 2—Habakuki 2, na 1 hadi 4:

Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwa—kwa—kwangu.

BWANA akanijibu, akasema, iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji.

Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia; ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia.

Tazama, roho yake hujivuna, haina unyofu ndani yake; lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake.

¹⁹⁶ Vema, na—nafikiri huyu mtu mpendwa aliyeuliza hili... Mwaona? Ni mtu anayenipenda, au hangeandika hilo. Ona? Sasa, singesema kuwa jina langu... Biblia haitaji jina langu—jina langu, *William Branham*, au kutaja jina lako ye yote yule, lakini sisi tuko ndani Yake haidhuru. Na hawa...

¹⁹⁷ Na sasa, unaona mahali panapojulikana palipotajwa katika Biblia, panaposema mambo fulani. Mwaona? Sasa,

ukichunguza, historia hujirudia yenyewe katika Biblia. Ona? Sasa, hebu tuwape Maandiko kwa moja sasa. (Naona wengi wenu mnaliandika). Sasa, katika ile sura ya 3 ya Injili ya Mathayo, ilisema, “Na Mungu alipomwita Mwanawe toka Misri ili yatimie yaliyonenwa, ‘Toka Misri nalimwita Mwanangu’...” Sasa, kama una—nakala ya—ya Scofield au nakala nyingine ya Biblia yenye marejeo, ukitafuta marejeo yake pale, maandishi ya pambazoni, yatakurejeza nyuma ambapo Yeye alimwita Yakobo, Israeli, toka Misri. Ona? Lakini Yakobo alikuwa mwanawe ambaye Yeye alimwita toka Misri; pia Yesu alikuwa Mwanawe ambaye Yeye alimwita toka Misri. Kwa hivyo (Ona?) Neno la Mungu halina mwisho. Ona, sisi hujitambulisha wenyewe katika Biblia kwa... Wangapi wanakumbuka ujumbe wangu juu ya kujitambulisha mwenyewe na tabia ya Kikristo, Phoenix. Arizona, nilipouhubiri? Naam, wengi wenu mnao kwenye kanda. Ona? *Unaweza Kujitambulisha Mwenyewe na Tabia ya Kikristo.* Ona? Unaweza kujitambulisha mwenyewe po pote unapotaka katika Maandiko kama wewe ni Mkristo, na kama wewe si Mkristo, unaweza kujitambulisha mwenyewe katika Biblia. Ona? Kwa hivyo nadhani labda hilo lingesaidia. Nataka kufikia mengi ya haya niwezavyo.

348. Ndugu Branham, wengine wanasema kuwa neema imekwisha na hakuna ye yote awezaye kuokolewa. Sasa, hili ni kweli? (Nina furaha nilipata hili). Sisi hukeshwa na kuomba—sisi hutazama mistari ya maombi na inaonekana bado wengine wanapata neema.

Sasa, hilo ni swali la **kwanza, unayo mawili.**

¹⁹⁸ “Neema imekwisha?” Usithubutu kuwazia hivyo! Ona? Endelea kufanya kila kitu uwezacho hata utakaponyakuliwa. Ona?

¹⁹⁹ “Twatambua katika mistari ya wanaohitaji maombi wengine wanapata neema.” Hakika! Neema ni—milango i wazi. Ona? Nadhani unakoenda, hili—wazo hili huenda likawa kati ya... Ona, sina wakati wa kupea kila moja ya haya Maandiko mahali pake panapofaa, (mwaona?), kila moja ya mambo haya mahali pao panapofaa. Wao...Katika mstari wa maombi unapata neema, hakika.

²⁰⁰ Kama nilijua Yesu yuaja adhuhuri ya leo, ningeendelea tu kufanya jambo ninalofanya sasa hivi (ona?), nikiendelea tu. Neema i wazi daima. Ona?

²⁰¹ Na sasa, ninapodhani unaipata, ni kuhusu kule kumalizika kwa zile Nyakati Saba za Kanisa na zile Mihuri Saba kufunguliwa. Ona? Zile Mihuri Saba, zimedhihirisha yale yanayotendeka yame—yamekwisha tendeka. Zile Nyakati Saba za Kanisa, sisi tuko mwishoni mwa ule Wakati wa Kanisa la Saba. Ninaposema *mwishoni* hilo halimaanishi saa ii hii, dakika ii hii. Mwakumbuka, Biblia ilisema kule nyuma

katika nyakati za—za Bwana Yesu, Paul alisema, “Kwa kuwa wakati umekaribia.” Je, unatambua huo ulikuwa urefu gani katika wakati wa Mungu? Huo ulikuwa jana. Kwa wakati wangu imekuwa miaka elfu mbili. Ona? Wakati u karibu. Ona? Kile Mungu anasema *kimekaribia* si kile tunachosema *kimekaribia*. Ona?

²⁰² Kwa hivyo endelea kuamini, endelea kuomba, endelea... Mungu bado ana neema wazi; endelea tu kuiendea upesi uwezavyo. Mungu ataikomesha wakati utakapowadia wa kuikomesha. Ona?

349. Sasa, Ndugu Branham, je ni kweli kuwa hakuna mtu anayepaswa kuhubiri ila wewe? Tumeona—tumekuona ukiwawekea watu mikononi. Hatu...hatuamini wewe ungefanya hilo kama hawapaswi—kama hawapaswi kuhubiri.

²⁰³ Jamani! Ndugu, Dada, ye yote aliyewahi kukwambia hakuna ye yote anayepaswa kuhubiri ila mimi, hakika ningekuwa raia duni kwa Mungu na hayo yote. La! Kila mtu au—kila anayesikia wito wa Mungu juu ya maisha yake, aingie katika huduma na aanze kuhubiri; tunawahitaji.

²⁰⁴ Watu wa Mungu wanatiwa mafuta ulimwenguni kote kuhubiri Injili. Ona? Mimi ni mmoja wa changarawe ndogo ukingoni kati ya mawe mengi makubwa. Ona? Kwa hivyo mimi...Kunao wengi wanaofaa zaidi, wanaostahili sana, walio bora kwa kila njia kuhubiri kuliko mimi; mimi ni mmojawapo wa walio wadogo, mtu mnyenyekevu nje hapa. Mimi ni punje moja ya ngano katika ghala lote. Ona? Kwa hivyo hilo tu... Mwajua lile ninalokusudia!

²⁰⁵ Mtu ye yote aliyelitwa na Mungu yampasa kuhubiri Injili.

350. Mkristo awezaje kuingia zaidi katika upendo wa Mungu?

²⁰⁶ Soma Neno na kuomba. Soma Neno la Mungu na kuomba. Nitaharakisha, nipate kuyafikia mengi niwezavyo.

Nilileta swali moja, lakini (s—i—k—u—l) sikuliuliza vizuri. Nataka kujua kama utakuwa na ibada ya uponyaji kabla Hujaondoka mjini. Kama sivyo... yanipasa ni—nipate mahojiano ya kibinafsi pamoja nawe?

²⁰⁷ Sasa, walakini, nadhani mtu huyu alikuwa kwa mahojiano asubuhi hii. Bila shaka tulikuwa na ibada ya uponyaji—tumekuwa na ibada ya uponyaji pia.

351. Ndugu Branham, tafadhali fafania I Wakorintho—I Wakorintho 11-11 na kifungu cha 4 hadi 6. Je, haya yanamaanisha kifuniko tofauti na nywele, au je, nywele ndefu ndiyo kifuniko pekee tunachohitaji? (Nifungulie I Wakorintho 11. Hebu tuone, I Wakorintho 11:4). Inasema tunapoomba...(Ee naam, yeye—alilipata hapa. Wanasema,) Katika kuomba au kuhutubu tunaweza

kutoa nywele zetu, tunaweza... (Hebu tuone, wana mstari uliochorwa kupitia kwa kitu fulani hapa). **Wakati tunapohutubu—wakati tunapohutubu je, twaweza kutoa nywele zetu wakati...** (U—unasema,) **Je, tunaweza kutoa nywele zetu au kuzitoa tunapotabiiri?**

208 Kama una—una nywele bandia, labda unaweza, lakini ninge—au kuvaa mojawapo wa hizi nywele bandia za Beatles, au cho chote kile, lakini... Kama ningeonekana sawa nikiwa na moja, labda ningalivaa moja mimi mwenyewe, lakini si zile nywele bandia za Beatles, lakini nywe—nywele bandia.

209 Lakini hilo ni sawa. Kama huna nywele zo zote na unataka moja. Kama unaweza kufanya hivyo, hilo ni nzuri kabisa. Naam, bwana! Kama nimwanamke, nywele zake si ndefu kutosha, naye anataka kishungi mle, ningesema, kiva, Dada.

210 Kama mtu ana homa mbaya na kadhalika, na anataka—kwa njia yote—hata kwa kuonekana kwake mbele ya mkewe, kama huyo mwanamume ataka kuvalia nywele bandia, mfanye hivyo. Naam, hakika. Hilo si baya (la, bwana!) si zaidi ya vile vile ingelikuwa kwa meno yako, au mkono bandia, au cho chote kile. Kama maumbile yanayo—yamekunyima kitu fulani na—ni muhimu sana kwako endelea, hilo ni sawa kabisa.

Lakini hapa lasema, “Je, tunaweza kuvalia nywele zetu au kuzitoa tunapoomba au kuhutubu?” Hili linamaanisha nini hasa?

211 Vema, soma, Ndugu Neville... kama 4-4 hadi 6, vema, vema.

Kila mwanamume asalipo au anapohutubu, naye amefunikwa kichwa, yuaaibisha kichwa chake. (Hiyo ni kusema, kama yeye ana nywele ndefu. Vema)

Bali kila mwanamke asalipo, au anapohutubu, bila kufunika kichwa, yuaaibisha kichwa chake;... (Hiyo ni mumewe)...kwa maana ni sawasawa na yule aliyenylewa.

Maana mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele... (Kama yeye ataka kufupisha nywele zake, mfanye ainyoe yote. Ona? Kama hawezi kuwa na...)...
Au ikiwa si aibu kwa mwanamke ku—ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake au kunyolewa, na afunikwe.

212 Sioni lo lote kuhusu kuvaa na kutoa nywele pale, isipokuwa mwanamke yule anataka... Yeye asema, kama yeye yapasa aikate, basi na ainyoe yote. Ona? Kwa sababu asipofanya hivyo, na awe na nywele zake; kwa sababu nywele zake ni kifuniko chake. Lakini kwa mwanamume kufunika kichwa chake, nywele ndefu kama mwanamke, akisimama mimbarani, yeye angeonekana kama mwanamke juu pale. Ona? Kwa hivyo yeye hapaswi kuwa hivyo. Ona?

²¹³ Hilo ni—hilo linamaanisha wanavaa nywele na kuitoa... Nadhani mtu yule huenda alikosea katika kuwaza pale kuwa ilimaanisha mwa—mwanamume anayehutubu akiwa amefunikwa kichwa, basi yeye hutoa kifuniko chake. Ona? La. Hilo si ati alikuwa na nywele ndefu, yamaanisha, kama amefunikwa... Sasa, endelea kusoma zaidi kidogo, wewe uliyeuliza swali hilo, na utatambua kuwa kichwa cha mwanamume ni mumewe. Wangapi wanajua hilo? Na kichwa cha mwanamume ni Kristo; kwa hivyo, mwanamume apaswa kukata nywele zake kwa ajili ya Kristo, kwa sababu katika yeye kuna mwanamume na mwanamume, na kadhalika. Yeye ni baba, mama, dada, ndugu, wote. Lakini katika mwanamume kuna uanaume pekee. Kwa hivyo, yeye apaswa kukata hiyo kwa sababu ya Kristo; lakini katika mwanamume mna uanawake pekee, kwa hivyo yeye angeweza kuwa kifuniko chake; kwa sababu mumewe anamtawala. Yeye ni bwana wake, mtawala wake; kwa hivyo basi, yeye apaswa kuwa na nywele ndefu.

²¹⁴ Halafu basi, yeye akisema hana budi—hana budi kuinyoa, basi na anyolewe. Kisha likasema, kama ni aibu au fedheha kwake, ambaye anapaswa kuonekana mrembo, hakuwa amenyoa nywele zake zote zimenyolewa, basi na akifunike kichwa chake; na awe na nywele ndefu. Ona? Kwa hivyo ni...Ye yote... Lote limefafanuliwa? Nakusudia, je laonekana sahihi? semini, “Amina!” Kama ndivyo, kama mmelifahamu. Ona? [Kusanyiko linaitikia, “Amina!” —Mh.] Vema.

352. Ndugu Branham (Tuna dakika kumi pekee sasa.)—**Ndugu Branham, hatuna mhubiri pale tunapoishi, lakini tuna ibada ya kanda Jumapili usiku pekee. Je, tuwapeleke watoto wetu kwa kanisa lingine kwa shule ya Jumapili? Je, ibada za kanda zinatosh?**

²¹⁵ Vema, acha hilo liwe kulingana na jinsi watoto wako wanavyoendelea. Ona? Sasa, mkiwapeleka watoto wenu, wao ni wadogo; kisha muwapeleke nje kule katika kundi fulani kule nje, ambalo litawashindilia upuzi ambao wao—ambao wao—hawapaswi kujua; singefanya hilo. Kama—kama inaonekana wanajifunza ya kutosha toka kwa kanda zile na kadhalika... Nawe, tuseme, uwapeleke kwenye kanisa Katoliki, uwapeleke kanisa Katoliki, uwapeleke kwa kitu kama hicho; singekushauri hilo. Ona? Kama wao... .

²¹⁶ Lakini sasa, kama una kanisa nzuri juu pale ambalo labda halikubaliani na mambo mawili au matatu nawe, na watoto wako wanataka kwenda kwa shule ya Jumapili, wawe ni watu wa Injili nzima, cho chote kile, vema, hilo ni sahihi kabisa. Lakini ona, lakini unapofikia mahali ambapo... Inategemea jinsi watoto wako waonavyo. Ona? Tazama yale watoto wako wanayofanya, yale—jinsi wanavyotenda kwake.

353. Hebu tuone. Kama huna kanisa la kuhudhuria, yakupasa usikize tu kanda?

Naam! Hilo—ninge—mimi . . . Hilo ni sawa.

354. Je, watoto wako sharti wapate tukio fulani ili wawe na Roho Mtakatifu? Kama wao—kama—kama wao wanafahamu Ujumbe wa siku za mwisho, je, wana Roho Mtakatifu?

²¹⁷ Kila mmoja yapasa awe na tukio! Watoto wako hawawezi kuingia kwa njia nyingine yo yote ila njia ile ile unayopitia. Ona? Hawana budi kuzaliwa mara ya pili. Hakuna wajukuu katika Ufalme wa Mungu; wao wote ni watoto. Hawana budi kuwa nalo, yapasa wawe na tukio la Mungu ili waingie, kama tu ilivyo kwako. Sasa natumai naweza kupata hili. Ni . . .

355. Mpendwa sana; (Hebu tuone.) Kuhusu Maandiko ya Waefeso 4:11 hadi 13, je, sisi sote (Hebu tuone)—je sisi sote tutapata kukamilishwa kwa watakatifu kupitia kwa kanda, au yatupasa kuwa hapa, ambapo karama za Roho zinafanya kazi na afisi mbalimbali za kanisa, kusaidia kutukamilisha sisi? Mioyo yetu imeamini Neno lote la Bwana.

²¹⁸ Sasa mtu huyu anatoka Oregon. Sasa, mpendwa wangu . . . naamini najua ni nani. Ona? Ni . . . Ee, naam, namjua, bila shaka namjua. Mvulana wa—wako . . . Kama mtu yule yuko hapa, najua wewe uko—kama sivyo, huenda ilikuwa Jumapili iliyopita. Ona? Hili huenda lililetwa Jumapili iliyopita. Lakini m—mtoto wako wa kiume huendesha ndege ya hifadhi za wanyama, ona, na ni—yeye husimamia . . . Yeye ni—nadhani yeye ndiye aliyenialika mimi kwenda kuwinda kulungu pamoja nawe kule Oregon, ambako . . . Nami nadhani hii ni kweli. Sasa, namjua mtu huyu kwa barua na kwa . . . na kwa hivyo . . .

La! Wanataka kuja humu kanisani kwa ajili ya kukamilishwa. Ona? Ili sisi—sisi tupate ushirika sisi kwa sisi hapa kanisani, lakini kukamilishwa huja kati yetu na Mungu. Damu ya Kristo ndiyo inayotukamilisha katika Roho Mtakatifu.

²¹⁹ Sasa, katika kanisa unasema, ” . . . karama zinatenda kazi.” Sasa, hatuna karama nyingi sana zinazotenda kazi hapa, lakini tuna baadhi yake. Tuna karama ya lugha na—na karama ya unabii (mbili au tatu).

²²⁰ Nafikiri Ndugu wetu Higginbotham hapa, ko kote aliko, yeye ana karama ya kunena kwa lugha. Nasi tuna Ndugu wetu Junior Jackson pamoja nasi, naye hunena kwa lugha. Kisha tuna wenye kufasiri wawili au watatu. Ndugu Neville hapa pia, mchungaji wetu, hunena kwa lugha na wakati mwingine hutoa unabii, na Bwana huleta kwake . . .

²²¹ Hivi majuzi tu yeye alisema jambo fulani. Yeye alipiga simu nyumbani nilimokuwa, ya kwamba yeye alitabiria juu ya

mtu fulani, akamwambia mlevi ange—kutakuwa na mabadiliko makubwa ndani yake papo hapo au kitu kama hicho. Na huyo mtu ameshatoka kwenye Chama cha Kuwasaidia Walevi wa Kupindukia, akiwa bado mlevi wa kupindukia, na kwa siku sitini na nane hajagusa pombe hata kidogo, wala dawa yake au cho chote kile. Huyo alikuwa Ndugu Neville akitoa unabii juu yao.

²²² Kwa hivyo sisi tuna—tuna karama kadha zinazotenda kazi kati yetu, nasi tutafurahiwa sana kushiriki na ye yote wenu, apataye nafasi, anayefanya kazi, au anayetaka kuja na kushiriki pamoja nasi, lo lote tuwezalo kufanya, tuna furaha tele kwake. Ona? Lakini sasa kukamilishana ni kazi ya Kristo.

Sasa, hebu nione moja au mawili zaidi.

356. Ndugu Branham, waweza kwa hisani yako kueleza juu ya ile picha iliyochukuliwa na Ndugu Arganbright? Swali la kwanza: ya pili kwenye—picha ya pili ukutani, ile nuru inayokuzunguka wewe, ile bizimu, na mengineyo.

²²³ Vema sasa, hebu niwaambieni. Waliandika majina yao, na hawako hapa sasa. tunavifahamu. Ni Ndugu na Dada Jackson toka Afrika ya Kusini; wamerudi. Kwa hivyo twafahamu hizo; tumekwisha eleza hayo.

357. Lini kanisa ambalo—lini kanisa lililo—lililokufa katika wakati wa ile dhiki kuu—litakapofufuka? Je, wao pia watangoja hadi ule ufufuo wa wasio mcha Mungu? Je, wataishi tena katika ule Utawala wa Miaka Elfu?

²²⁴ Sasa, hilo ni swali zuri. Lahitaji zaidi ya wakati ambao ningelipea, lakini ili tu nipate... Ona? Sina... Nina yasiyopungua theluthi mbili ya yale niliyoanza nayo asubuhi hii—imechukua masaa mawili. Ni mengi sana hata siwezi kuyafikia. Mwaona? Nami nataka tu kufikia mengi niwezavyo, sikuona tu yaliko. Najua kunayo mazuri mno ndani humo pia ambayo yapasa yajulikane, kama kufafanua ule uzao wa nyoka, na mengineyo; lakini nitaharakisha na kuingilia hili upesi.

²²⁵ “Je, kanisa waliokufa katika wakati wa ile dhiki (ona?) watakuwa katika ufufuo ule?” Ule ufufuo wa pili, ufufuo wa pili.

²²⁶ “Je, wao pia watangoja hadi ufufuo wa wasio mcha Mungu?” Wenye haki na wasio haki watafufuliwa wakati mmoja.

²²⁷ “Je, wataishi tena katika ule Utawala wa Miaka Elfu?” La. Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu. Sasa, hilo ni fupi mno, lakini nina hakika. . .

358. Paulo amaanisha nini kwa kuwekwa huru na kuwa huru katika Kristo? Kuwa huru toka kwa sheria ni nini?

²²⁸ Vema, hatufungwi na sheria. Tuseme, kwa mfano, hapa kuna jambo lile lile; nitaeleza katika njia ya kawaida, upesi. Kwa mfano, nje hapa inasema nenda barabarani, maili thelathini kwa saa ndio mwendo unaopaswa kwenda. Vema sasa. Sasa nikienda

chini kwenye njia ya mji mwendo wa maili arobaini kwa saa, ninahukumiwa na sheria. Lakini nikienda tu kwa mwendo wa maili thelathini kwa saa, mimi siko chini ya sheria. Ona? Huo ndio uhuru katika Kristo (ona?) jambo lile lile.

²²⁹ Haufungi na sheria mradi tu... Kama siibi, sisemi uongo, sivuti sigara, sizini, yo yote ya mambo haya pale, mimi sihukumiwi na sheria yo yote. Ona? Mimi niko huru toka kwa sheria, mimi niko katika Kristo.

359. Waonaje kuhusu kupanga uzazi?

²³⁰ Nilikuwa na baadhi ya hayo kwa mahojiano asubuhi hii. Heri niongee binafsi na—nawe juu ya mambo hayo (ona?), juu ya mambo hayo, kwa sababu kuna maneno na mambo ambayo yanipasa kusema, ambayo mimi... Afadhali niyaseme kama mume na mke...

²³¹ Na kuna uwezekano wa kufanya jambo hilo katika njia ifaayo. Ningesema kwa—kwa maelezo ya juujuu. Kuna siku nyingi sana katika maisha ya mwanamke ambazo yeye havezi kupata mimba. Mwafahamu? Vema. Kwa nini...

²³² Naam, kuna wakati mwingine ambapo m—mtoto angemwua mwanamke, kama angelipata mtoto ingelimwua mamaye. Yakupasa uchungu hilo Ona? Kwa hivyo uwe mwangalifu sana kwake. Ona? Ona, hiyo ni kuleta uhai, kwa hivyo lile ulilowekwa hapa duniani kufanya.

²³³ Kama mkeo huugua mara kwa mara, na mtoto mwi—mwingine angelimuua, si—si—singefanya hivyo. Sidhani Bwana akutaka wewe ufanye hivyo. Nanyi—ninyi mnijie binafsi kwa mambo hayo; myalete kwenye mahojiano ya faragha. Hebu niongee nanyi binafsi (mwaona?) nami naweza kutambua...

²³⁴ Ona, kila mtu binafsi, naweza kutambua kama wananidanganya au la. Ona? Wananiambia mambo mbalimbali. Heri niwaone ninyi tu... Ona? Kwa sababu unapoliweka nje hivi, hujui. Ni kwa sababu kuna mtu binafsi na mambo kama hayo; naweza kuyatambua, kama wanasema kweli au la. Ona?

360. Kwa nini—kwa nini Shetani afunguliwa kwa muda mdogo baada ya ile miaka elfu ya Ufunuo 20 na 3, na Ufunuo 20:27?

²³⁵ Kwa nini afunguliwe? Apate kuwakusanya watu wake kwenye ule ufufuo wa pili, kwa sababu Shetani pia hana budi kusimama hukumuni. Mwaona? Hana budi kuhukumiwa.

Lo, jamani, hiki ni ki—kitabu kilichojazwa hayo. Siamini... Pia hii ni barua nyingine iliyojaa hayo. Hebu sasa niyapate hapa mengine upesi sana, sana.

361. Ndugu Branham, tafadhali fafaua Matendo 9 mlango wa 7 Matendo 20—Matendo kifungu cha 22. (Je, waweza kunitafutia, Ndugu Neville). Tafadhali fafaua Matendo 9 kifungu cha 7.

236 Sasa anapofungua hilo, nitaona kama naweza kupata lingine upesi mno. Je, mmechoka? Najua mmechoka.

Tafadhali fafanua ile siri ya kugeuzwa kwa Bibi-arusi. Itakavyotendeka na ni wapi, mahali, Bibi-arusi atakapoenda. Si ni maswali mazuri mno. Haya ni mazuri mno. Ningesimama tu hapa siku nzima . . .

[Ndugu Branham ajibu swali 361—Mh.] Hebu kidogo sasa, kifungu—kifungu. . . Matendo 9 kifungu 7 (asante, Ndugu Neville)—kifungu cha 7:

Na wale watu waliosafiri pamoja naye wakasimama kimya, wakiisikia sauti, wasione mtu.

237 Sasa, najua unapoelekea. Ona? Sasa, mahali panapofuata palisema kuwa wao—vinginevyo. Sasa, si—sijui yale yaliyotendeka pale. Siwezi kuwaambia, kwa sababu mahali panapofuata walisikia. Pamoja hawakuona, na panapofuata, waliona na hawakusikia. Wangapi wamewahi kuona hilo hapo mbeleni katika Biblia? Nimeliona, nami siwezi kulifahamu. Ona? Ni. . . Itampasa Bwana anifunulie. Ni—niliwaambia muda mchache uliopita, yanipasa niwe mwaminifu kwenu. Ona? Sijui. Nasikitika. Kama nina—kama siwezi kueleza, nitakuwa mwaminifu kutosha kuwaambia ninyi siwezi. Lakini si—sitalitua ikiwa—ikiwa sijui.

238 Siwezi kueleza hilo, maana mahali pamoja ilisema, waliona Nuru ile na hawakusikia ile sauti kamwe, au kitu kama hicho; na mahali panapofuata waliona ile—walisikia ile sauti na hawakuona kamwe ile Nuru. Siwezi kulieleza. Ona? Si—sijui ilikuwaje, nami sitajua hadi Bwana anifunulie; si zaidi ya vile ningeliwaambia kuhusu ndoa na talaka. Sikujua hadi Yeye aliponifunulia mimi.

239 Na hata asubuhi hii, Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi ajua hili kuwa kweli, asubuhi hii Yeye alimaliza jambo hilo lote, kuniambia mimi kuhusu ndoa na talaka. Naam. Hiyo ndiyo sababu nasema, hebu nikakusanye yote pamoja kutafuta . . .

240 Wakati mojawapo wa mambo hayo kama ule uzao wa nyoka, yalipotolewa kwangu si—singeyaona, lo lote; lakini niliendelea tu kufuata hilo, na muda si muda. . . Ndipo huna budi kwenda mbali sana uwe peke yako, ndiposa Roho Mtakatifu ataanza kulifunua. Sasa, nataka mtu ye yote ajaribu kuhukumu hayo sasa. Ona? Huwezi kufanya hivyo.

362. Tafadhali fafanua ile siri ya kugeuzwa kwa yule Bibi-arusi.

241 Ni mageuzi tu (ona?), miili yetu sasa. . . Hebu tuseme yetu. Mwajua lile ninalomaanisha ninaposema hilo? Sikusudii kukufuru. Sikusudii kusema *yetu*; sikusudii kusema kanisa hili; nakusudia kusema kila mwamini.

242 Ibrahimu, Yeye alikuwa akimtarajia mwana wa ahadi, yule aliyeahidiwa kwake. Sivyo? Na Kanisa linamtarajia Mwana wa

ahadi. Bibi-arusi (sivyo?), yule Bibi-arusi anamtarajia Mwana wa ahadi.

²⁴³ Kabla yule mwana wa ahadi hajapata kuwajia Sara na Ibrahimu, miili yao ilipaswa igeuzwe. Sivyo?

²⁴⁴ Yeye alikuwa mzee sana kupata mtoto. Yeye hakuwa na mishipa ya maziwa matitini mwake; matiti yake yalikuwa yamekauka. Tumbo lake la uzazi halingeweza kupata mimba; yeye alikuwa tasa. Yeye hangempata huyo mtoto; moyo wake ulikuwa umezeeka sana kustahimili utungu wa kuzaa. Kwa hivyo nini ilitendeka? Mungu alimgeuza akawa msichana tena. Naye alimfanyia Ibrahimu vivyo hivyo, kwa sababu Yeye alisema mwili wake ulikuwa umekwisha kufa. Ona? Na ilimpasa Yeye ageuze miili yao kusudi wapate kumpokea yule mwana wa ahadi.

²⁴⁵ Nasi hatuwezi kumpokea huyo Mwana wa ahadi siku hizi katika miili hii tunayoishi ndani yake; miili hii ni dhambi.

²⁴⁶ Hii dhamiri ya kwanza inaongoza mwili huu kwa kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia, na imetufarakanisha; tunatoa hoja kadhalika. Lakini huo mwili mpya, unatokana na huu aliozaliwa mara ya pili (si dhamiri hii ya kwanza, itakwisha)...Ni hicho kitu cha ndani kilicho hai. Kila mtu anayefahamu hilo asema, "Amina!" [Kusanyiko linaitikia, "Amina!"—Mh.]

²⁴⁷ Si huu wa nje kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Sio Huo sharti ufe na utakufa, lakini ile sehemu yako ya ndani, mle ndani kabisa, ndani, hiyo ndiyo mtu ambaye hawezi kufa. Ona? Na huyo ndiye mtu ambaye maisha mapya huanzia, toka kwa huku kuzaliwa kupya; na yanamjenga mtu mwingine katika mfano wa mtu huyu ambaye ni wewe, kuzunguka maisha hayo. Mwaifahamu?

²⁴⁸ Kwa hivyo mwili huo uko lakini si wazi, na ni nini? Neno lililoahidiwa kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na pale, huu huonyesha ule usio halisi; huo utaonyesha ule halisi, lile Neno. Ona? Na jambo lile lile ni—au kugeuzwa kwa Bibi-arusi kutakuwa vivyo hivyo. Lile Neno lililo ndani yako, mwili ule utaumbika kuzunguka hilo Neno, vivyo hivyo kama ilivyofanyika kwa Sara.

²⁴⁹ Kabla...Ule mwili wa kale Sara aliokuwa nao, huo mwili wa kwanza, ilipasa ugeuzwe ili umzalie mwana. Mnafahamu? Mwili huo haungeliweza kufanya hivyo. Mwili huu hauwezi kufanya hivyo. Kwa hivyo sharti ugeuzwe vivyo hivyo kumpokea yule Mwana.

363. Itatendekaje na ni lini—ni wapi—Bibi-arusi ataenda wapi?

²⁵⁰ Ataenda Utukufuni, Mbinguni kwa ajili ya ile Karamu ya Arusi, katika mfano tu kama Isaka na Rebeka, Rebeka alipoenda kumlaki Isaka. Kumbuka Eliezeri, akiwakilisha sasa ujumbe

uliotoka kwa Ibrahimu, Eliezeri aliondoka akaenda kumtafuta bibi-arusi kwa ajili—kwa ajili ya Isaka. Yeye alimpata yule mrembo Rebeka wakati wa jua kupungua, yule msichana mdogo mwenye ngozi nyeusi kidogo akija huku ameubeba mtungi wa maji. Na Eliezeri akaomba, kasema, “Bwana Mungu, nipe safari nzuri sasa na mafanikio kwa ajili ya bwana wangu, Ibrahimu.”

²⁵¹ Naye akasema, “Nenda zako, usimchukue kati ya Wafilisti—usimchukue.” Akaondoka akaenda juu pale kati ya watu wake, ikionyesha ya kwamba Bibi-arusi wa Kristo na Kristo wana uhusiano wa damu, kwa sababu Rebeka na—na Isaka walikuwa binamu.

²⁵² Na kwa hivyo wao wakashuka wakaenda, na huyu mrembo Rebeka akajitokeza na akateka maji naye akaomba—na kunywesha ngamia na mengineyo. Halafu, utatambua Rebeka alikuwa na... Chaguo la mwisho lilipasa litoke kwa Rebeka. Yeye alimsihi baba kwa ajili ya yule binti; yeye alimsihi mama kwa ajili ya yule binti; wala hakuna hata mmoja angekubali. Walimtaka yeye akae kidogo. Yeye kasema, “Msizinziue katika kazi yangu.”

²⁵³ Na Rebeka alipaswa kujiamlia, kwa sababu yeye alisema, “Yeye ndiye mwanamwali; hebu ajiamulie.”

²⁵⁴ Na mara tu alipoulizwa, akajiamulia upesi; alisema, “Nitaenda.” Naye akapanda juu ya ngamia akaenda kumlaki yule...Tazama, ngamia yule yuye yeye aliyemnywesha maji ndiye ngamia aliyembeba hata kwa bwana arusi wake na mafanikio yake yote. Na ngamia yule yule, nguvu ile ile ya (mnyama katika Biblia huainisha nguvu)...Na Nguvu ile ile tunayoipa maji na sifa (Amina! Ona), maji uzima, kusifu, lile Neno, ni kitu kile kile kinachotupeleka sisi katika ile nchi yenye utukufu kumlaki Bwana arusi. Naam, bwana! Amina!

Tukitazamia kuja kwa huo Utawala wa Miaka
Elfu wenye furaha;

Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja,
kunyakuwa Bibi-arusi wake anayemngoja.

²⁵⁵ Na kumbuka, Isaka alikuwa ameondoka hemani na alikuwa amesimama kondeni akitafakari wakati wa jioni sana. (Amina!) Yeye alipomwona Rebeka akija...Rebeka hajapata kumwona mbeleni naye Isaka hakuwa amemwona kamwe, lakini ulikuwa upendo wa kuonana mara ya kwanza. Rebeka alimpenda na Isaka akampenda, naye Rebeka hata alikuwa amefunikwa shela. Amina! Lo, Jamani!

²⁵⁶ Na tazama, Rebeka alipomwona, moyo wake ulijawa sana na furaha. Yeye hakujua alikuwa anaenda kuolewa na nani, lakini kwa imani. Amina! Na—na—na kumbukeni, Yesu ataondoka Ufalmeni, nasi hatutamlaki Utukufuni, itatupasa kumlaki hewani, kati ya mbingu na nchi, ambapo pamepanuliwa kutukomboza sisi. Naye alimlaki Rebeka katikati,

kati ya nyumbani kwa Rebeka na kwake. Amina! Akampeleka nyumbani kwake, akamwoa, na akawa mrithi wa kila kitu alichokuwa nacho babaye. Amina! Ee, kamili, kamili tu. Vema.

Swali: Je, Mungu hutenga mwanamume na mwanamke katika...

²⁵⁷ A—afadhali nisisome hili. Ona, Ona? Ni—ni—huenda nitasema neno fulani. Mwaona? Najua ninyi nyote, lakini haya—haya—haya yanaswa (mwaona?), kwa hivyo afadhari—nisiseme. Ni kitu fulani kuhusu... Mtu yule aliyeliandika, mwajua ni nini; na a—afadhari nikuone wewe kwa mahojiano ya kibinafsi. Ona? Heri nisi—... Sidhani itakuwa vizuri hakika kusoma hili. Ona? Ni—ni vema, mtu yule, hakuna ubaya wote; wao waliuliza swali halali, lakini na—nafikiri ingekuwa vema kwangu kuona hilo kwa mahojiano ya kibinafsi. Sivyo? Ye yote yule... Wajua ndivyo, ye yote yule.

²⁵⁸ Lo, jamani! Ee, tumekwisha pitisha wakati wetu, enyi watu. Heri tu—tumalize tupate kwe—kwenda kwa chakula chetu cha kutwa. Mnataka nisimame—nitumie wakati gani? Jamani! Ni... ni—naam, hebu—labda kidogo tu. Ye yote apaswaye kuondoka upesi sana, usiache chakula chako kiungue. Lakini kama wewe—kama una... Na—na huenda labda nitakula chakula katika Blue Boar, au Pryor, au mojawapo wa mahali hapo, na labda hawatawasumbua. Kama yakupasa kuondoka, Mungu akubariki; nafahamu. Ona? Nami nitachukua karibu... Nitayaweka haya papa hapa, na ni hayo pekee nitakayoyajibu. Kisha ni—nitaenda ku... haya papa... Itakuwa karibu itachukua karibu dakika kumi na tano zaidi, ndipo nitaenda kula.

364. Nina binti wawili walioolewa na watu wa k—i—d—e—nao wanaamini Ujumbe huu. Wao—madhehebu, (Naam), nao wanaamini Ujumbe huu na wamechukua msimamo wao Kwake, nao wamepata... Wafanyeje?— wamepata pingamizi. Tufanyeje?

²⁵⁹ Shikilieni msimamo wenu! Hakika. Onyesheni mliyvo. Naam; usijitolee kwao. La, bwana! Sisemi, msiende kati yao, kushiriki, au kitu kama hicho, mradi tu mnaweza kushiriki; lakini wanapofikia pa kugeuza mlo, mwajua, hua hawezi kula pamoja na kunguru.

365. Ndugu Branham, je, waweza kufafanua Marko 13:27? Pia, Ndugu Branham, na wale watu katika Ufunuo 20:7 na 9, je, nini—watakaofanya vita dhidi ya watakatifu? Wanatoka wapi? Je, kutakuwako kuelea juu kama ilivyokuwa kwa—kwa jamaa ya Nuhu?

²⁶⁰ Ufunuo 13—au la, Marko 13:27, Ndugu Neville. Ufunuo 20. Una Biblia yako pale, Ndugu Capps? Ufunuo 20, na inaonekana kama 7 na 9. Nafikiri mimi, wanapofungua hayo... Hapa, yeye

amepapata papa hapa. Ufunuo, ilikuwa nini sasa? Marko 13:27, 13 na 27.

Ndipo atakapowatuma malaika na... kuwakusanya wateule wake toka pepo mne, na—toka upande wa mwisho wa nchi hata na hata na upande wa mwisho wa mbingu—toka upande wa mwisho wa mwisho wa nchi hata upande wa mwisho wa mbingu.

²⁶¹ Hilo lanena kuhusu ufufuo, kugeuzwa kule, kunyakuliwa. Yeye atawatuma malaika zake kuwakusanya. Je, uliwahi kuwaza malaika ni nini? Enhee? Wajumbe. Yeye atawakusanya pamoja, kuwakutanisha pamoja (ona?), akiwaleta, kuwafunganisha pamoja toka upande wa mwisho wa nchi hata upande wa mwisho wa Mbingu, lile neno ambalo limekwisha kuweko na limedhihirishwa duniani. Ona? Mwafahamu? Neno limekwisha kunenwa, hapa limedhihirishwa. Ona? Vema, Ndugu Capps. Hebu tuone.

Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani ata... funguliwa, atoke kifungoni mwake;

²⁶² Vema. Nimemaliza tu kueleza hayo, sivyo, jinsi yeye angefunguliwa toka kifungoni mwake hiyo miaka elfu moja itakapokwisha?

Vema, nina lingine papa hapa. Ngoja kidogo.

366. Ndugu Branham, ilikuwa ni Mungu, au ni mimi ni niliyejiletea hayo wakati yale mambo yalipotendeka, nilipo (j-a-r-) jaribiwa... Hiyo ilikuwa... (Ona kama unaweza kusoma hilo. Ni mwandiko mzuri, lakini elimu yangu ni haba. Lasemaje hapo? [Ndugu Branham aongea na Ndugu Neville—Mh.] Si—siamini naweza kujibu hilo. Ndugu Capps au siwezi kulisoma... kasema.) Ilikuwa... (Isipokuwa ni...?...Hebu tuseme, kama alikuwa ni muuguzi. Kitu fulani kuhusu uuguzi). Hiyo ilikuwa ya Mungu nilipoacha uuguzi, au ilikuwa kosa langu?

²⁶³ Singejua. Heri nikuone kwa mahojiano ya kibinafsi. Ona?

Sasa, uuguzi ni jambo halali, kama tu muuguzi. Ningesema... Sasa, mtu yule haku-... Sikurudisha tu hilo nipate kusema sitajibu, kwa sababu hilo ni muhimu sana kwa mwanamke yule kama swali lako lilivyo muhimu kwako au kwangu. Ona? Lakini sasa, kama ni—kama ni—mwiuguzi, uliacha tu uuguzi kwa sababu ulidhani tu haikupasi kufanya kazi... Vema, nafikiri uuguzi yapasa uwe kama kitu cha huruma. Ona? Yakupasa uwazie kuhusu kufanya jambo fulani, kama udaktari.

²⁶⁴ Daktari ambaye ni daktari mzuri, angemsaidia mtu bila kujali kama yeye alikuwa na hela ya pesa au la, daktari halisi. Ona? Nami nadhani mhudumu, mtu ye yote, huduma yetu

inapaswa kuwa ya sisi kwa sisi, kwa sababu tunafanya maisha bora sisi kwa sisi.

²⁶⁵ Mimi. . . Wao waliponiambia ilinipasa kuchukua dolla mia kwa juma toka kwa kanisa hili kama mshahara, naam, ilikuwa—ilikuwa karibu kuniva, Sasa. . . Bi. Wilson, najua, na labda mwanawe, na hao wanaoketi hapa, mwakumbuka miaka mingi iliyopita, nilihubiri hapa kwa miaka kumi na saba na sikuwahi kuchukua hata senti moja maishani mwangu. Hata—pesa kidogo yo yote, cho chote ningeliweza kupata, niliweka kwake. Ona? Basi waliponiambia ilinipasa kuchukua ili nipate kuwa katika mikutano hii, ilikuwa karibu kuniangamiza. Ona? Bila shaka, naamini ni sawa, lakini kwangu mimi tu (mwaona?), sitaki cho chote, pesa zo zote, kitu pekee nitakacho ni—ni—urafiki wenu na kupata fadhili machoni pa Mungu.

²⁶⁶ Ni—ninawapenda (ona?), nawapenda, nami nataka kuwa sahihi; nami nataka kuwa sahihi. Na sasa, nawatakeni mnamini mimi; nawaamini ninyi. Na ukija kwangu na swali, nataka niwe mwaminifu kwako. Na kama, ni—ninamwambia ninyi katika Jina la Bwana, nawatakeni ninyi mfanye hasa vile ninavyowaambia mfanye. Msiondoke kwake—hata kidogo, ndipo nafikiri tutaendelea hivyo vema. Ona? Halafu, mengine. . .

²⁶⁷ Na kwa hivyo sasa, kama ni uuguzi. . . Nami nafikiri kama wewe, moyoni mwako kuwa mwuguzi. . . Kila mtu hawezi kuwa mwuguzi. Mwuguzi ni mtu ambaye ni mpole na mwema, lo, nadhani mwuguzi halisi. . . Kama umewahi kuwa mgonjwa hospitalini, au cho chote kile, ukamwona mwuguzi halisi ambaye angekuja na kukufariji, au kitu kama hicho. . .

²⁶⁸ Nilifanyiwa upasuaji kwa ajili—nilipopigwa risasi wakati huo; ilinibidi kwenda hospitalini. Kulikuwa na mwuguzi mzee pale, nilimwita “Achali Tamu,” kwa sababu wao—yeye kila mara alikuwa na achali mdomoni mwake akizila. Ilikuwa hivyo daima. Nami nilikuwa tu mwenye umri wa miaka kumi na minne, na nilikuwa nimepigwa risasi. Naye alikuwa tu mtu mdogo tu haidhuru, naye ange-. . . hiyo miguu iliyopigwa risasi, karibu yote miwili ililipuliwa hivyo, naye angeweka hapa mto na *pale* mto; na kila wakati yeye alikuwa akinisaidia. Nami kila mara nilidhani (nilikuwa tu mtoto)—niliwazia ningemwoa, kwa sababu yeye alikuwa—yeye alikuwa mkarimu na mzuri kwangu. Vema nili-. . . Hilo. . . Mwaona, hilo lamaanisha jambo fulani (ona?) kufanya kitu fulani.

367. Ningependa kuuliza swali. Swali la kwanza:

Je, suruali ndefu na koti za wanawake kulalia. . . (sasa, ngoja kidogo; hebu nilisome. [Ndugu Branham ajisomea mwenyewe swali hilo—Mh.] La, hili litakuwa sawa). **Je, suruali ndefu na koti za wanawake kulalia ni mavazi yanayowapasa wanaume?**

²⁶⁹ Wee, usiniambie hawawezi kukuuliza mengine moto moto. Sijui. Nitawaacha tu mjiamlie hayo. Haikupasi kusimama nazo walipo watu huku umezivaa; ni—ninajua hilo. Kwa hivyo hivyo ingekuwa, lakini katika—katika kwenda kulala si—si—sijui. Itanibidi kuthibitisha hilo pia.

Niliwaambia nitakuwa mwaminifu kama sikujua. Sitatoa maoni yangu kuhusu hilo (vema), isipokuwa unataka maoni yangu binafsi. Kama unataka hayo, nitakwambia. Ona?

Sasa kumbuka, si—si—si—ni—ningekosea maili milioni. Nadhani ingelifaa kuvalia vazi refu la kulalia. Lakini—lakini kama wewe—lakini iwapo wewe... Lakini hiyo ni juu yako. Sasa, siwezi—siwezi kukwambia wewe hilo, kwa sababu singelithibitisha. Sasa, ni—hiyo ni—hiyo ni mimi, si Yeye, kumbuka. Ona?

368. Je ni kosa kukata nywele za mwanamke juu juu?

Naamini tulieleza hayo dakika chache zilizopita (ona?) kwa... nadhani wanaviita—vile vitu vidogo vinavyopepea chini hivi...

369. Ndugu Branham, moja ya zile kanda za? Nyakati Saba Kanisa ilitaja kuwa Yuda alikuwa amehesabiwa haki, ametakaswa. Haya yalikuwa halisi (pale kuna lingine zuri.)—fafanua—tukio— tukio halisi la neema ambalo yeye alipokea? Ulitaja pia kuwa jina la Yuda lilikuwa kwenye kile Kitabu cha Uzima, hata hivyo, tunajua yeye alienda kuzimuni na akapotea. Jina la mtu linawezaje kuwa kwenye kile Kitabu cha Uzima na apotee? Au kwa nini Mungu anaweka jina la mtu kwenye kile Kitabu cha Uzima hali Yeye ajua kuwa mwishowe watapotea?

²⁷⁰ Sasa, hilo ni zuri, sivyo? Sasa, hili lingekuwa zuri. Sasa, nitamtegemea Bwana tu kujibu hili, kwa sababu ninazungukazunguka—ninachunguza-chunguza, samahani. Tazama! Kwanza katika—makanisa yetu, nilitaja kuwa jina la Yuda lilikuwa kwenye kile Kitabu cha Uzima. Sasa, hilo ni kweli. Sasa, tunajua hilo, kwa sababu Yesu aliwaambia wao wote waliotumwa nje (Mathayo 10), kutoa pepo, kuhubiri Injili, wamepokea bure, watoe bure; nao walirudi wakifurahi, kwa sababu pepo waliwatii. Sivyo? Kisha Yesu akawaambia, na aliita majina yao (walikuwa akina nani, wangapi walitumwa); nao wakarudi na Yuda Iskariote ambaye pia alimsaliti Yeye... Ona? Walirudi wakifurahi, kwa sababu pepo waliwatii. Sasa, ona, nia zao zilikuwa baya. Ona? Haiwapasi kufurahi kwa maana wana uwezo wa kumtoa shetani. Ona? Haiwapasi kufanya hivyo, inawapasa kufurahi kwa sababu mmepokea neema ya kutosha kuokolewa. Ona, Ona? Haiwapasi kufurahi... Hivyo ndivyo watu...

²⁷¹ Kwa desturi watu walio na karama ni wale wasiotaka karama. Ona? Paulo alijaribu kutorokea kitu kile, Musa vile vile.

Viongozi wakuu kama hao hujaribu kutorokea kazi ile; wanajua mambo yaliyo mbele yao. Mungu . . .

Ona, ukimchukua mtu ambaye kila mara, “Ee, Bwana, nijaze na nguvu, nami nitaenda nje hapa, nami nitatoa pepo.” Yeye hawezi kamwe kulifanya. Mungu ajua vema kuliko kumsadiki mtu kama huyo. Ona? Yeye hawezi kamwe kufanya hivyo.

²⁷² Ni mtu yule ambaye hataki uhusiano wo wote nalo. Mwaona? Huyo ndiye mtu ambaye Mungu humchukua na kumfundisha kitu fulani wakati mwingine. Mwaona?

Kwa hivyo basi, Yuda alirudi akifurahi, wote wale, kuwa majina . . . Yeye alisema, “Msifurahi kwa kuwa pepo wanawatii; bali furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa katika—katika Kitabu cha Uzima.” Sasa, ukichunguza na kuchukua Danieli pia. Yule . . . Ona?

Kwa sababu jina lako liko kwenye kile Kitabu cha Uzima (kwa sababu liko Mbinguni, jina lako limetambuliwa), hilo bado halimaanishi umeokolewa. Ona? Haujaongoka, hata utakapompokea Roho Mtakatifu. Kumbuka hilo. Umeongoka tu kwa uwezekano. Ona? Huja- . . .

²⁷³ Uki—ukiniuliza nikupe mti mwaloni nami nikupe mbegu ya mwaloni, kwa uwezekano una mwaloni, kwa uwezekano, lakini bado haujakua. Hiyo ndiyo sababu, naamini katika usalama jinsi nifanyavyo.

Kama nina—kama ninakuomba shamba la mahindi, nami naona mahindi yamejitokeza karibu urefu huu, kwa uwezekano, nina shamba la mahindi. Si—bado hayajakua, kitu fulani kingetendeka. Ona?

Sasa, uko njiani mwako kupitia kuhesabiwa haki na kutakaswa hata kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Lakini unapobatizwa kweli na Roho Mtakatifu, wewe uko katika ufalme. Sasa, unasema, “Ndugu Branham, hilo ni kweli?”

²⁷⁴ Sasa, sina wakati sasa ku—kuwapeni ninyi Andiko; yachunguzeni tu mfikapo nyumbani, kwa sababu sijui . . . niani mwangu. Yanipasa nitafute tena hapa katika kamusi yangu ya maneno muhimu kuyapata. Yesu alimwambia Petro, ambaye alikuwa ameokoka na kutakaswa . . . Alimwamini Yesu, akatakaswa. Yohana 17:17, Yesu alisema, “Uwatakase, Baba, kwa ile Kweli; Neno lako ndiyo Kweli.” Na Yeye na Neno ni mmoja. Walitakaswa, kwa uwezekano, kwa ile Kweli, Neno, ile Kweli. Halafu, Yesu alimwambia Yuda—au—au Petro usiku ule aliposalitiwa, Yeye alisema, “Nawe utakapoongoka, waimarishe Ndugu zako —baada ya kuongoka.

²⁷⁵ Mtu yule alikuwa amemfuata Yeye kwa miaka mitatu na jina lake lilikuwa kwenye kile kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, na walikuwa wamewatoa pepo, na kufanya kazi kuu, kuponya, na kufanya kila namna ya . . . alihubiri Neno, na kila

kitu, na bado hakuwa ameongoka. Mnaona lile... Unaelekea uongovuni. Ona?

276 Yule mtoto mchanga ambaye... Tendo linapotendeka kati ya lile—lile yai na shahawa, au ile mbegu... Lakini vinapo... Kwa uwezekano mtoto yule yuko pale tendo lile linapofanywa. Ndipo mwili ule unaanza kuumbika, sehemu ya pili; lakini huyo mtoto mchanga apaswa azaliwe hapa, na ndipo anapokea pumzi na uhai. Bado si pumzi ya uhai. Ukasema, “Lo, ni hai!” la, si hai! Hiyo ni neva zinazorukaruka, misuli. Ona? Mtoto hajapokea uhai hata atakapozaliwa. Na huenda ukaruka na kushtuka-shtuka, lakini wewe bado... Ona, Ona? Yakupasa uzaliwe. Mwajua lile ninalokusudia? Vema.

277 Sasa, sasa, yeye alisema basi chukua... “Ulitaja kuwa jina la Yuda lilikuwa kwenye kile Kitabu cha Uzima, hata hivyo, tunajua kuwa yeye alienda kuzimuni na alipotea. Mtu awezaye, basi, kuandikwa kwenye kile Kitabu cha Uzima na apotee?” Sasa, hebu nipate jambo moja zaidi ndani humu kwa mtu mpendwa.

278 Sasa tazama, Biblia ilisema Danieli alipoona... Yeye—yeye aliandika kile Kitabu cha kwanza cha Ufunuo, Danieli. Na twaona, katika ono lile alimwona Yeye akija kwa Yule Mzee wa siku ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu. Wangapi wanakumbuka wamesoma hayo? Na mlitambua, Yohana katika Ufunuo alifikia kitu kile kile, Ufunuo 1? Na Yeye alisimama pale; nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu, miguu Yake na jinsi ilivyoonekana—Mzee wa siku. Mzee wa siku, hivyo ni kusema, hakuwa na wakati, alikuwa aliye wa Milele. Na Yeye alikuja... Sasa tazama! Na watakatifu walikuja duniani na vitabu vikafunguliwa, na Kitabu kingine kilifunuliwa, ambacho kilikuwa ni kile Kitabu cha Uzima, kitabu kimoja. Walikuja hukumuni, na ile... Yeye alikuja, na pamoja naye wakaja makumi elfu mara kumi elfu. Sivyo? Wakamtumikia, yule Bibi-arusi, yule Malkia wa Mfalme.

279 Nami malkia wako mdogo nyumbani? Yeye hukuandalia wewe chakula. Sivyo? (Ambacho umechelewesha) Lakini yeye—yeye anapokuandalia, hayo ndiyo... Yule Bibi-arusi humtumikia Kristo, lile Neno. “Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno.” Ona? Yeye huhudumu lile Neno kwa yule Mfalme, akidhihirisha lile Neno Lake la ahadi katika wakati ambao Yeye anaishi. Amina! Ahaa, nilisema kitu fulani wakati huo, hamkukifahamu, lakini... .

280 Tazama! Jamani! Hilo lilikuwa nzuri. Ona? Akihudumu katika wakati huo, lile Neno. Sasa tazama! Naye alikuja—yeye akafa, na kumi elfu mara kumi elfu walimjia; na hukumu iliwekwa, na vitabu vilifunguliwa; na Kitabu kingine kilifunguliwa ambacho ni kile Kitabu cha Uzima; nao walihukumiwa hivyo. Ni nani huyo aliyekuja? Yule Bibi-

arusi ambaye haikumpasa kuhukumiwa, Yeye yu huru kwa ule hukumu.

²⁸¹ Kitabu kingine kilifunguliwa ambacho ni kile Kitabu cha Uzima, na wale ambao majina yao yalikuwa kwenye kile Kitabu cha Uzima ilipaswa wahukumiwe kwa Kitabu hicho. Na Yuda Iskariote alikiri kuwa mwamini, na jina lake liliandikwa kati yao kwenye kile Kitabu cha Uzima. Sivyo? Yeye alidai kuwa na Uzima wa Milele. Na jina lake liliandikwa katika kile Kitabu cha Uzima. Kwa hivyo yeye apaswa ku- . . . Naam, yeye hana budi kuhukumiwa basi kuona sababu gani yeye alilihukumu lile Neno la Uzima wakati huo, akaliuza kwa vipande thelathini vya fedha. Wengine huliuza kusudi wapate kuwa Wamethodisti, Wabatisti na kadhalika. Aliuza nafasi yake toka kwenye kile Kitabu cha Uzima. Naye atahukumu—yeye hana budi kuhukumiwa, kusimama pale na ahukumiwe kwa hayo, kwa lile Neno. Ona? Hiyo ndiyo sababu ilimlazimu Yuda kutenda hivyo. Ona? Yuda hana budi kuja hukumuni. Jina Lake lilikuwa kwenye kile Kitabu cha Uzima, lakini hilo halimaanishi yeye ameokolewa. Hana budi kusimama hukumuni.

²⁸² Yule mwanamwali aliyelala atasimama papo hapo chini ya jambo lile lile—jambo lile lile. Tazama, Yesu alisema katika Yohana Mt, 5:24 “Yeye asikiaye Maneno Yangu (hiyo ni kusema yeye ayapokeaye, si yeye asikiaye tu likihubiriwa na anaendelea kusema, ‘Upuzi.’ Ona?) Yeye apokeaye Neno Langu—Yeye asikiaye Neno Langu na kumwamini (si anayejifanya anaamini, lakini aaminiye kweli) Yeye aliyenipeleka (ambaye alikuwa lile Neno) yuna Uzima wa Milele na hataingia hukumuni bali amepita (wakati uliopita) kutoka mautini kuingia Uzimani.” Ona? Naam.

²⁸³ Kwa hivyo Yuda aliandikwa jina lake kwenye kile Kitabu cha Uzima (ndivyo hasa), lakini yeye alihukumiwa, kwa sababu yeye alifanyaje? Yeye aliua haki yake ya mzaliwa wa kwanza.

Esau alizaliwa katika jamaa yenye ahadi ya Mungu. Mwana wa kwanza ndiye aliyekuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza. Wangapi wajua hilo? Kwa ahadi ya Mungu, jina la Esau lilikuwa kwenye kile kitabu kwa ajili ya ile haki ya mzaliwa wa kwanza (sivyo?), lakini yeye aliibadilisha kwa ajili ya mchuzi wa mboga mwitu—au mbaazi. Akiwa njaa ya kujaza tumbo lake, tikiti ya kujipatia riziki yake, yeye alipoteza haki ya mzaliwa wa kwanza kwa ajili yake ya riziki zake na hangepata mahali pa kutubia.

²⁸⁴ Wale wapelelezi walioenda na—kule kupeleleza nchi ile, walikuja na hata wakala zabibu ambazo Yoshua na Kaleb walarudi nazo. Hata hivyo, walifanyaje? Waliuza haki yao ya urithi.

²⁸⁵ Yesu alisema—au Paulo akinena kwa kutiwa pumzi na Kristo katika Waebrania ile sura ya 6: “Maana wao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washiriki wa roho Mtakatifu, na

kuonja zile Nguvu za zamani zijazo; wakianguka, haiwezekani kufanywa upya tena hata wakatubu, kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu, na kuihesabu ile damu ya agano, ambayo walitakasiwa kwayo, kitu bure, na kufedhehi ile kazi na neema. . .” Haiwezekani mtu huyo akarudi.

²⁸⁶ Wao, kila mmoja wao isipokuwa Yoshua na Kaleb, walikufa na kuangamia katika jangwa hilo, ingawa wao walikuwa waamini, ingawa majina yao yalikuwa kwenye vile vitabu.

²⁸⁷ Na hapo, Paulo akinena, mtu afikiapo mahali ambapo yeye amekolewa, na kutakaswa (ile Damu hutakasa; Waebrania 13:12 na 13 yasema ile Damu hutakasa), na ndipo wakafikia papo hapo kwenye lango la ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kwa ajili ya sifa au dhehebu ahakataa kuingia, kasema, “Mtu yule amepotea na hawezi kuokolewa” (ona?); maana yeye amefedhehi hata ile kazi ya neema iliyomwita hata mahali hapo na kumwonyesha, kisha akageuka, aiondokee. Yeye aihesabu ile Damu ya agano ambayo alisulubiwa kwayo—Kristo alisulubiwa kwayo kama kitu kiovu. Kwa sababu ile Damu iliyomwoko, na kumhesabia haki, na kumtakasa yeye inamleta hata kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na ndipo aondoka na kuiacha. . .

²⁸⁸ Sasa, tazama mfano huo. Nachukua wakati mwingi, lakini tazama! Yuda Iskariote alifuata nyayo hizo. Yeye alihesabiwa haki kwa kumwamini Bwana Yesu kisha akamkubali Yeye kama Mwokozi wake binafsi. Yeye alitakaswa na akapewa nguvu kutoa pepo; jina lake likaandikwa kwenye kile Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Lakini ilipofikia Pentekoste na kwa ule ubatizo wa Roho Mtakatifu, ule utimilifu wa Neno, yeye alionyesha alikuwa nani hasa. Ndivyo hasa wale wapelelezi walioenda Kanaani walifanya: hivyo ndivyo hasa Esau alifanya.

²⁸⁹ Hivyo ndivyo hasa Shetani alivyomfanyia Hawa katika ile bustani ya Edeni: “Hakika Mungu hata. . .”

Lakini Hawa alisema, “Mungu alisema. . .”

Yeye alisema, “Naam, najua ilisema *hayo*; najua ilisema *hili*, lakini hakika. . . Ona, jambo lile lile kote kote, na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi.

²⁹⁰ Kanisa limeanguka kupitia Kuhesabiwa Haki, Martin Luther; kupitia kwa Utakaso, Wesley. Lakini wakati, inapofikia wakati wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, wanaonyesha walivyo hasa; hawataki uhusiano wa wote nao. Nazarini, Pilgrim Holiness, Church of God, hao wote pale wanaoamini utakaso, huwezi kuwaelekezea kidogo; ni kweli. Lakini inapofikia mpakani, kwenda moja kwa moja hadi mahali pale kumpokea Roho Mtakatifu kwa ajili ya kuzaliwa mara ya pili, ndipo shetani atafanyaje? Anakuja pale na kujaribu kuifarakanisha. Ee, yeye ana—yeye atafanya kila awezacho kuwafanya watu wasiingie mle.

²⁹¹ Walipitia kando na kusema, “Yakupasa unene kwa lugha. Yakupasa uwe na mwamsho. Yakupasa ufanya *hili*.” Huna budi uzaliwe ndani yake. Usiache mtu ye yote akwambie kuwa kutakaswa na Roho Mtakatifu ni kitu kile kile, kwa sababu sivyo! Hakika sivyo!

Msikize huyu Mnazarini nyuma kule akipaza sauti, “Sivyo.” Ona? Yeye ajua kuna tofauti ndani yake, kwa sababu ni—Ndugu Capps, Ndugu yetu hodari. Ona?

²⁹² Hakika, Nazarini. . . Hakuna ye yote awezaye kusema neno dhidi yao watu wazuri wa kidini; ni wazuri tu wawezavyo kuwa. Church of God, Nazareni, Methodisti Huru, watu wale ni halisi, lakini inapofikia kwa ile kazi ya Roho, wao husema, “Ee, ee, huyu ni shetani.” Na wanafanyaje pale? Kukufuru Roho Mtakatifu. Wanapofanya hivyo. . .

²⁹³ Sasa, kukufuru ni nini? Hakuna msamaha. Sivyo? Yeye aliyekwisha kupewa nuru, na kufanya mshiriki na kuonja kipawa cha kimbinguni (kuojeshwa—kuonja utakaso wa Mungu; kusafishwa toka kwa sigara, na wanawake wachafu, na kila namna ya maisha kama hayo)—na kuonja vitu vya kimbinguni (kuona kuwa wanatembea hadi kwa huo mpaka kama hao wapelelezi walivyofanya waliokula sehemu ya zabibu zile. . . Lakini wao wapaswa kufanya nini? Ilipasa wavunje dhehebu lao kuingia katika hili. Ona? Tuseme—Ona?)—kuonja karama za kimbinguni; kwa kuwa wao wanamsulubisha upya kwa nafsi zao wenyewe Mwana wa Mungu, na kuihesabu ile Damu ya agano ambayo walitakasiwa kwayo kitu kiovu.

²⁹⁴ Utakaso ni wakati jina lako linaenda kwenye kile kitabu kama mwamini. Neno lako—jina lako limeandikwa katika Damu Yake. Ona? Utakaso hufanya hilo; na unakuja, Yeye anapokuamini umbali huu, kisha unainuka na kusema, “Vema, Yeye aweza kujua hivyo.”

²⁹⁵ Naam, Yeye alijua, Yeye alijua hungelifanya hivyo tangu mwanzo. Yeye alijua Yuda hangelifanya hivyo. Yeye alimjua tangu mwanzo; yeye alikuwa mwana wa uharibifu. Lakini mambo hayo hayana budi kutimizwa. Ona? Lile Neno halina budi kutimia, ijapokuwa kwa mifano na vivuli. Jamani! Tugedumu kwa hilo kwa masaa kadhaa.

370. Ndugu Branham, ulipotoa ule ujumbe unaohusu majuma sabini ya kanisa—majuma sabini (samahani.) ya Danieli, naamini kuwa ulitaja kuwa lile juma nzima—lile juma nzima la mwisho au ile miaka ya saba mwisho itanza Bibi-arusi atakaponyakuliwa.

²⁹⁶ La, la, la, la, la, hasha, hasha, hasha! Ulilipata kwa kosa (ona?), si majuma saba yote. Lile—lile juma lilianza Yesu alipokuja duniani. Yeye alisema, “Masihi, Mtawala, atakuja na atahubiri, na katikati ya yale majuma saba, Yeye atakatiliwa mbali.” Na Yesu alihubiri kwa miaka mitatu na nusu, ambayo ni

nusu ya yale majuma sabini, zile siku saba, juma—siku za juma. Ona? Na kuna miaka mitatu na nusu iliyosalia.

²⁹⁷ Sasa, Eliya na Musa wajapo duniani, ambayo ni Ufunuo na Zekaria. . . (Ndugu Coomer lako—lako na swali la Dada Coomer pale lilikuwa—lilikuwa vivyo hivyo.) Sasa, wao watakapo- . . . Zekaria 4 na Ufunuo 11, hiyo mizetuni miwili na kadhalika—ambayo ni Musa na Eliya—watakapokuja duniani wanatabiri siku 1,264. Ni nini? Ni miaka mitatu na nusu hasa. Hayo yalikuwa kitu kile kile hasa. Si . . . Ona? Sijui huyu mtu mpendwa ni nani. Limeandikwa—limeandikwa vizuri sana, kwenye karatasi iliyo na maandishi makubwa ya kidini—kichwa cha maneno hapa na kadhalika, na ni nzuri mno. Na ni swali nzuri sana, lakini (ona?) hukufahamu, yale tu niliyosema. Sijawahi kamwe kuamini kuwa majuma yote sabini yangukuwa upande huu. Masihi amekatiliwa mbali. Wangapi wanakumbuka mahubiri hayo juu hapa? Hakika! Ona? Majuma saba.

371. Tangu wakati huo, inaonekana kama miaka mitatu na nusu ilitimilika katika ile huduma (Vema, hapa umelipata sahihi hapa.) ya—ya Yesu, lakini matamshi yale “katikati ya majuma” yaonekana yanahusu yule tu mpinga Kristo kuvunja agano lake na . . . (La, huyo mpinga Kristo atavunja agano lake mwishoni mwa ile miaka mitatu na nusu ya mwisho. Ona?) Kama nilivyolewa ule ukanda wa Danieli, yale majuma sitini na tisa ya kwanza yalikuwa wakati Yesu alipopanda punda akiingia Yerusalemu A.D. 30, ili ile miaka mitatu na nusu ya huduma yake ingehesabiwa katika yale majuma sitini na tisa; na yale majuma yote ya mwisho—na lile juma nzima la mwisho au miaka sabini bado ingetimizwa na inganzia katika Wakati wa kunyakuliwa. Tafadhali eleza hili dhahiri kwangu.

²⁹⁸ Wajua, Ndugu, Dada, ye yote aliyeuliza swali hili. Sawa (ona?), lakini naamini ulitatanishwa kidogo na yale niliyosema. Ona? Sasa, ile— Yesu alipoingia Yerusalemu (hilo ni sawa hasa), huo ulikuwa mwisho wa . . . Ona? Yeye alienda moja kwa moja toka pale na kusulubishwa. Ona? Naye—Yeye alitabiri kwa nusu ya juma la sabini ambayo ni miaka mitatu na nusu. Sasa, Yeye alikatiliwa mbali, na nafsi Yake ilifanywa dhahihu. Na sasa, kungekuja basi. . . Katika hizi siku za mwisho, kuna miaka mitatu na nusu ambayo bado imeahidiwa Wa—Wayahudi. Na ile—katika—katika wakati huu kulikuwa na kukusanyika kwa watakatifu kwa ajili ya kule kunyakuliwa, lile Kanisa.

²⁹⁹ Sasa, sitayamaliza haya yote, Ndugu—Ndugu, Dada.

372. Je, waweza kufafanua I Wakorintho sura ya 7, kifungu cha 1 na 9? (ifungue Ndugu Neville, I Wakorintho, sura, 7, kifungu cha 1, sasa).

373. Je, kila mwamini wa kweli atafanya kazi zile Yesu alisema, kama ilivyotajwa katika Yohana Mt 14:12 (Sivyo hasa. La!):

kuponya wagonjwa, kutoa pepo, kufufua wafu. (Sidhani hayo yako katika Injili ya Yohana 14, lakini ni sawa. Ni Marko 16); **au—au—hili ni la Eliya pekee? Sharti mwamini kufanya hayo yote—au haya—yule ambaye kweli—aminiye kweli kweli? Na kama yeye yu mwamini halisi, je, yeye atafufua wafu na kufanya miujiza mikuu?**

³⁰⁰ Sasa, hilo ni kati ya waamini. Ona? Kila mtu hana karama hizo, na halimaanishi tu kuwa ni mtu mmoja atakayefanya hayo; kutakuwa na makundi ya watu. Kama kwa mfano, vipi kama—kama tungekuwa na msichana mdogo hapa kanisani, au mvulana mdogo, au mtu fulani tunayempenda sana, na uhai uwatoke. Kanisa lote lingekusanyika pamoja, nao wangeomba na kufunga; “Bwana, mrehemu mtoto huyo.” Ona? Mungu angemfufua.

³⁰¹ Wangapi wamewahi kusoma kile kitabu kiitwacho *Makasisi wa Nikea* na vinginevyo? Mwajua, hivyo ndivyo walivyofanya katika lile kanisa la mwanzoni. Wangukusanyika pamoja, mwajua, na hata kufufua mchungaji wakati mwingine na mambo kama hayo, kama Mungu aliona lafaa kutendwa, lakini wao walilifanya.

374. Kama kanisa limeokolewa hata ijapokuwa halitanyakuliwa, kama ninavyoamini wewe ulitufundisha linapaswa kupitia katika ile dhiki kutakaswa. Lakini itakuwaje basi kwa hawa waliokufa, watatakaswaje?

³⁰² Vema, wale waliokwisha... Bibi-arusi hahitaji kutakaswa; amekwisha takaswa. Na wale ambao—ambao—ambao wamekufa nyuma kule, hao watakaopitia... Ona? Hawakupokea Nuru ambayo kanisa hili juu hapa limepokea; waliishi chini ya Kuhesabiwa Haki, Kutakaswa, na mambo kama hayo. Waliishi kwa ile Nuru waliyokuwa nayo. Labda katika—katika njia ambayo—waliteseka, na yo yote yale waliyopitia, na mateso yao... Lakini sasa, katika huu wakati wa kunyakuliwa kama huu (ona?), kutakuja wakati sasa ambapo huyu bibi-arusi ata—aliyekataa sehemu ya Kichwa ya yule Bibi-arusi—atapaswa kuteshwa kwa kukataa kwake, kwa sababu Injili ile haikudhihirishwa kwao nyuma kule, kama ilivyodhihirishwa kwenu siku hizi. Ona? Mnaiona dhahiri mno. Mmekwisha kuwa na miaka hiyo yote na mifano, zile Mihuri zimefunguliwa, zile Nyakati za Kanisa zimeelezwa, na kila kitu hivyo. Ni dhahiri mno hamwezi kulikosa. Ona? Ndiposa, mkikataa kabisa, kuna jambo moja pekee la kufanya, kuteseka kwa ajili yake.

³⁰³ Je, ulipata hilo Ndugu Neville? Vinahusiana na nini? Ni—heri mimi—heri niende sasa, kwa sababu inachelewa sana. Mwaona? Saba—saba, tisa... Hebu tuone.

Lakini ikiwa hawawezi kujizuia, na waoe; maana ni afadhali kuo kuwaka tamaa.

³⁰⁴ Vema. Hilo ni kwa ajili ya maisha mabovu. Badala ya mwanamume, mvulana, msichana, au ye yote yule wanapoenda pamoja na—na wanajua kuwa wao wapaswa kuonana, basi oaneni. Nafikiri ninyi—ninyi mngeelewa lile nakusudia, sivyo? Ona? Usiishi maisha machafu pale, kwa sababu si sahihi. Mwaona? Kwa upande mmoja, huyo ni dada yako, kama wewe ni Mkristo. Sasa, kama ni ulimwengu, ni ulimwengu: mbwa hula mbwa. Lakini msichana huyo unayeenda naye, huyo ni dada yako pia. Huyo atakuwa mama ya watoto wa—wako watakaokuja. Usiishi maisha machafu pamoja naye, mwonyeshe kuwa wewe ni Mkristo halisi muungwana. Ishi jinsi impasavyo Mkristo mwungana. Ona? Na mtendee kama dada yako, kisha mtakapooana, endelea kumtendea hivyo.

³⁰⁵ Huenda nikajibu hili hivi sasa. Siamini katika maisha machafu kati ya Wapentekoste, watu wa—utakatifu, hata ingawa wameoana. Siamini hilo. La, bwana! Baadhi ya mambo haya machafu ambayo—ambayo ni ya kuogofya mno... Mimi huja ndani humu wakati mwingine kwa haya... Si asubuhi hii sasa, lo, sisemi hayo. Lakini namaanisha katika nyakati ambazo mimi niko California na mahali mbalimbali kama hapo. Nakutana na wahudumu kule ambako kwa upambanuzi, najisikia kama ningaliwapandisha gotini mwangu na kuwapa “Injili kidogo ianzishayo msisimuo wa uhai” Naam, bwana! Lo, kumwona mwanamume ambaye angemchukua mkewe mpendwa, na mchafu, mtovu wa uadilifu, hilo ni... Mwafahamu ninalomaanisha? Nafikiri yakupasa uaibike kama mtu wa Mungu ku-. . . Wewe kuwa tu mume; kuwa mpenzi. Mheshimu kama ulivyomheshimu daima. Usivijali hivi, baadhi ya hivi vitabu, visivyo vya kizinzi—au upuzi huu katika hivi vitabu vya kizinzi, na mambo mnayoyasoma, na upuzi huu wote, na vitu kama hivyo. Ondoa upuzi huo mawazoni mwako.

³⁰⁶ Biblia ilisema, usiache hata usemi mmoja mchafu utoke kinywani mwako unapokiri utauwa. Mtendee maskini bibi huyo kama kwamba yeye ni mpenzi wako. Kama yeye ana umri wa miaka sitini, uwe tu vivyo hivyo. Uwe huyo mpenzi mwanamume shujaa; kumbuka, ndivyo ulivyo.

Usijaribu yo yote ya mambo haya mapya, nami najua kuwa ninaongea... Na uwe tu mume, ndugu halisi, Mkristo halisi.

Najua hilo laonekana... Lakini ile... Ninyi mu watoto wangu. Nina haki ya kuwaambieni yale ninayotaka kuwaambia ninyi. Mwaona? Ninyi mu watoto wangu; ishini ipasavyo.

³⁰⁷ Nanyi wanawake, ishini ipasavyo kwa waume zenu. Nanyi waume, ishini ipasavyo kwa—kwa—kwa—kwa wake zenu. Iweni wema sana, na heshimianeni tu na... Na uhusiano we—wenu wa jamaa na mambo kama hayo, hebu uwe na kicho, na wa kumcha Mungu, na unaokubalika kati yenu na kila kitu kama kiwezavyo

kuwa. Msisukumane kamwe, na kububurushana, na—na kuwa wachafu na watovu wa uadilifu.

³⁰⁸ Fahamikianeni, ongea na mkeo. Kama—kama una tabia moja naye ana nyingine, ongea hayo naye. Ja—jaribu kufanya jambo lile lile kwa mumeo, Dada. Na vivyo hivyo. . . Fahamikianeni na uwe—uwe Mkristo mwungwana halisi na bibi Mkristo halisi, na—na ndugu na dada ninyi kwa nyinyi. Kila mara kumbuka, ninyi ni watoto wa Mungu, nanyi mnatoka kwa Jamaa ya Kifalme. Ninyi mna damu ya kifalme; hakuna damu bora ulimwenguni kuliko yenu. Na hiyo ni kweli! Na damu ya kifalme hujionyesha yenyewe. Hivyo ndivyo ilivyo, ni ya kifalme. Wote wanaoamini hilo semeni, “Amina!” [Kusanyiko unaitikia “Amina! —Mh.] Naam, bwana! Onyesha jinsi ulivyo. Mimi ni—mimi ni mwana wa Mfalme, Mimi ni mwana wa Mfalme. Mke wangu ni binti ya Mfalme. Ningemtendeaje huyo binti Mfalme? Yeye angemtendeaje huyo mwana wa Mfalme? Mwaona ninalomaanisha. Iweni halisi kabisa.

375. Je, kutakuweco na mwenendo wa Roho Mtakatifu, ishara, na maajabu, na miujiza zitakazofanywa na Bibi-arusi kabla Yeye hajanyakuliwa, au tunangoja tu kule kuja Kwake?

³⁰⁹ Sina budi kufungia kwa hili, nadhani, kwa sababu ninayo mengi sana hapa ya kufikia. Na kunachelewa sana. Ni saa saba kasoro dakika ishirini sasa, nami nina karibu nina thelathini au arobaini yayo hapa, labda. Nitajibu hili vizuri wakati wangu—ni—nitachukua tu dakika tatu zaidi. Nitajibu haya niwezapo. Ona? Sijui nitayapata lini; nitafanya niwezavyo. Je, mnayafurahia? Nina. . . Yananisaidia mimi pia. Ona?

Kuja hapa na kuyanyakua hivi, kabla hata sijayatazama (mwaona?), unapata mambo mengine ambayo huwezi kuyajibu, na—na mimi—mimi nilikuwa na matumaini ningechukua. . . Najua kuna moja ndani humu kuhusu ule uzao wa nyoka. Nilitaka kulifikia sana; nilitaka kulieleza. Ona? Lakini nafikiri sikulipata, kwa hivyo itanipasa tu ku-. . . Labda Bwana hataki ifanywe hivyo, lakini lilikuwa kuhusu ule uzao wa nyoka. Asije mtu fulani kwenye ukanda huo aka—akasema, “Vema, yeye alifanya—yeye aliruka hilo.” Wangapi watanistahimili dakika mbili zaidi kwa hilo? Enhee? Vema.

³¹⁰ Sasa ngoja, hebu nipate hili kwanza. Hebu tuone! “Je, ile—ile. . .La. Swali hili hapa ni: “Je, kutakuwa na miujiza itakayofanywa na Bibi-arusi?” Naam, bwana! Inafanywa hivi sasa. Hiyo ni kweli! Ona? Lakini usitazamie kitu fulani kikubwa—au kushusha mbingu na kufunga mbingu, kusinyeshe. Hilo linawaendea wale—wale Wayahudi sasa. Ona? Hilo halihusu hili kamwe; hilo ni Musa na Eliya kwa Wayahudi, si Kanisa hili kwa vyo vyote vile. Soma zile sura za kwanza tatu za Ufunuo; unapata kile kanisa lilivyo papo hapo. Ni hayo tu kwa kanisa.

Na hilo litakaporudi pamoja na Bibi-arusi, litakaporudi pamoja na . . . Soma . . . Ukitaka kujua kuhusu lile Kanisa, yanayolihusu, soma Ufunuo sura za kwanza tatu, kisha ruka hadi ile sura ya 19 na anza kusoma toka pale . . . ? . . . unampata yule Bibi-arusi. Mengine yote ni kwa Wayahudi pale.

³¹¹ Sasa, kwa ule uzao wa nyoka. Siwezi kulipata humu ndani, kwa sababu (mwaona?) mna chungu nzima yayo. Lakini mtu yule alisema, “Kama yule nyoka—kama ule uzao wa nyoka (ona?) . . . Yule mwanamke, yeye—yeye alimpata mtoto mwanamume kwa Bwana, yeye alisema hivyo.”

Vema, naamini Jumapili iliyopita, nilieleza jinsi, huyo alivyompata kwa Bwana. Kama alimpata kamwe, yeye alimpata kwa Bwana (Ona?), kwa sababu ilipasa aje toka kwa Bwana. Kwa sababu sheria za Mungu zina-. . . Zitam-. . . Zitamtii Mungu. Hakika.

³¹² Yeye aliagiza ya kwamba jua liangaze; jua hung’aa. Yeye aliagiza kwamba mvua itanyesha juu ya wenye haki na wasio haki; hufanya hivyo. Na mbegu zikipandwa katika shamba lo lote, au ni nzuri au ni baya, zitamea; ni mbegu. Kama mbegu zimepandwa, haidhuru . . .

Na njia pekee nyoka angepanda mbegu ile, yeye alikuwa ndiye mnyama pekee aliyemfuatia mwanadamu. Kwa maana katika yale mageuzi yanayoendelea ya uzao wa mwanadamu, wakati—Mungu alipoatimia dunia. Naye akaanza kuzaa ndege, na wale—toka kwa ndege Yeye akafikia vitu mbalimbali, ndipo sokwe, na toka sokwe hadi kwa nyoka.

³¹³ Sasa, Yeye aligeuza nyoka yule hivi kwamba (ambayo ilipasa ifanyiike) hata ingefarakanisha kizazi hiki, kinachojaribu kupata mifupa inayofanana na namna ya mnyama fulani aliyekuwa nusu mwanadamu na nusu mnyama), kusema hapo ndipo mwanadamu . . . Wamelipoteza toka kwa sokwe; ila tu sokwe hana busara. Sokwe hana nafsi; yeye hawezi kuwazia. Yeye tu ana . . . Yeye—yeye aweza . . . Ke—kelele tu, naye aweza . . . Farasi, “hii,” “hoo,” au kitu fulani kama hicho . . . Mbwa, “Njoo hapa, Fido, fanya hila fulani. Ruka juu!” . . . Na kupanga mawe na mambo kama hayo, na matendo; hayo, wanafanya hivyo kwa mwamsho, kwa kusikia, na mambo kama hayo, na matendo; lakini kuwazia na kufahamu, hawawezi. Hawajui wako uchi, hawajui wa kiume na wa kike, ile tofauti, hivyo. Hawana taratibu za mambo kama hayo . . . ? . . . Ona? Hawawezi. Mwanadamu ndiye pekee.

Na aliyemfuata mwanadamu alikuwa yule nyoka. Biblia ilisema yeye alikuwa ndiye mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu. Mwerevu, yeye—yeye—yeye alikuwa karibu awe na nafsi. Yeye alikuwa na mahali kwa ajili ya nafsi, lakini yeye alifanyaje? Aliiua kwa Shetani kumdanganya Mungu—kujaribu kufanya hivyo. Wangapi wanalipata umbali huo?

³¹⁴ Shetani, yule nyoka, karibu alikuwa na nafsi. Mungu alijua wangetafuta mifupa hiyo, na hakuna mfupa ndani ya nyoka unaofanana na wa wanadamu. Yeye alikuwa . . . Hiyo ndiyo laana yake. Yeye alisimama wima kama tu mwanadamu.

³¹⁵ Tazama, ndipo uzao huo, ambao ulikuwa unaofuata uzao wa mwanadamu . . . Shetani mwenyewe, yule roho, alijua kuwa hiyo ilikuwa ndiyo mbegu pekee ambayo ingemtia mimba huyo mwanamke, kwa sababu sokwe hawezi. Wameichanganyisha na mengineyo; haiwezekani. Lakini yeye alijua kuwa kiini cha uzima kilichokuwa ndani ya sokwe, hakingeingia kwenye eneo la mwanamke—lile yai; lakini yeye alijua mbegu ya yule nyoka ingefanya hivyo, kwa hivyo yeye akamshughulikia huyo nyoka.

³¹⁶ Na Adamu alikuwa hajajua kamwe—kamwe tendo hili lingefanywa. Ona? Yeye alifanywa mwanamke. Bila shaka, yeye angelilifikia hilo baadaye; lakini mwaona, ule uenyezi wa Mungu kujidhihirisha kama Mwokozi na—na kadhalika, kama nimekwisha kueleza wakati mwingi. Lakini Shetani alijua hili, maana yeye alimjia katika mfano wa nyoka, ambaye alikuwa mnyama na—mnyama, na kamjia. Naye akadungwa mimba na Shetani kwanza.

³¹⁷ Na kama mtatambua, yalifanywa matendo mawili tu, kisha wakazaliwa watoto watatu. Chunguzeni Maandikoni. Yeye alizaa mapacha. Mmoja wao alikuwa mzao wa nyoka, yule mwingine alikuwa Habili. Yeye alimdanganya mumewe na kumwambia . . . Ona? Ndipo yeye alimwonyesha mumewe ilikuwa nini, na ndipo mumewe pia akaishi naye, naye akamzaa mtoto huyu. Nami nawatakeni ninyi—kuonyesha, yeye alipata mimba ya mapacha kwa wanaume wawili mbalimbali . . . Yeye alikuwa . . . Huyu ni mwanamke bikira.

³¹⁸ Mbegu yao ina nguvu. Tazama hapa kwa mfano. Ibrahimu alimwoa dada yake. Naam, mwanamume akimwoa dada yake siku hizi, watoto wake wangukuwa baradhuli. Ona? Lakini mwanadamu . . . Na hapa Yakobo au—au Isaka alimwoa Rebeka ambaye alikuwa binamu yake, binamuye halisi, uhusiano wa damu (ona?), mtoto wa ndugu ya Ibrahimu.

³¹⁹ Tazama, tazama, sasa, kwa hili (ona?), kuna—ule uzao wa mwanadamu ulikuwa na nguvu mno. Sasa, ukichunguza kila wakati imekuwa mapacha kote. Kulikuwa na . . . Kaini na Habili walikuwa mapacha, na Esau na Yakobo walikuwa mapacha. Yesu na Yuda walitoka kwa kabila lile lile na kanisa lile lile. Na ile—hata Roho Mtakatifu na yule mpinga Kristo watakuwa mapacha, “Zitafanana sana hata ingewapoteza walio Wateule, kama yamkini.” Mmelifahamu? Vema.

³²⁰ Sasa kuthibitisha hili, ninataka mchukue Yuda kile—naamini kile kifungu cha 17—au kifungu cha 14 cha Yuda na kusema . . . Sasa, sasa, tazama hili. Sasa, nitafunga. Tazama. Kufupisha jambo lote na kulithibitisha, kwanza Yeye alisema,

“Nitaweka uadui kati yako na uzao wa huyo nyoka.” Ona? Sasa, mwanamke hana mbegu. Kwa hivyo, jinsi alivyopata mzao huyu alikuwa mzao wa Shetani. Kaini alikuwa mwana wa Shetani. Mwanamke hakuwa mbegu, kwa hivyo aliipata kwa kujuana kimwili. Na alipotenda hayo, alipewa hiyo na adui wa Mungu. Ndiposa, Mungu alipompa Mzao, haikuwa kwa kujuana kimwili kamwe. Mwalifahamu? Mwanamke mjakazi na mtoto wake walifukuzwa, kwa sababu hawatarithi pamoja na aliye mwungwana kwa mtoto wake.

³²¹ Basi tazama, ndipo yeye akapewa Mzao ambaye alikuwa Kristo. Wala yai lake. . . Sasa, Waprotestanti wanataka kuamini kuwa ni damu iliyozaliwa kibikira, hiyo ilikuwa Damu iliyoumbwa na Mungu ambamo kile kiini cha uhai kilikuwa, lakini wakasema ilikuwa yai lake. La, bwana! Yai hilo haliwezi kuingia kupitia kwa bomba hilo kuingia katika tumbo la uzazi isipokuwa kuwe na mwamsho. Ndipo unamweka Mungu na Ro—Roho wakijuana kimwili na mwanamke. Inawezekanaje kufanyika? Kitu hicho chote kilikuwa kimeumbwa na Mungu, lile yai na ile mbegu.

³²² Yeye alikuwa Mwana wa Mungu, si mwana wa Mariamu, maana hakumwita Mariamu mama, kamwe. “Mwanamke,” Yeye alimwita hivyo, wala si mama. Yeye hakuwa mamake. Ilikuwa Mwana wa Mungu, na Mungu ni Mmoja. Mwafahamu?

³²³ Sasa, jambo lingine kulithibitisha hili na kulihakikisha, ambapo kama ye yote akibishana nawe, rudi nyuma hapa kwa Kitabu cha Yuda, nadhani ni sura ya 17 (kile kifungu cha 14 au cha 17), yeye alisema, “Sasa, Henoko. . .” Mnataka mimi nilisome? Mna wakati mwingi hivyo? Hebu—hebu tu—na ndipo nitapata. . . Ndipo nitajua, kwa sababu kanda zile hapa zinaendelea, nasi—sisi huenda tukalitatanisha katika—katika hili sasa. Hebu nione kama hii ni. . . Kifungu cha kumi na nne:

. . . Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu,

³²⁴ Sasa, rudi katika sura ya 5 (nadhani ni hapo) ya Mwanzo, kisha nenda pia, katika Kitabu cha Luka (laiti ningelipata, nililiandika chini hapa—laiti ningelipata ndani humu) na utatambua katika orodha ya vizazi hivi, hakuna po pote katika Biblia. . . Kama. . . Tazama! Kama Nuhu—kama Henoko ni mtu wa saba toka kwa Adamu, Biblia ilisema, “Adamu kisha mwanawe Sethi,” kwa sababu Kaini hakuwa mzao wa Adamu. Ilisema Adamu alimzaa Sethi, na Sethi akamzaa. . . Yaredi; Yaredi akamzaa, kuendelea hadi kwa Henoko; na Henoko alikuwa wa saba toka kwa Adamu. Hakuna po pote ambapo paliwahi kunena kuwa Kaini alihebiwa kuwa cho chote katika ukoo wa Mungu.

³²⁵ Sasa, tazama tu uone kama ndivyo au sivyo; itafute. Na Luka aja hapa na kuirudia kuitaja tena, na akiaanzia kwa Adamu. Hakuna wakati mmoja ambapo Kaini anatajwa huko kote. Na kama Henoko (ona?) alikuwa wa saba toka kwa Adamu, Kaini aliingilia wapi? Kwa sababu Biblia ilisema hivyo ule ukoo, kuwa Adamu alimzaa mwanawe, Sethi. Na Sethi akamzaa Yaredi, na Yaredi akamzaa *Fulani*, na kuendelea; na hakuna wakati hata mmoja ambapo Kaini aliwahi kutajwa. Basi yeye hangelikuwa mwana wa Adamu. Kwa hivyo yeye alipaswa kuwa mwana wa nyoka, naye hangekuwa mwana pasipo kujuana kimwili. Amina! La, sivyo, alizaliwa kibikira, ndipo yeye angalikuwa mwana wa Mungu. Si—sitaki hao watoke kwa hilo wakati mmoja.

³²⁶ Sasa, Mungu yule yule aliyefunua hayo, ndiye Mungu aliyeniambia kuhusu ndoa na talaka. Yeye asemapo mambo hayo, Ndugu yangu, Dada . . . Mimi ni ndugu yenu, mwanadamu. Lakini Yeye asemapo hayo, na hilo lagonga mle ndani, siwezi kulieleza kwenu. Hakuna haja kwangu kujaribu kufanya hivyo, kwa sababu singeweza. Lakini halijawahi kamwe kukosea wakati mmoja. Ijapokuwa, singeliliona mimi mwenyewe kwa vyo vyote vile, singeliliona, lakini nalishikilia tu; kisha Yeye anaanza kulifunua, ndipo nili—lanitupa sakafuni. Lilikuwa papo hapo, nami sikuliona. Elimu yenu—yenu imerukwa, na mawazo yako yamerukwa, na cho chote kile; vivyo hivyo Kaini alirukwa.

Sasa, kama tungelikuwa na wakati kurudi nyuma hapa katika Mwanzo na kuanza kusoma . . . Hebu tuone kama ningelilichukua na kulipata nyuma hapa. Sijui kwa kweli kama—kama ningeweza au la. Bi. Wood, unakumbuka nilipokuwa nakuonyesha hilo majuzi? Yale tu . . . je, hiyo ilikuwa sura ya 5? Ile ya 5, enhee. Vema.

Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku ile Mungu alipoumba mtu, kwa sura ya Mungu . . . alimfanya:

Mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.

Adamu akaishi miaka mia-na thelathini, akamzaa . . . wana—na akamzaa—akamzaa mwana kwa sura yake, na—na kwa mfano wake; akamwita jina lake . . . (Kaini? Alimwitaje jina lake? Yuko—yuko wapi yule kifungua mimba aliyekuwa na ile haki ya mzaliwa wa kwanza basi? Hakutajwa kamwe. Sethi ndiye aliyekuwa mwanawe).

³²⁷ Sasa, tunarudi hapa tena nasi tunapata ambapo ilisema . . . Na sasa, Hawa alipewa mwana mwanamume, kwa sababu Kaini alimwua Habili. Sasa tazama tunapoendelea:

Siku za Adamu baada ya—Na Adamu akaishi miaka mia na thelathini, akazaa mwana kwa sura yake, kwa mfano wake, akamwita jina lake Sethi.

Si—siku za Adamu baada ya... kumzaa Sethi zilikuwa miaka mi—mia nane, akazaa wana, waume na wake.

Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mi—mia kenda na—na thelathini, naye akafa.

Sethi akaishi miaka mi—mia na mitano, akamzaa Enoshi... (Na kuendelea hadi kufikia chini kule, naye ni wa saba, Henoko ni wa saba toka kwa Adamu.)

Sasa, sikumbuki tu ni wapi katika Luka. Umetia hilo alama pia, Bi. Wood? Yeye na mimi... Nilikuwa nikimwonyesha hivi majuzi pale katika... Wasemaje? [Ndugu Branham aongea na Dada Wood—Mh.] Naamini uko sahihi, Dada Wood. Tulitia alama mle katika kitabu chake ambacho tulikuwa—Biblia yake nilipokuwa nikimwonyesha... Liko hapa, naam, ule ukoo. Naam.

³²⁸ Sasa, kama tutatambua hapa... Katika ile sura ya 3 ya Luka tunapata kitu kile kile. "... wana gani na kadhalika... na Nuhu, ambaye alikuwa wa Lameki, ambao pia walikuwa wana wa Methusela, ambaye pia ni mwana wa Henoko, ambaye alikuwa mwana wa Yaredi, ambaye alikuwa mwana wa Mahalaleli, ambaye alikuwa mwana wa Kainani, ambaye alikuwa mwana wa Enoshi, aliyekuwa mwana wa Sethi, aliyekuwa mwana wa Adamu, aliyekuwa mwana wa Mungu." Kaini aliingilia wapi? Kaini yuko wapi, yule kifungua mimba? Mweye ile haki ya mzaliwa wa kwanza; yeye angetokea wapi? Yeye alikuwa mzao wa Shetani, na si wa Mungu. Wala hakuwa wa Adamu, kwa sababu jina la mwana wa Adamu lilikuwa—lilikuwa Sethi. Kaini, yule mzao wa nyoka, alimwua mwanawe wa kwanza ambao ni mfano na kivuli cha yule nyoka pia kumwua mwanawe mwingine, Yesu. Na Sethi akapachukua mahali pake katika ule ukoo, ambalo lilimaanisha ufufuo, ya kwamba vizazi vya Mungu vingendelezwa kabisa.

³²⁹ Nataka kuona mtu fulani akimweka ndani mle sasa na kusema hakuwa mzao wa nyoka. Hakutabuliwa katika ukoo wa Mungu, wala katika ukoo wa mwanadamu, ukoo wa Adamu, na vingine vyote. Sivyoy? Wangapi wanaamini hivyo, semeni, "Amina!" [Kusanyika waitikia, "Amina! —Mh.] Hakika. Yeye hakuwa; yeye alikuwa mzao wa nyoka na si mzao wa Adamu!

³³⁰ Hawa alisema alikuwa mwana wa Adamu. Hakuwa mwana wa Adamu. Yeye alisema, "Nimepata mtoto mwanamume kwa Mungu." Naye ilimpasa ampate hivyo, alikuwa mzao. Alikuwa mzao, lakini mzao wa nyoka. Ona?

³³¹ Naye ilimpasa arudi kwa kuzaa kwa bikira ili atakase huko kuuwana kimwili ambako kulikuwa kumefanywa. Adamu aliwekwa hapa duniani, lakini yeye ange—yeye hangetambua kamwe kuwa yeye alipaswa kuwa baba. Mwafahamu ninalomaanisha? Shetani akijua hili, yeye alimwendea Hawa

kabla Adamu hajafika pale. Na hapo ndipo jambo lote lilipo siku hizi. Na ndugu, hilo ndilo lifanyalo ndoa na talaka na mengine yote farakano kubwa hivyo kama yalivyo siku hizi. Ni la kuhuzunisha mno. Ona? Lakini mimi. . . Mungu amefanya njia, ambayo kwayo twashukuru.

³³² Je, mwampenda? Si Yeye ni wa ajabu? Sasa, je, uzao wa nyoka ni kweli? Nilidhani labda mtu fulani kwenye kanda ange—huenda akawazia niliogopa kulitatua. Mwaona? Kwa hivyo wangesema, “Sababu gani yeye aliliruka mara mbili. Yeye anaogopa kulijibu.” Sisi hatuko hivyo. Mradi tu Bwana, yu ndani yake, hilo ni sahihi.

Mwajua, kama vile nilivyosema ya kuwa nilimtaazama tai akitayarisha mabawa yake, mwajua. Nami niliwaza, “Je, haunilogopi.” Nilikuwa—bunduki yangu ikikaa nje pale, nilisema, “Ningekupiga risasi.” Yeye alijua singempiga risasi; nilikuwa mbali sana na bunduki hiyo. Nilisema, “Je, huogopi?” Yeye alipepesa macho yake makubwa na kunitazama. Kuchakulo mdogo ameketi pale akilia, “Cha, cha, cha, cha, cha; nitakurarua vipande, nitakurarua vipande!” Yeye hakumjali kuchakulo huyo, lakini alichoka kumsikiza. Kwa hivyo baada ya kitambo kidogo, yeye alipigapiga mabawa yake mara moja, akaenda hivyo, na akatandaa mabawa yake. Naye alijua jinsi ya kupeperusha mabawa hayo, akapuruka asionekane tena. Ona? Nilimwona tu yeye akiwa kitu kidogo hivyo, chembe ndogo tu.

³³³ Ndugu Fred, naamini nilikuonyesha wewe. Nilimwona Ndugu nyuma kule sasa, yeye aliposhangilia “Amina!” muda mchache uliopita. Ni—ninaamini nilikuonyesha wewe mahali pale kule juu, na Ndugu Wood, ko kote uliko, kule juu sana mlimani juu kule, ambako hayo yalitukia. Nilimwona yule tai. Ni. . . Yeye alisukumwa chini na hiyo tufani, nami nilikuwa nimesimama nyuma ya mti huu.

³³⁴ Nilikuwa nikiwinda kulungu (na kuendelea baadaye), na ilikuwa mwezi wa Oktoba, na theluji na vinginevyo. Ndugu huyu hapa alikuwa juu pale mwisho wa mwaka uliopita pamoja nasi, Ndugu John na kwengineo, juu pale kwenye kilele kiitwacho Corral ndipo alipokuwa.

³³⁵ Nilisimama pale, nami nilisimama nyuma ya mti huu. Theluji ndogo na mvua kidogo, nami nilikuwa tu nimesimama pale. Tai yule amesimama pale, naye alilazimika kushuka. Yeye alipaa juu pale, ndege anayeonekana mkubwa, mkubwa mno, tai mkubwa wa hudhurungi. Akaketi juu pale na kutazama hapa na pale, niliwazia, “Vema. . .” Nili—nilikuwa na wakati wa furaha te—tele. Nilikuwa nikipaza sauti, “Bwana asifiwe! Haleluya!” Nilikuwa nikizunguka na kuzunguka na kuzungukazunguka kichaka kile, nikipiga shangwe hivyo. Nilitazama kule chini; ningesikia huyo mbwa mwitu akibweka. Mwajua wabwekavyo.

336 Mwaka uliopita kule chini, wakati—kabla tu haijaanza kunyesha, wangeanza kubweka; alikuwa mbwa mwitu mdogo, mwajua. Napenda tu kuyasikia.

337 Ndipo ningesikia kulungu upande huu wakisema, “Weeee hooo” [Ndugu Branham anaiga kulungu—Mh.] jinsi wafanyavyo. Na juu pale mwenziwe amwitikia. (Juma lijalo, juma baada ya lile lijalo, nitawawinda. Bwana akinijalia.) Kwa hivyo basi, niliposikia hayo juu kule, ee, ni kitaua sana kuwa juu pale. Ee, ni—ni. . . Hilo—hilo ni kanisa langu la jimbo kule ambako naongea na Yeye, kisha nashuka hapa na kuongea nanyi. Ona?

338 Na mle ndani, ee, ni ajabu mno, kustarehe tu. Nikisimama pale, niliwazia, “Ee, Mungu. . .” Nilitazama, ndipo mvua ile ikanyesha, na mimea isiyokauka ilikuwa imejawa na barafu, na upinde wa mvua ulienea kuzunguka hicho kilele cha Corral hata ukafikia Mlima wa Sheep, juu *hivyo*, kuuzunguka *hivyo*. Nami niliwazia, “Ee, Mungu, tazama pale, Uum,” Niliwaza, “Wewe uko hapa Alfa na Omega, mwanzo na mwisho. Hapa yaja chini hapa, pale. Ni wewe yule jana, leo, na hata milele, zile Nyakati Saba za Kanisa, vile Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu. Wewe uko, Mungu, Wewe u wa ajabu jinsi gani.”

339 Nami nilikuwa nikipiga shangwe tu, nikaweka chini bunduki yangu; na kuuzunguka ule mti huku nikipiga shangwe, “Mungu atukuzwe! Bwana asifiwe,” nikizunguka na kuzuunguka mti ile hivyo. Nilikuwa tu na wakati wa furaha pale peke yangu, mimi na Bwana tu peke yetu, mwajua.

340 Baada ya kitambo kidogo tai yule akaja kutoka kwenye hicho kichaka na kunitazama mimi. Niliwaza, “Vema, hupendi hilo?” Nilisema, “Wee, jamani, ninamwabudu Mungu yule yule aliyekuumba wewe.” Ona? Yeye aliopesa tu macho yake makubwa ya kijivu na kunitazama mimi pale, huku nami nikipaza sauti hivyo.

341 Maskini kuchakulo mdogo, wa mlimani (kwa ye yote aliyewahi kuwinda milimani, yeye—yeye ni askari wa mwitu), naye aliruka pale (maskini mnyama mdogo, si mkubwa kutosha kukufanyia cho chote, lakini ee, kelele jinsi gani)—naye akaruka juu pale, akiruka juu chini, mwajua, “Yaa, yaa, yaa, yaa, yaa, yaa—yaa, yaa, yaa, yaa, yaa, yaa,” akaendelea tu hivyo.

342 Na yule tai alikuwa akimtaazama; yeye angenitazama mimi. Niliwaza, “Lo, Bwana, vema, Wewe ungenikomeshaje kwa kitu kama hicho?” Ona? Nilisema, “Kwa sababu, Wewe wajua, nilikuwa ninakuabudu Wewe. Je, wataka nione kitu fulani kwa tai huyo?” Nilisema, “Nitamchunguza, au ni juu ya huyo kuchakulo wa msunobari?” Nilisimama pale na kuwatazama; niliwaza, “Nitawachunguza kidogo.” Nilisema, “Jambo moja niliona kwake, yeye hakuwa mwoga.” Napenda hilo, si mwoga. Yeye alisimama pale, huyo ndege mkubwa mno; Nilisema, “Wajuaje?” (Bunduki yangu ilikuwa imewekwa juu

pale kuegemea mti). Nilisema, “Wajua ngingekupiga risasi?” Yeye alijua bora kuliko hilo; yeye alijua jambo moja; singempiga risasi; nilimpenda sana. Ona? Ndiye amesimama pale, na hakuogopa hata kidogo.

³⁴³ Nami niliwaza, “Ngingekupiga risasi.” Sasa, nilimwona yeye; yeye angenitazama mimi pale hivyo. Naye aliendelea kutengeneza mabawa yake, mwajua, kuyarudisha nyuma. Mwajua jinsi wafanyavyo hivyo, mabawa yao, mwajua. Mabawa makubwa mno karibu urefu *huu*, mwajua, naye alikuwa ndege mkubwa. Yeye alikuwa ameketi pale, nami nilimtaazama. (Hiyo ilikuwa nyuma kule kabla sijajua mambo haya; hiyo ilikuwa miaka na miaka mingi iliyopita, labda miaka ishirini iliyopita.)

³⁴⁴ Nami nilimtaazama; baada ya kitambo kidogo nilimwona yeye. Nilidhani “Yeye yu nani—yeye...” Yeye haogopi, kwa hivyo napenda hilo. Lakini nini lililo la kiungu sana kuhusu maskini tai huyo mzee?” Nilipoona huo mdomo ngumu uliopindamana, mkubwa, mno, umejitokeza hivyo, na hayo macho makubwa, niliwaza, “Wee, yeye ni ndege halisi.”

³⁴⁵ Sasa, hakuna ye yote... Mwewe, kama angevunjika—vunjika. Hakuna cho chote kiwezacho kumfuata. La, la! Ingehitajika eropleni kufanya hivyo. Naam, bwana! Hakuna ndege awezaye kumfuata, kwa hivyo—yeye hupaa juu sana. Ndiposa, yeye ana macho; yeye aweza kuona moja kwa moja hadi ardhini pia, yeye akiwa juu pale, anaweza kuona mbali sana.

³⁴⁶ Sasa, Yehova alifananisha manabii wake na tai (mwaona?); Yeye alikwisha kuwainua juu hivyo. Ilipasa waumbwe kimaalum. Hebu tuone. Kuchaguliwa tangu awali, kuzaliwa kwa kusudi hilo (ona?), kuinuliwa hivyo. Kisha wewe... Ya nini kwenda juu kule kama huwezi kuona uliko? Ona? Inafaa nini kuenda juu pale kama hujui kile unachofanya? Ona, ona?

³⁴⁷ Inakufaa nini kuruka juu chini, kupiga shangwe, kunena kwa lugha kama hujui yote ni ya nini? Ona, ona? Yakupasa kufahamu unapokuwa kule. Ona?

³⁴⁸ Kwa hivyo basi, nilimtaazama yeye, mwajua, yeye alipozunguka pale. Niliendelea... Nilimpenda tu; yeye alikuwa ndege mzuri mno. Hata hivyo, yeye labda angekula baadhi ya nyama zangu za paa na kadhalika ambazo nina... Nilimtaazama, na baada ya kitambo kidogo niliwaza, “Wajua, nini—yeye ana...”

³⁴⁹ Baada ya kitambo kidogo akachoka. Sidhani yeye alichoka kwa kunitazama, lakini nadhani yeye alichoka kusikiza maskini kuchakulo huyo mzee aliyeketi juu pale. Mwajua, tunao wengi mno wa hao kambini siku hizi. Mwajua? Ona? “Cha, cha, cha! Siku za miujiza zimekwisha! Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hamna vitu hivi tena!” Ona? Maskini kuchakulo wa kale waliofungiwa duniani wanaoketi pale juu ya gogo hilo. “Yakupasa uwe wa *hili*. Sisi tuna—sisi tuna—sisi ndio lile...”

Ona, ona? Wameketi pale wa—wakiruka juu chini. Ee, yeye alikuwa akitikisatikisa, yeye alikuwa akitetemeka sana.

³⁵⁰ Akachoka kusikiza hayo, naye alifanya mruko mmoja mkubwa mno, na kutikisa sana tawi lile likatikisika, hivyo, naye akatoka nje. Ona, yeye alipigapiga mabawa yake na kufanya njia kwenye hiyo miti-mbao pale. Naye alipofanya hivyo, nilimtaazama. Ona? Yeye hakuogopa, kwa sababu angesikia ule uwepo wa mabawa aliyopewa na Mungu. Yeye alijua mabawa hayo yangemwinua juu ya hatari yo yote. Ona?

³⁵¹ Na kwa hivyo, hivyo ndivyo tunataka kujisikia. Hili ni Neno, na Yeye yule aliyeandika Neno ndiye Mabawa yangu. Siogopi Neno lile; litakuinua wewe moja kwa moja kupitia aina yo yote ya shida zilizoko. Ni Upanga utakaokata njia moja kwa moja kupitia humo. Msiwe na wasiwasi juu yake. Ona?

³⁵² Sasa, nikatambua wakati huo. Yeye yeye aliyatandaa tu. Ona? Na hilo—kila wakati upepo ulipoingia, yeye angeinuka Juu tu, kupaa Juu zaidi na zaidi.

Nilisimama pale, na kukunja mikono yangu, na kumtaazama hata akawa tu tone ndogo ikawa vigumu kumwona tena. Nami niliwaza, “Mungu, ndivyo. Si tu jiunge na *hili*, na kukimbia kujiunga na *hilo*, na kufanya *hili*, *hilo*, au *linginelo*; ni kutandaa tu mabawa yako (ona?); kujua jinsi ya kutanda mabawa yako ya imani katika Neno la Mungu, na uelee mbali na upunzi huu wote wa kupayapaya hapa na kupayapaya pale.” Naam! “Mbingu na nchi vitapita, bali Neno langu halitashindwa.”

³⁵³ Sasa, nina karibu ishirini yenu tena jinsi hii. Sasa, ninyi mlilo kwenye hiyo ni kusema—mahojiano jioni hii, naam, mwoneni Billy, kwa sababu nafikiri watajaribu kuanza mapema kidogo nipate kuwaingiza wote ndani. Nikiweza, nataka kupata kila mmoja wao ambaye nitaweza. Na nilifanya hili, si kwa sababu... Billy hakujua hili (ona?), lakini akili zangu zilizunguka-zunguka sana baada ya karibu maono ishirini ndani mle asubuhi hii (mwaona?) hata—au cho chote kile... inakuingiza tu... Naye Billy alisema, “Mbona usitoke nje upate... Pumzika, toka nje, na ujibu baadhi ya maswali hayo pale.”

Nami nikasema “Ndugu Neville ana ujumbe wake.” Kasema, “Nitamwambia.” Yeye akaenda huku.

Ndugu Neville kasema, “Njoo!” Kwa hivyo basi, niliinuka na nikaja hapa. Na wengine wao wanangoja jioni hii. Nasikitika niliwakawisha hapa hadi saa saba, lakini nita—nadhani yanipasa kuondoka kesho kutwa, kwa hivyo—kurudi tena Arizona.

³⁵⁴ Kumbuka, Bwana akipenda, wakati ujao nitakaporudi, nataka kuhubiri kuhusu kuwahubiria juu ya—kuwaonyesha ninyi katika Maandiko usahihi wa ndoa na talaka. Hili... Ndiposa, nita... Halafu, kuiacha tu i-... Nieleze jinsi ilivyo

hasa, ndipo mtafahamu tangu sasa. Kwa hivyo hadi wakati huo, iweni na moyo wa ushujaa. Bwana awabariki sana sana. Je, twaweza kusimama? [Unabii unatolewa na mwanamke fulani katika kusanyiko—Mh.] Bwana asifiwe.

Nampenda, nampenda, (Nanyi je?)
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

³⁵⁵ Mwampenda? Sasa, hebu na tusalimiane kwa mikono sisi kwa sisi, tunapimba tena.

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

³⁵⁶ Ee, si hilo ni la ajabu? Ee, lo! Billy alinitaka nitangaze, kuwa baada ya dua ya kutakia heri, yeye ana neno la kuwaambia ninyi watu hapa mnaotaka haya mahojiano ya kibinafsi. Mwaona? Yeye ataka kukutana nanyi kwa dakika chache. Lakini najisikia sasa hivi, muda mfupi tu wa kuabudu. Hawa- . . . Je, si mnappenda kumwabudu Yeye katika Roho?

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

³⁵⁷ Ee, si ni la ajabu? Ee, ni—ninampenda Yeye. Moyoni mwangu ninampenda, kama naujua moyo wangu. Naamini hata nanyi pia. Kwa hivyo pamoja sisi tu watoto Wake. Tunapendana. Sasa, siwezi kumpenda Yeye pasipo kuwapenda ninyi. Na kama nikisema kuwa ninampenda Yeye nami siwapendi ninyi, Biblia ilisema, mimi ni mwongo. Ona? Na kama nina . . . Kama mnataka—kama mlitaka kunipenda mimi au kupenda jamaa yangu . . . Chaguo lilikuwa, ninalotaka ninyi mfanye, mnipende au mpende jamaa yangu; mpende jamaa yangu, ningefurahiwa kama mngalimpenda Billy Paul kuliko kunipenda mimi. Kama ikifikia chaguo la kuamua la namna hiyo, ningefurahiwa mkifanya hivyo. Nawatakeni mnisikize, kwa sababu Billy si mhudumu. Lakini nataka mnisikize mimi, yale ninayowaambia; lakini wakati—ukitaka kumpenda mtu fulani, kuwapenda sana, useme, “Nataka nimpende mmoja wenu, wewe au Billy,” mpende Billy. Ona? Mungu ajisikia vivyo hivyo kutuhusu sisi. Nasi hatuwezi. . . Ndipo najua kuwa huwezi kumpenda Billy pasipo kunipenda mimi, kwa sababu yeye ni sehemu yangu. Ona? Kwa hivyo siwezi kumpenda Mungu pasipo kuwapenda ninyi, kwa sababu ninyi ni sehemu ya Mungu. Nasi tunapendana. Ee, nadhani ni ajabu mno. Je, hamwoni kwamba nyimbo ni kitu kizuri baada ya kupata haya—kujibu maswali haya, ambayo yanatuweka katika mbano? Enhee, enhee, lo halisi mno.

Nampenda, Nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.
Ee, walitoka mashariki na . . .



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org